ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR
MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Rashid Seif Suleiman	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ziwani.
9.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa

11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa
12.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Gando
13.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Kuteuliwa.
14.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Jang'ombe
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la Makunduchi
18. Mhe. Shawana Bukheti Hassan	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/ Jimbo la Dole
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu

22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka
23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake
29. Mhe. Mohammed Said Mohammed	Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/ Jimbo la Mpendae
30.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
31.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
32. Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa
33.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
34.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
35. Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
36.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake

37. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
38.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
42.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
43.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
44.Mhe. Hamad Masoud Hamad	Jimbo la Ole
45.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
46.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
47.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
48.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Jimbo la Bububu
49.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
50.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
51.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
52.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni
53.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
54.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	Jimbo la Kiembesamaki
55.Mhe. Marina Joel Thomas	Kateuliwa na Rais
56.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa	Jimbo la Mkwajuni
57.Mhe. Mgeni Hassan Juma	Nafasi za Wanawake
58.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma	Jimbo la Bumbwini

59.Mhe. Mohammed Haji Khalid Jimbo la Mtambile

60.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad Jimbo la Chambani

61.Mhe. Mussa Ali Hassan Jimbo la Koani

62.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali Jimbo la Uzini

63.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa Nafasi za Wanawake

64.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi Nafasi za Wanawake

65.Mhe. Nassor Salim Ali Jimbo la Rahaleo

66.Mhe. Omar Ali Shehe Jimbo la Chake-Chake

67.Mhe. Panya Ali Abdalla Nafasi za Wanawake

68.Mhe. Raya Suleiman Hamad Nafasi za Wanawake

69.Mhe. Rufai Said Rufai Jimbo la Tumbe

70.Mhe. Saleh Nassor Juma Jimbo la Wawi

71.Mhe. Salim Abdalla Hamad Jimbo la Mtambwe

72.Mhe. Salma Mohammed Ali Nafasi za Wanawake

73.Mhe. Salma Mussa Bilali Nafasi za Wanawake

74.Mhe. Salmin Awadh Salmin Jimbo la Magomeni

75.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman Nafasi za Wanawake

76.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha Jimbo la Mwanakwerekwe
77.Mhe. Subeit Khamis Faki Jimbo la Micheweni
78.Mhe. Suleiman Hemed Khamis Jimbo la Konde
79.Mhe. Ussi Jecha Simai Jimbo la Chaani
80.Mhe. Viwe Khamis Abdalla Nafasi za Wanawake
81.Mhe. Wanu Hafidh Ameir Nafasi za Wanawake

Ndugu Yahya Khamis Hamad Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Ishirini na Nane - Tarehe 23 Julai, 2013

(Kikao Kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika, (Pandu Ameir Kificho) alisoma Dua

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2013/2014 - Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe hoja iliungwa mkono jana ikimaanisha kwamba sasa tuanze mjadala. Kwa maana hiyo naomba sasa nimkaribishe Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari.

Mhe. Mlinde Mabrouk Juma (Mwenyekiti wa Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari): Mhe. Spika, naomba kutoa maoni ya Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari, kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kwa mwaka wa fedha 2013/2014.

Mhe. Spika, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi mungu mwingi wa rehma kwa kutujaalia kufika hapa tukiwa wazima na wenye afya njema pamoja na kunijaalia mimi nguvu ya kusoma maoni ya Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari juu ya makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo kwa mwaka wa fedha 2013/2014.

Mhe. Spika, naomba pia uniruhusu kuipongeza Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo. Pongezi hizi zimuendee Waziri wa Wizara hii, Naibu Waziri, Katibu Mkuu wake, Naibu Katibu Mkuu pamoja na watendaji wote wa Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo kwa mashirikiano yao walotupatia kipindi chote wakati Kamati ilipokutana nao mpaka leo tunawasilisha maoni ya Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari juu ya makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo kwa mwaka wa fedha 2013/2014.

Mhe. Spika, kabla ya kuendelea mbele, naomba niwashukuru Wajumbe wanaounda Kamati hii, kwa mashirikiano yao pamoja na fikra ambazo zimenifanya leo niwe nawasilisha maoni ya Kamati hii. Naomba niwatambue Wajumbe hao kwa kuwataja majina kama ifuatavyo:

1. Mhe. Mlinde Mabrouk Juma - Mwenyekiti
2. Mhe. Abdalla Mohammed Ali - Makamo Mwenyekiti
3. Mhe. Asha Bakari Makame - Mjumbe
4. Mhe. Kazija Khamis Kona - Mjumbe
5. Mhe. Amina Iddi Mabrouk - Mjumbe
6. Mhe. Asaa Othman Hamad - Mjumbe
7. Mhe. Mussa Ali Hassan - Mjumbe
8. Mhe.MohammedrazaHassanaliMohamedali- Mjumbe
9. Ndg. Maryam Hussein Rajab - Katibu
10. Ndg. Abubakar Mahmoud Iddi - Katibu

Mhe. Spika, utakubaliana nami kuwa gharama za maisha na utendaji zimekuwa zikipanda maradufu kila mwaka ambapo katika bajeti ya Wizara hii, utaona kuwa kuna baadhi ya taasisi Bajeti iliyoombwa kwa mwaka huu wa fedha 2013/2014 haina tofauti sana na bajeti iliyoidhinishwa mwaka wa fedha unaomalizika yaani 2012/2013.

Mhe. Spika, kwa kufanya hivi ni kutokutenda haki kwa baadhi ya taasisi. Tufahamu ya kuwa gharama za maisha na utendaji kwa mwaka jana haziwezi kuwa sawa na mwaka unaofuata. Hali ya kiuchumi duniani sote tunaijua kuwa haitabiriki *(not stable*). Kamati inashauri ni vyema inapofanywa ukomo wa bajeti yaani *ceiling* suala hili liangaliwe kwa undani zaidi kwani linaweza kupelekea kutokutekelezeka kwa baadhi ya malengo ambayo Wizara imejiwekea.

Mhe. Spika, baada ya utangulizi huo, naomba nitumie wasaa huu kutoa maoni ya kamati kwa utaratibu huu.

Shirika la Magazeti

Mhe. Spika, Shirika la Magazeti Zanzibar kwa muda mrefu sasa wamekuwa na kilio kikubwa cha kukosa mtambo wa uchapishaji. Inafahamika kwamba Shirika limekuwa likizalisha magazeti ya Zanzibar Leo, Zanzibar Leo Jumapili na Zaspoti lakini uchapishaji wa magazeti hayo unafanyika Tanzania Bara ambapo asilimia 71 ya mapato ya gazeti yanatumika katika uchapaji. Kamati inapendekeza Shirika kutengewa fungu kwa ajili ya ununuzi wa mitambo ili kuondokana na kadhia wanayoipata. Naamini Waziri atakubaliana na Kamati yetu na kulishajihisha suala hili kwani kwa kuwa na mitambo yetu

wenyewe Shirika litazalisha ajira mpya na fedha zitakazopatikana zitabaki hapa Zanzibar kwa mantiki hiyo zitawanufaisha Wazanzibari.

Mhe. Spika, kamati imetilia shaka Fungu lilotengwa kwa ajili ya malipo ya mishahara ya Wanyakazi wa Shirika la Magazeti. Fungu hilo ni kubwa sana na maelezo yake hayajairidhisha Kamati.

Shirika la Utangazaji Zanzibar (*ZBC*)

Mhe. Spika, ni jambo la kutia moyo kuona Shirika la Utangazaji limeingia katika mfumo wa digitali. Kwa msingi huo, nchi yetu sasa imekuwa ikienda sambamba na mabadiliko ya teknolojia ya dijitali. Majaribio ya urushaji wa matangazo ya dijitali yameonekana kuwa na mafanikio ambapo kuanzia mwezi wa Februari mwishoni, wananchi wamekuwa wakifaidika kwa kupata huduma za matangazo hayo. Ni jambo la kumpongeza Waziri na watendaji wake kwa kuhakikisha kuwa Zanzibar hatuachwi nyuma kimaendeleo. Lakini pia Kamati inatoa ushauri kwa watendaji wa Shirika la Utangazaji Zanzibar kubadilika kiutendaji na kuacha kufanya kazi kwa mazoea *"business as usual"* kwa kuwa uendeshaji wa Mfumo wa digitali unahitaji umakini wa hali ya juu. Kwa kutokuwa kwao makini tutakuja kulaumiana na kuona ni bora tungelibaki katika mfumo wa analogia. Na tukumbuke kuwa serikali/nchi imetumia fedha nyingi kuingia katika mfumo huo.

Mhe. Spika, wengi wetu tunaamini kuwa mawasiliano ni kitu muhimu sana katika jamii hii yetu ya leo. Wakati Kamati ikipitia bajeti ya Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo imeona kuwa Shirika la Utangazaji Zanzibar halijatendewa haki kabisa. Shirika limetengewa jumla ya Tsh 2,100,000,000/- ambapo kwa mwaka 2012/2013 Shirika liliidhinishiwa 2,016,224,000/-. mtakubaliana nami kwamba kiasi cha fedha hizi kwa kuzisikia utaona ni nyingi sana lakini kiutekelezaji fedha hizi ni kidogo sana ukilinganisha na malengo ya Shirika lilojiwekea. Kwa mfano, kwa mwaka ujao wa fedha Shirika limepanga kuweka vifaa vya dijitali na linki katika studio za redio Unguja na Pemba, kuandaa na kurusha hewani vipindi maalum 52 katika maeneo makuu manne ambapo vitahusu maendeleo ya Zanzibar katika kipindi cha 50 baada ya Mapinduzi ya 1964.Tujiulize kwa vipesa hivi kweli Shirika litaweza kujikwamua katika hali iliyopo sasa na kukidhi haja ya wananchi.

Mhe. Spika, nasema hivi simaanishi kwamba tuvunjike moyo bali tujidhatiti katika hili "mfumo wa uendeshaji wa digitali si mchezo hata kidogo" unahitaji uelewa, mipango na utaalam wa hali ya juu kabisa.

Kamisheni ya Utalii

Mhe. Spika, Kusema kweli fedha zilizotengwa kwa ajili ya Kamisheni ya Utalii Zanzibar ni ndogo, ambapo tumeipa Kamisheni majukumu yaliyo yake na yale yanaliyokuwa yakifanywa na Shirika la Utalii Zanzibar. Huwezi kuutangaza utalii aidha kitaifa ama kimataifa kama huna mfuko ulio imara. Mheshimiwa Spika tukitaka kujikwamua kutoka katika dimbwi la umaskini ni busara kutilia mkazo suala la Utalii Zanzibar.

Mhe. Spika, kwa mazingira ya Nchi yetu, tunategemea utalii katika kuongeza pato la taifa letu ambapo Utalii unachangia pato la taifa takriban asilimia 27 katika uchumi na unachangia asilimia themanini za fedha za kigeni yaani *Foreign Exchange Earning*. Kwa maana hiyo, ikiwa taifa letu linategemea sekta ya utalii kama chanzo cha mapato ni vyema basi sekta ya utalii ikatizamwa kwa jicho la huruma ili yale yalokusudiwa yaweze kufikiwa.

Mhe. Spika, sekta hii ina majukumu ya kuimarisha na kuongeza wigo wa vivutio vya utalii pamoja na kutangaza utalii wa Zanzibar kitaifa na kimataifa. Kama tupo makini basi tufahamu ya kuwa Fedha nyingi sana zinahitajika kwa ajili ya kuutangaza utalii wetu.

Mhe. Spika, tukiwa sote hapa tunafahamu kwamba utalii ni chachu ya maendeleo na nchi nyingi duniani zimenufaika na utalii kama vile *Seychells* na Mauritius ambapo wamekuwa wakiendesha utalii wa kitajiri. Lakini hata majirani zetu Kenya ambao kwa sasa wamekuwa wakiingiza watalii wengi na sekta hiyo kunufaisha taifa lao. Kwa upande wetu Zanzibar kama suala la utalii hatujaliwekea mikakati iliyo imara basi sekta hii itakuwa kichochoe cha umaskini badala ya kuwa chachu ya maendeleo.

Mhe. Spika, Kamati inatoa rai kwamba Dhana ya utalii kwa wote itekelezwe kwa vitendo na wala si maneno. Ukiangalia Nchi kama India ambayo imepiga hatua kubwa sana kwa kuutangaza utalii kwa wananchi wake, ambao wamekuwa na muamko mkubwa katika suala hili na kupelekea kuiingizia India pesa nyingi. Kinyume na nchi yetu ambapo pesa nyingi zinatokana na watalii kutoka nje. Kamati inaomba kuwekwa sera na sheria ambazo zitapunguza gharama kwa wazawa. Mfano mzuri, Tanzania bara wamepunguza gharama katika mbuga za wanyama na kuwashajihisha wanachi kutembelea mbuga hizo. Kwa kufanya hivyo, wameweza kuwavutia wanachi waliowengi kwa kuwa gharama walizowawekea ni ndogo ambapo hata mtu wa kawaida anaweza kumudu.

Mhe. Spika, ni jambo la kushangaza kuona kuwa nchi za Afrika hazifahamu kama Zanzibar ina vivutio mbalimbali vya utalii. Nitatolea mfano wa baadhi

ya Wanachi wa Namibia ambao waliuuliza kama Zanzibar kuna vivutio vya utalii. Kwa hali hiyo, Kamati inaishauri Wizara kujidhatiti katika kuutangaza utalii yaani kufanya *"aggressive marketing and advertisements"* kwa nchi jirani, Afrika na duniani kwa ujumla. Ila kufanya hivyo kunahitaji fedha za kutosha, hivyo tunaiomba Serikali kuona kuwa sekta hii inaipa kipaumbele cha pekee.

Mhe. Spika, Kamati ina kubali pia kuna changamoto mbalimbali wanazokabiliana nazo Kamisheni ya Utalii. Hata hivyo, Kamati inatoa ushauri kwa taasisi hii, kutumia Balozi zetu zilizopo nchi mbalimbali katika kuutangaza utalii wa Zanzibar.

Mhe. Spika, fedha ilopangwa kukusanywa na Kamisheni ya Utalii Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2013/2014 ni bilioni moja, mia mbili na mbili milioni (1,202,000,000) ambapo ni sawa na fedha ilopangiwa Kamisheni kukusanya mwaka 2012/2013. Kwa hali hii, watendaji wa Kamisheni wanatuvunja moyo, kweli basi fikra za watendaji hao zimeshindwa kubuni pahala pa kuongeza pato hilo na kutupa angalau matumaini ya ongezeko baina ya mwaka jana na mwaka huu wa fedha.

Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale

Mhe. Spika, Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale pamoja na majukumu mengine, majukumu yake ya msingi ni kuenzi, kuhifadhi na kuendeleza historia ya Zanzibar kwa kutumia makumbusho na maeneo ya kihistoria. Kwa msingi huo, Kama Idara ilivyojipangia malengo yake katika mwaka 2013/2014, Kamati inaomba malengo hayo yatekelezwe kwani kwa kuimarisha maeneo ya kihistoria na kuwa na hadhi ya kitaifa na mataifa itawavutia idadi kubwa ya wananchi na wageni kutembelea maeneo hayo.

Kamisheni ya Utamaduni na Michezo

Mhe. Spika, suala la michezo hapa kwetu limekuwa kitendawili kisichokuwa na jibu. Nchi nyingi sana duniani zimekuwa zikijitangaza kupitia michezo. Isitoshe michezo imekuwa ikitoa ajira mbalimbali kwa vijana. Lakini ni kinyume kwa nchi yetu hususan katika kipindi cha miaka ya hivi karibuni. Kamati inatoa ushauri kwa Wizara kujipanga na kuweka mikakati maalum ya kuimarisha michezo iliyopo na kuifufufa michezo mingine ambapo katika miaka ya nyuma michezo hiyo iliipa sifa kubwa nchi ya Zanzibar na kutoa ajira kwa wananchi.

Hoteli ya Bwawani

Mhe. Spika, Kamati ina furaha ya dhati kwa kuona sasa hoteli ya Bwawani inafufuka kwa kufanyiwa matengenezo muhimu ya vyumba vya wageni na kumbi za mikutano. Kamati inamuomba Waziri anayehusika, kuhakikisha kuwa katika bajeti ya mwaka 2013/2014 yale yote yalokusudiwa kufanywa yafanyike ili kuweka hoteli yetu katika hali nzuri. Hii ni hoteli pekee ya Serikali iliyobakia hivyo, Serikali ihakikishe kwamba inaitunza na inaiendeleza na kuiweka katika hali nzuri ili ibakie kama ni kumbukumbu ya matunda ya Mapinduzi ya "64".

Chuo cha Maendeleo ya Utalii

Mhe. Spika, Chuo cha Maendeleo ya Utalii ni taasisi iliyopewa jukumu la kutoa taaluma itakayowezesha kujenga rasilimali watu wenye ujuzi, utaalamu na stadi zinazohitajika na kukubalika katika viwango vya Kimataifa ili kuimarisha sekta ya Utalii Zanzibar. Kamati ilipata wasaa wa kutembela Chuo cha Maendeleo ya Utalii na kupata taarifa kuwa moja wapo ya sababu ya kushindwa kuendeleza kikamilifu mashirikiano ya kikanda na kimataifa kwa kutoshiriki mikutano mbalimbali ya kimataifa ni kutokana na uhaba wa fedha. Kamati yetu inaamini kufanya jambo kwa usahihi ni matokeo ya kujifunza kutoka kwa watu au sehemu mbalimbali. Kamati inaomba, Chuo kupatiwa fedha ili kutekeleza malengo yaliyojiwekea, ikitiliwa maanani kuwa kukiwezesha chuo hichi ni kutoa upeo wa vijana wetu kujifunza na kujipatia ajira zaidi.

Mhe. Spika, kwa dhati kabisa, kamati imefarijika na utekelezaji halisi ulofanywa na Chuo kama vile uendelezaji wa jengo la ghorofa moja la madarasa na ofisi za Chuo, pamoja na kuweka samani katika jengo jipya la Chuo. Kwa kweli ni hatua ya kupongezwa na inatia moyo kuwa fedha zinazoidhinishwa zinatumika kama ilivyopangwa. Aidha, pamoja na mafanikio mbalimbali yaliyofikiwa katika Chuo hicho ikiwa ni pamoja na kuwakuza kitaaluma walimu wake, Kamati inaona kuwa changamoto iliyopo ya vigezo na sifa za kujiunga na Chuo ni dhaifu sana ambapo inapelekea Chuo kukosa hadhi. Isitoshe, wanafunzi wanaodahiliwa katika Chuo hicho ni wale ambao hawakubahatika kuendelea na masomo yao. kuna haja suala hili likatatuliwa ili sifa ya Chuo iendane na wanafunzi waliopo.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo, naomba nitumie wasaa huu tena kukushukuru wewe binafsi kwa kuniruhusu kutoa maoni ya Kamati ya Mifugo, Utalii,Uwezeshaji na Habari. Aidha, Napenda kuwashukuru pia Wajumbe wote kwa usikivu na utulivu wao wakati nasoma maoni ya Kamati yangu.

Mhe. Spika, kwa niaba ya Kamati ya Mifugo, Utalii,Uwezeshaji na Habari na kwa niaba ya wananchi wa jimbo langu la Bumbwini ninaunga mkono hoja ya Mhe. Waziri wa Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha**.**

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Spika, nakushukuru kuweza kuchangia wizara muhimu sana ambayo inakusanya mambo mengi michezo, utangazaji na utalii. Mimi niende katika ukurasa wa 6, imeonesha dhahiri hapa kuna sekta ya habari, sekta ya utamaduni, sekta ya michezo na sekta ya utalii. Hii ni moja ya faraja kubwa Mhe. Waziri ameturahisishia Waheshimiwa kuweza kuchangia kwa taaluma nzuri kwa kisayansia.

Mhe. Spika, tunaelewa sana katika wizara hii kuna mambo ambayo nilitegemea sana mara hii hasa katika bajeti ya nyuma tuliyotoka nayo nilikuwa nina imani kubwa leo Mhe. Waziri atatueleza jinsi gani asilimia ambayo ya utekelezaji katika bajeti ya nyuma tuliyoondoka nayo. Nimejaribu kuangalia sana sijaona lakini isiwe tatizo na isiwe hoja kwangu mimi kusema nizuie mafungu ya kutokuweza kutekeleza hayo. Ndio maana binadamu tukaambiwa tukumbushane katika mambo yaliyokuwa mema na tukatazame mambo yaliyokuwa mabaya. Mimi nitaanza kumkumbusha Mheshimiwa wangu Waziri kwa yale aliyoyaacha au aliyoyasahau.

Mhe. Spika, niingie katika sekta ya habari na utangazaji ambayo imo humu kwenye ukurasa huo. Kusema ukweli niwapongeze sana wafanyakazi wa Idara hiyo ambayo kwenye ukurasa wa 18. Wafanyakazi hawa wanafanya kazi vizuri sana. Tukiangalia hasa katika miongoni mwa wafanyakazi tunao humu ndani ya hili jengo lenyewe. Mimi niwapongeze sana wanastamina kubwa sana ya kuweza kuwajibika, tena niwapongeze akinamama wajasiri, wanastamina kubwa hawa. Si rahisi akinababa ovyo ovyo kwenda kusimama kama wanavyosimama wao, wanatumia masaa. Lakusikitisha posho lao ni dogo sana, kwa kweli inasikitisha.

Mhe. Spika, hebu tuangalie mandhari ya hali halisi ilivyo tangu asubuhi ndio wanaanza kukaa, wengine hao wapo tunawaona wengine wamo katika *control room*, wamelipamba sana Baraza lako hili. Siku moja kama kitu hakikurushwa wananchi wanalalamikia ni sababu zipi zilizowafanya hata leo msiturushie vipindi tukawasikiliza viongozi wetu wanavyotutetea. Lakini leo mfanyakazi huyo analipwa Sh. 5,000/- nayo anakopwa. Hili suala linasikitisha sana kusema kweli. Mhe. Waziri, posho hili la Sh. 5,000/- halifai hata kidogo, halistahiki. Leo inakwenda kumsimamisha pale mtu kwa posho hili.

Mhe. Spika, ukikaa sana ule mzunguko wa damu mwili unakuwa sio nzuri, afya inakuwa si nzuri kama wapo wataalamu wa afya wanisaidie, kwa sababu unapokuwa umesimama kwa masaa yote ule mzunguko wa damu katika mwili inakuwa inakosekana katika baadhi ya sehemu inakuwa haizunguki vizuri, kwa sababu unakuwa umekaa. Ndio maana nikakwambia Mhe. Spika, ukataka usitake mimi dokta tu.

Mhe. Spika, mimi naomba sana Mhe. Waziri awaangalie sana hawa watendaji, kwa kweli inasikitisha na ni suala ambalo linatia imani kuwapa Sh. 5,000/- halafu pesa ile inakopwa. Hili halileti faraja hata kidogo. Niseme hata hizi nguo tulisema mwaka jana wasaidiwe angalau mavazi yawe mazuri, suti nzuri wavae lakini mpaka sasa hivi sioni suti, ninavyofikiria wao wenyewe pia wametaka pesa kwa kujiweka nadhifu. Wizara bado hatujawaangalia na kama unawaangalia njoo unijibu vizuri kwamba nawaangalia, wanawapa suti nzuri, sina tatizo na wewe. Nitakubaliana na hivyo na tutakwenda vizuri sana.

Mhe. Spika, niende katika sekta ya utalii. Utalii ni uti wa mgongo wetu wa Zanzibar. Hatuko *serious* katika utekelezaji wake, tuseme ukweli. Tunapanga program nzuri lakini utekelezaji wake unakuwa hauna mafanikio mazuri. Kuna vivutio vingi Mhe. Spika, vya kuwaleta hapa wawekeza. Cha kushangaza inakuwa hatuvienzi vizuri. Tunavamiwa hata katika hizi sekta zetu tunawaacha wageni wao wanawatembeza tu na sijui wanawapotosha vipi na wanawaambiaje, hili suala kwa kweli si zuri. Kwa sababu unakwenda kuitangaza Zanzibar ndani, unaijuaje Zanzibar wewe hali ya kuwa ni mgeni pasi na mwenyewe mwananchi.

Mhe. Spika, sasa hivi kuna hata hizi gari zile wanazopakia wageni, inaonesha wale hawapewi vibali, wale watu wanaambiwa lazima wafungue *tours*. Jamani hizi *tours* zitakuwaje itakuwa kila kichochoro *tours* na kila gari itakuwa ina *tours*, kwa kweli hili suala Mhe. Waziri naomba sana hawa wanyonge maskini za Mungu wakale wapi. *Tours* hizi mtu hawezi kuunda kama hujawa tajiri.

Mhe. Waziri waokoe hawa maskini wa Zanzibar, hawana uwezo wa kuweza kufungua *tours*, sasa wapeni vibali wachukue wageni, ndiyo kazi yenyewe hiyo, vyenginevyo vyovyote tutakusanya watu ambao hawana kazi tutakaa vibarazani bure hatimaye kuingia katika dimbwi la wizi. Hili mimi sifurahiki sana na namuomba sana Mhe. Waziri aliondoe mara moja awapatie vibali wale watu ambao wanaochukua wageni kwa kutafuta rizki na watoto wao. Tusiwawekee mazingira ya kusema lazima hatuwapi kibali lazima kuwe na *tours*, tunaomba sana ili suala liondoke.

Mhe. Spika, vile vile na *traffic* wetu wazungu wanapoendesha vyombo vyao ni vizuri waangalie zile leseni zao. Inawezekana wengine hawana leseni wakatuletea balaa na wao wenyewe wakajifanyia balaa. Kwa sababu huwezi kuendesha chombo bila ya leseni, likitokezea tatizo ina maana tatizo lile linakuja katika masuala ambayo hayastahiki.

Mhe. Spika, sasa hivi lazima tugeuke, kuna hizi safari ambazo wanaokwenda nje. Kamisheni ya Utalii hebu watueleze faida yake kubwa sasa hivi tunayoipata hapa. Zanzibar katika uendaji wa maonyesho hayo, hebu naomba kidogo atwambie asilimia ngapi tunayoipata faida yake katika maonyesho yanayokwenda huko nje. Lakini je, *website* yetu iko inakwenda na wakati hebu tuangalie *website* kama inakwenda pahali vizuri basi naomba sana Mheshimiwa tusaidiane.

Niingie sekta ya michezo, sekta ya michezo Mheshimiwa, kuna hizi sheria ambazo ZFA wanatunga mnaona nyengine zinakuwa na upungufu kutokana na sheria zilizokuwa ni kali sana kwa wanyonge, naomba sana Mheshimiwa sheria hizo ziwe marekebisho ambayo tunakwenda na wakati. Lakini Mheshimiwa kuna jambo moja muhimu sana nizungumzie suala ambalo nishalizungumza mwaka jana lakini mara hii sijapata *briefing* nzuri. Mheshimiwa nilisema kule kuna hoteli ambayo *long time* imelala, hoteli ya *VENTA* hebu nitafutie Mheshimiwa leo uje kunipa jibu. Nasikia muwekezaji tayari yupo kama yupo Mheshimiwa tunashangaa kwa nini tusimpe tukaukuza ule utalii wetu, kwa sababu utaliii mambo mengi hata na mahoteli yakawa mazuri watalii wanavutiwa. Lile sasa hivi Mheshimiwa badala ya *five star*, sasa hivi limekuwa *five mwitu*, maana mna mwitu ukiambiwa leo mule akitoka simba hukatai, utashangaa sana inasikitisha sana, serikali sijui ilikuwaje ikawacha mpaka ikafika pahali sasa hivi hoteli ilikuwa *five star* hapa kwa Zanzibar leo imekuwa mwitu. Mheshimiwa kama yuko mwekezaji tunaomba haraka sana apewe airudishe mandhari yake na watu waweze kupewa wakaazi na wa utalii waanze kuja pale kuja kukaa. Mheshimiwa hili naliomba sana tena hili naliomba sitaki nikuzuilie fungu lako mimi naomba sana umlete huyo mtu.

Lakini Mheshimiwa nikenda katika masuala ya michezo kama nilivyosema hapo, nikushukuru sana Mhe. Waziri katika suala la riadha nilisema mimi lakini nimeona jitihada yako Mhe. Waziri hapa, mimi ninakupongeza sana wala sikutii ubayani kwa sababu umeichukua jitihada ya kuwakusanyisha wajumbe wa Kamati Kuu ya Riadha na kupitisha rasimu mpya na kupongeza sana lakini kilichobakia ni uchaguzi hii juu yako, nakuomba sana Mheshimiwa lifanye haraka sana suala la uchaguzi uweze kupitishwa haraka sana ili uweze kufanyika.

Lakini Mheshimiwa nilikwambia mwaka jana kuna fedha ambazo alizitoa Dr. Karume Mheshimiwa huyu Rais Mstaafu wa Zanzibar alitoa 2006 pesa zile mpaka leo wale watu hawajapewa na sijui zime-*displace* wapi, hebu naomba mara hii Mheshimiwa zifuatilie kwa umahiri wako haraka sana zile pesa wenyewe wanariadha wapewe maskini hawa na ndio maana tukasema kuwa tufanye rasimu mpya. Lakini nimshukuru sana Katibu mwenyewe Mheshimiwa wa Baraza aliyesimama mahiri na kuhakikishia rasimu inapatikana kwa wakati na hatoshindwa kusimamia uchaguzi naamini hiyo, kwa kupitia kwako wewe Mhe. Waziri hili suala liweze kukakamilika na lifike pahala.

Mheshimiwa sekta ya utamaduni, kuna nyumba kule ya sanaa kwa kweli inasikitisha sana ni mbovu mno iko Kwerekwe pale, sasa sijui tunakusudia vipi. Naomba sana Mheshimiwa nyumba ile katika kasma ambayo utakayopewa hapa na hatutokuzuilia fungu lako na hilo ulipe *priority* ya mwanzo kwenda kulitengeneza lile jumba ili ioneshe hadhi yake na haiba yake tujue kama kweli watu wa sanaa.

Lakini Mheshimiwa kuna msanii wetu huyu alituwekea nembo hii ya Baraza mpaka leo tunaitumia haidhuru kalipwa lakini kulipwa kwenyewe kweli inakwenda na wakati huyu Bwana Khamis Faki inasikitisha, kwa sababu mpaka leo katupa haiba nzuri nembo nzuri ya Baraza la Wawakilishi Mhe. Spika, lakini tumuenzi na yeye angalau *at least* kuwepo na jambo ambalo na yeye tumpe kumbukumbu kama alivyotupa kumbukumbu nembo nyingi tu aliziweka za serikali hizi KMKM sijui na wapi, lakini hii la Baraza lako tukufu Mhe. Spika, Baraza kubwa linakubalika *world*. Sasa Mheshimiwa lazima na yeye tumuenzi, tumtafutie na yeye *at least* kitu ambacho awe anakumbuka kama Baraza hili la Wawakilishi Zanzibar limepatiwa nembo inaoneshwa ile pale ni suala ambalo naomba sana na yeye tumfikirie tumpe suala ambalo la kumuenzi.

Nimalizie Mheshimiwa katika masuala ya kumbukumbu nimpongeze sana mama jasiri mkurugenzi huyu kwa umahiri wake na kufanya kazi zake vizuri katikia sekta yake, lakini nisikitike sana Mheshimiwa anapewa mafungu kidogo sana ya fedha kwa sababu suala la kumbukumbu la ukumbusho yetu haya tuliyokuwa nayo haya lazima kuwe na fedha. Mheshimiwa fedha anatiliwa kidogo sana. Mheshimiwa tukenda katika nchi za wenzetu kusema mtu kusema si vibaya, binadam usingojee ukasifiwa siku zote jisifu wewe mwenyewe unapopata nafasi.

Mhe. Spika, nilipokwenda pale Ujerumani katika kijiji cha Munich, kijiji kile wenzetu wana yale majumba yao wameyafanya kuwa nyumba za kulala na mambo haya vinywaji, maana wale wageni wale wanavutika katika masuala

yale ambayo unayoyapenda. Mheshimiwa sisi hatuna hiyo lakini ingelikuwa anafuta *special day* akaweka sheria za mila za Kizanzibari katika zile *street* za majumba yetu ambayo ya kale, angefanya jambo la msingi sana lakini atafanyaje wakati pesa hana. Mhe. Waziri naomba sana umtafutie mafungu hayo ili ayatangaze vizuri makumbusho yetu tutakuwa tunayasema bure katika vitabu vyetu na hii inatakiwa kuwa *theory* na *practicle* yenyewe ifanyike tumuwezeshe. Mimi naomba sana Mhe. Spika, waziri amtafutie *any fund* ya mpango wowote lakini lipatikane fungu la kumpa yule mwanamama pale Mkurugenzi wetu ili aweze kuendesha kazi zake vizuri ieleweke makumbusho ya Zanzibar yakoje. Lakini utakuta Mheshimiwa makumbusho ya Zanzibar yanaishia kwenye vitabu tu, hayaishii maonesho ya kuonesha kuna kitu pale *activity* ya kwenda wale watu wakenda wakafanya pale shughuli zao wakacheza msewe wakaonesha na shughuli nyengine akinamama pale kazi zao za mkono za Kizanzibari jinsi gani mavazi ya Kizanzibari yanavyovaliwa na nini watu wakashajihishwa, lakini hiyo Mheshimiwa hakuna kitu hicho.

Mhe. Spika, kama nilivyokwambia mimi kuwa sina mchango mkubwa sana katika wizara hii lakini la kumalizia ili kufungia namuomba sana Mhe. Waziri Hoteli ya Bwawani nimpongeze sana na mimi kama mwenyekiti wangu Regan, hapa alivyoeleza kuwa anaipongeza sana kwa sasa hivi limepatikana fungu la kuitengeneza. Naomba sana na wale waliokuwa na wizara zao mle ofisi zao kama hawalipi watoe usiwaweke mle. Sasa hivi hasa kwa nini hoteli inakwenda kufanywa wizara kitu ambacho Mhe. Spika, inasikitisha sana waondoeni hao, bora waweke watu wenye *tours* mle, ingekuwa ni suala ambalo ni zuri kwa sababu linaendana na utalii lakini leo unakwenda kumueka mtu waziri, unakwenda mtu sehemu nyengine haiendani. Hoteli na kuna wizara nyengine Mhe. Spika, hilo suala haliendani sana, ninaomba sana hilo hawa watu waliokuwa hawana *activities* za utalii watoe kabisa. Tunataka mle ndani umewaweka watu wenye sura za utalii ili kuwapata wazungu kuwashawishi kuwaleta na kila kitu. Hilo nakuomba sana nimalizie nishukuru sana Mhe. Spika, na mimi kama nilivyosema leo sitokuwa na mchango mkubwa kwa sababu wizara hii naamini na hasa nina historia naye Mheshimiwa wangu Waziri alivyokuwa zamani akichangia alikuwa mzuri sana akikemea sana, alikuwa mkali sana. Mimi Mheshimiwa ninakuingia mkono asilimia mia kwa mia ninangojea kwenye mabuti sikuachii kama hujanijibu vizuri.

Mhe. Spika, ahsante sana naunga mkono.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, awali ya yote hatuna budi kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kutuwezesha kufika siku ya leo tukiwa hai na hatimae kutujaalia hazina ya uzima na afya njema na

uwezo wa kuondoka katika majumba yetu hadi hapa, hii ni hazina kubwa aliyotujaalia Mwenyezi Mungu na kwa vyovyote vile hatuna budi kumshukuru.

Mhe. Spika, mara baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu nadhani nitakuwa mchache wa shukurani kama sikutumia fursa hii kukushukuru wewe kunipa nafasi hii ya kuwa mtu wa pili baada ya kumaliza Profesa Mshimba pale. Kwa kweli Profesa Mshimba kanifilisi lakini katika hili na mimi nitatia tia nyalio.

Mhe. Spika, nianze na Shirika hili la Utangazaji (*ZBC)*. Mhe. Spika, shirika hili limepatikana baada ya kuunganisha Sauti ya Tanzania Zanzibar pamoja na Televisheni Zanzibar tukapata Shirika la Utangazaji la *Zanzibar Broadcasting Corporation*. Kwa kweli Mhe. Spika, huu ni mdomo wa serikali, kauli yake inatoka kupitia pale. Kwa mnasaba huo Mhe. Spika, watu unaowaajiri katika shirika hili sio tu kama wanatakiwa wawe makini, lakini wanatakiwa wawe mahiri sana katika kufanya kazi yao hii kwa sababu mdomo, hata binadamu mdomo wake kama hakuutumia vyema huweza kumtia katika mashaka na majanga makubwa. Kwa hivyo utakapoweka watu katika mdomo wa serikali lazima tuweke watu makini, mahiri na adilifu katika kufanya kazi hii kinyume na hivyo tunaweza kuitia nchi katika matatizo kama ilivyoingia Rwanda na Burundi kupitia *Radio Interahamwe*. Hawa waliitumia vibaya tu redio vibaya tu Mhe. Spika. Warundi waliitumia vibaya redio yao na matokeo yao wakapata tatizo kupitia *radio Interahamwe.* Mwenyezi Mungu asitufikishe huko Mhe. Spika.

Mheshimiwa ninachoomba serikali lazima wawe makini katika kukisimamia hiki chombo. Hichi chombo kinafanya kazi zake kupitia kodi ya wananchi, sote hapa tunalipa kodi ndio wao wanapata mishahara. Tukishalipa kodi sisi ndio Waziri na wafanyakazi wake wanapata mishahara, kama hatukulipa kodi hawapati mishahara hawa. Kwa hivyo wanatakiwa *ZBC* wasiwe *bias,* watoe haki sawa kwa wote bila ya kujali mtu kama ni jinsia ya mwanamke au mwanamme, wapi anatoka au rangi lazima mtoe haki sawa kwa wote.

Mhe. Spika, katika hili sasa inasikitisha sana kwamba hichi chombo ambacho sote tunakilipia kodi kinafanya kazi katika misingi ya *biasness*, sijui niseme upendeleo au hakitoi haki sawa kwa kila mtu.

Mhe. Spika, mimi ni mwalimu *in profession.* Sasa ikiwa Mhe. Jaku pale atanitaja mimi ikiwa hakuniita Maalim Saleh nitaona kama kanidhalilisha, *this is my personal prestige,* hii ndio sifa yangu kwamba Maalim Saleh. Sasa inasikitisha sana Mheshimiwa vijana wetu hawa wa *ZBC* kupitia Mkurugenzi wao na hawa vijana hawajui kwamba kuna kitu kinaitwa *personal prestige.* Sasa waziri katika hili hapa hatutokubaliana mimi na wewe mpaka uje

unieleze kwa kina. Kuna viongozi wetu watatu sawa sawa hawa, kuna mheshimiwa wetu Rais tunayependa sana,Dr. Ali Mohammed Shein, Rais wetu wa Zanzibar na kama ikiwa hukumwita Mheshimiwa na Doctor inakuwa hukumpa ile *really personal prestige.* Kwa hivyo utakuwa unamdhalilisha kabisa. Halikadhalika Mhe. Spika, tunae Makamu wetu wa Pili tunampenda sana kwa sababu ni muadilifu na makini sana katika kufanya kazi zake sio za jimboni kwake lakini mpaka hapa Barazani huyu si mwengine isipokuwa ni Mhe. Balozi Seif Ali Iddi. Halikadhalika Mhe. Spika, tunae Makamu mwengine ambaye yeye haingii katika Baraza hili lakini ni Makamu wa Kwanza wa Rais huyu naye anaitwa Mhe. Maalim Seif Shariff Hamad.

Leo cha kusikitisha Mhe. Spika, hawa jamaa hawa *ZBC* wakiongozwa na Waziri wao Mhe. Said Ali Mbarouk wanawavunjia heshima baadhi ya viongozi wetu wakubwa inasikitisha sana. Mimi nishawahi kumwambia Waziri huyu lakini mkaidi kwamba iweje watoto wadogo wale wanapomtaja Makamu wa Kwanza wa Rais katika shughuli inayofunguliwa na Makamu wa Kwanza wa Rais Seif Shariff Hamad, mara kadhaa nimemwambia wanamdhalilisha Makamu wa Kwanza wa Rais. Sasa leo hapa tutabanana hapa hapa leo. Iweje hawa wengine wawataje Mhe. Dr. Ali Mohammed Shein, huyu mwengine atajwe Mhe. Balozi Seif Ali Iddi, huyu mwengine atajwe Seif Shariff Hamad iweje?

Huu ni udhalilishaji, Mhe. Waziri na wafanyakazi wako wapo juu hizo pesa zinatokana na sisi sote, *let me declare my interest* kwa sababu mimi nina *interest* kwa sababu mimi Katibu wa Chama wa Wilaya bwana ni mtu mkubwa katika nchi hii ni Katibu wa CUF Wilaya ya Chake Chake, hamuwezi kumdhalilisha mtu hivi ikawa mimi kiongozi wa chama na siasa nipo haiwezekani kabisa kabisa. Hichi chombo kama mnataka kutumikia watu basi anzisheni vyombo vyenu nendeni *Zenj FM.* Nataka nimshauri rafiki yangu kinana aanzishe redio yake ili mkatumikie redio ya Chama cha Mapinduzi, lakini hii ni redio ya wananchi, tunawalipa sisi mifukoni pesa zetu ndio mnazolipwa mishahara na maposho. Katika hili mimi bwana hapa siambiliki Mhe. Waziri mpaka unambie watu wako wanafanya hivi kwa sababu hawajui kama huyu ni Makamu wa Rais, hawajui wanafanya hivi watu wako hawa kwa sababu ya uadui tu au wanafanya hivi kwa sababu ya ujinga.

Kama hawajui basi waelimishe lakini kama wanafanya kwa uadui ni tatizo, lazima upambane nao hawa kinyume na hivyo bajeti yako hatukupitishii hapa. Mhe. Spika, inasikitisha sana mimi si lazima kama hutaki kumwita Mheshimiwa basi mwite japo Maalim Seif Shariff Hamad usimkate jina hukumzaa wewe yule. Tena ninamwambia Mkurugenzi wao Mitawi pamoja na hawa watoto hawa lazima wawe na heshima, *Radio Interahamwe* iliwapigisha watu pale mpaka sasa wameingia katika *genocide* na *ZBC*

msitake kuifanya kuwa kama *Radio Interahamwe*, hii nasema kwa uchungu kabisa Mhe. Spika.

Mhe. Spika, katika hili basi ninamshauri Mhe. Waziri anapotaka kuajiri watu katika vyombo vikubwa kama hivi basi asiokote kwenye maskani za vyama vya siasa, tafuta watu walio-*qualify* katika mambo ya *information technology*, mambo ya *mass communication*, mambo ya *Public Relation*, sawa anaweza akakufanyia vizuri lakini watu hawa wanaozungumzia mambo haya mengine hebu wapelekeni katika *Zenj FM*, anzisheni redio ya Chama cha Mapinduzi muwapeleke, redio ya serikali watu ambao ni *intellectual* katika mambo haya *information technology*.

Mhe. Spika, sasa niende katika suala zima la Idara ya Habari na Maelezo. Katika hili hii ni Idara muhimu sana kwa sababu ni Idara inayoweza kuwapa watu taaluma ya habari, ndio inayoweza kuwahabarisha watu mambo na haki ya kupata habari .Mhe. Spika, ni ya kila Mzanzibari wa nchi hii ana haki ya kupata habari kupitia chombo chake hususan hiki chombo cha serikali ikiwemo hii *ZBC*. Sasa inasikitisha sana kwamba tatizo liliopo sheria za vyombo vya habari katika nchi, zinawafanya baadhi ya Wazanzibari wasipate taarifa kutokana na mapungufu yao ya kimaumbile.

Kwa mfano walemavu pamoja na kwamba wanalipa kodi katika kulipa haya magazeti haya, hili gazeti letu la Zanzibar Leo lakini walemavu wa macho wasioona hawawezi kulisoma, hii ni kuwanyanyasa na kuwaonea kwa sababu na wao wanalipia kodi. Mimi naomba sheria ya vyombo vya habari zirekebishwe ili na hawa wenzetu wenye mapungufu ya macho waweze kufaidi hii *national cake* kwa kujisomea kwa yale maandishi ya kupapasa; maandishi nundu. Kwa hivyo sheria zitajwe wazi hasa kwamba gazeti lolote katika nchi hii halitasajiliwa ikiwa halijatoa angalau nakala chache za maandishi nundu kusudi kuwapa nafasi na hawa wenzetu walemavu waweze kujisomea taarifa za nchi yao. Kwa hivyo Mhe. Waziri katika hili nakuomba sana Mheshimiwa ili waweze hawa wenzetu kufanya hiyo habari.

Mhe. Spika, tatizo jengine ni kwamba gazeti hili ilikuwaje likachapishwa Dar es Salaam. Jamani mimi ndio nasema kama hii serikali yetu hii ingekuwa binadamu angekuwa mlemavu kabisa kabisa kwa sababu tulikuwa tukilichapisha hapa hapa sisi na magazeti mengi tuliuwa tukichapisha hapa hapa enzi zetu sisi. Gazeti la 'Kweli Ikidhihiri Uongo Hujitenga', tulikuwa nalo gazeti hilo tukilichapisha hapa hapa. Nyinyi kwa nini mshindwe, ni kwamba ulemavu huo. Sasa kama ni hivyo basi ninawaombeni sana ikiwa mnakuwa mna matatizo Mhe. Spika, turuhusu sisi, mimi mara nyingi husema hivi lakini inaonekama kama ninatania. Hebu turuhusuni miezi miwili tu tuje tukae hiyo benchi ya mbele tukiwa chini ya uongozi wa Mhe. Salmin Awadh

na Mhe. Abdalla Juma muone kama gazeti la Zanzibar halitochapishwa hapa hapa Zanzibar, uwezo tunao kabisa kabisa, uwezo tunao bwana linachapishwa hapa hapa. Leo gharama zimekuwa nyingi mimi nataka Waziri anieleze ni gharama kiasi gani zilizokwaza nchi hii mpaka gazeti letu likachapishwa kwa ndugu zetu wa damu, sababu gani za msingi, hizo si kasoro za Muungano nazo pia ati Mhe. Waziri.

Sasa niende katika sekta ya utamaduni. Mhe. Spika, katika sekta ya utamaduni kwanza nataka nikwambie kwamba msanii ni kioo ambacho mtu anaweza kukiangalia akajirekebisha. Kwa hivyo siku zote kazi za sanaa zinatakiwa ziende sambamba na utamaduni, inasikitisha sana kwamba Waziri wetu wa Habari na Wizara yake wanashindwa kuziendesha, hizi kazi za sanaa kuziendesha sambamba na utamaduni wetu.

Mhe. Spika, mimi sijui siku hizi tujifunze nini, yaani kama ni kioo hebu tuangalieni ile wanaita rusha roho siku hizi mimi nilikwenda na mama yangu siku moja katika harusi ya mjukuu wake katika *hall* fulani hapa Unguja kwenda kuangalia lakini kukapigwa rusha roho. Mhe. Spika, nilisikitika sana taarabu hiyo inayoitwa rusha roho, kuna mama kainama anacheza rusha roho utafikiri kafunga feni huku nyuma na kuna jamaa kamkamata hivi, nilimwambia mama twende zetu hapakaliki hapa, ile si mila na silka ya Kizanzibari kabisa kabisa. Mhe. Spika, kipindi cha nyuma utamaduni ulikuwa makini sana katika nchi hii na wasanii akinamama Siti binti Saad. Mama Siti binti Saad alikuwa akenda katika maonesho Mhe. Spika, alikuwa anasikilikana sauti tu anajifunika buibui na tulikuwa tukiburudika vizuri sana na mama Siti binti Saad, mpaka wakasema sura yake mbaya ndio anajifunika buibui. Kuna jamaa zangu wa Kiwani walimuimba kwamba Siti binti Saad umekuwa mtu lini, umetoka kwenu shamba na kaniki mbili chini kama si sauti ungekula nini? Walimuimba hivyo kwa sababu haonekani ati sura yake mbaya. Kama kuna mwanamke mzuri katika nchi hii hasa huku Kusini mwa jangwa la Sahara alikuwa bibi Siti binti Saad tatizo nilikwenda kule *archive* picha zao haziko tu ningewaletea mkamuona alivyokuwa anang'ara yule mama kabisa kabisa, lakini kwamba si hoja uzuri na sura jamili kuwa mtu mkuu na Juba kubeli, uzuri wa mtu kukosa akili aliwajibu jamaa. Sasa mambo kama haya Mheshimiwa hawa watu wewe unakwenda kuangalia rusha roho la kutikisa feni huku nyuma ni tatizo, kwa hivyo lazima sanaa zetu ziende na utamaduni wetu.

Niende katika mambo haya ya makumbusho. Mhe. Spika, makumbusho ni muhimu sana katika kuangalia utamaduni wa nchi na historia ya nchi hii. Historia ya nchi hii lazima mufanye utafiti wa kina katika kuidhibiti historia hii na kuweza kujenga makumbusho mengine inanisikitisha sana Mhe. Waziri Ofisi yako haiko serious katika kuangalia vyanzo vyengine vya makumbusho

ya kale. Kwa mfano katika kijiji changu kule Makaani Vitongoji kuna gofu la kasri ya mfalme aliyekuwa Ngezi hamjalishughulikia lolote, halafu kile kijiji changu cha Umangani, mimi nataka kiwe ni cha historia kwa sababu katika kijiji cha Umangani Vitongoji pale Waarabu kutoka Oman katika maeneo ya Nisua, Rustak, Sib na Muslimat walikuwa wakitoka kwao wanafikia pale Vitongoji na wanaoa.

Aidha Wangazija kutoka Anzuani, Mayote walikuwa wakifikia Vitongoji pale na wakawa wameoa wamezaa na watoto wao wengine wamo humu humu ndani. Sasa inanisikitisha kwamba kijiji changu hakijawekwa katika kijiji cha historia mkajua mkafanya utafiti hawa Waarabu na Wahindi mpaka walioa kule na hawa Wangazija walikimbilia Vitongoji pale kwa sababu ya uzuri wa wale wanawake waliopo pale au kwa sababu ya hulka nzuri tu ya wakaazi wake au kwa nini, ukieka kwenye makumbusho mambo kama haya Mhe. Waziri mimi kidogo ukitaka kujua kuhusu wale unaweza ukapata kwa Mhe. Mohammed Aboud pale pamoja na mwanangu Omar Yussuf Mzee wanaweza wakaeleza chochote katika hili waoneni hao. Vipi Vitongoji kwa nini Waarabu wakakimbilia pale.

Namalizia Mhe. Spika, katika hili kwamba Hoteli ya Bwawani imepoteza muelekeo kwa sababu tuliianzisha kibiashara sisi leo, natapata habari kwamba Hoteli ile Ofisi za serikali zinahamia hatukuianzisha kwa kuweka Ofisi za Serikali sisi ile.

Jengine Mhe. Spika, mikataba ya wafanyakazi ni matatizo wafanyakazi mikataba yao si mizuri.

Jengine Mhe. Spika, mapato je nauliza kuhusu mapato anambie waziri yale mapato wanayoyatumia pale Bwawani mara baada ya kuwapata bila ya kuyapelekea serikalini imekubalika au wanajifanyia tu pale Bwawani.

Naunga mkono hoja.

Mhe. Spika: Ingekuwa ninajua kwamba Mhe. Saleh ana maneno kwenye sehemu ya utamaduni bajeti hii ingekuwa si katika mwezi wa Ramadhani, maana yale maneno mengine yale yamesahau kama kumbe tuko kwenye mwezi wa Ramadhani mtukufu. Ninamuombea radhi kwa Mungu.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, naomba nianze kwa kumshukuru Muumba wetu Mwenyezi Mungu Subhanahu Wataala kwa kutuamsha tukiwa hai na wazima na tukaweza kuendelea na mfumo wa mwezi mtukufu wa Ramadhan hapa Barazani tukiendelea kufanya kazi ya wananchi wa Zanzibar waliotupigia kura kutuleta hapa ili kusimamia maslahi yao. Mhe. Spika,

nikushukuru na wewe kwa kunipa nafasi na mimi kuchangia bajeti hii ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo na nisiwe mpungufu wa shukurani Mhe. Spika, naomba pia nimpongeze Mhe. Waziri wa Wizara hii Mhe. Said Ali Mbarouk kwa kuwasilisha hotuba hii na pia kamati kwa kutupa maoni yake.

Mhe. Spika, mimi kabla sijaendelea naomba niseme kwamba sitaiunga mkono bajeti hii.. Naomba niseme kabisa kwamba nitatumia kanuni ya 98.6 kuzuia shilingi mia katika bajeti hii ikiwa sitapata maelezo ya kuridhisha hasa katika maeneo mawili ambayo nitayazungumza baadae kwa kina kidogo, moja ni kuhusiana na utendaji uliofeli wa Shirika la Utangazaji Zanzibar (*ZBC).* La pili ni kuhusiana na hifadhi ya Turafi.

Mhe. Spika, naomba nianze na suala Idara inayohusika na Makumbusho na Mambo ya Kale. Mhe. Spika, ili nisipoteze muda nataka nilikumbushe Baraza lako tukufu kwamba zikiangaliwa *Hansard* mwaka juzi, mwaka jana katika vikao kama hivi vya bajeti, lakini hata mwaka huu tulipokuwa tukijadili ripoti za kamati tulizungumza sana juu ya jinsi gani tusivyoenzi historia yetu.

Mhe. Spika, Zanzibar ni Zanzibar na inathaminika na kuheshimika na kutambulika, na historia yake na kama ilivyokuwa historia ya taifa lolote duniani inaweza kuwa na matukio mazuri ya kujivunia, inaweza kuwa na matukio mabaya ambayo tunapaswa kujifunza nayo lakini vielelezo vya historia vyote huwa vinabakia kutunzwa ili kuonesha wapi tulipotoka tujue wapi tulipo na tunapokwenda.

Mhe. Spika, inasikitisha sana kwamba tunapenda kuimba sana kuhusu historia na kuimba sana kuhusu majengo ya kisheria lakini hatuyatunzi. Tahadhari niliyoitoa mwaka juzi, nikaitoa mwaka jana ikatimia mwishoni mwa mwaka jana, jumba ambalo ndio kielelezo cha Zanzibar lipo katika Mji Mkongwe Beit el Jaib, jumba ambalo kama inapigwa picha maarufu katika eneo lile la ukanda wa bahari katika eneo lile la Shangani, Forodhani mpaka kufika kwenye bandari, basi kama hulioni lile unaona Zanzibar haijatimia. Lakini jumba lile lililokuwa na historia yote ile Mhe. Spika, liliachwa pamoja nakulitaja mimi mara mbili katika miaka miwili tofauti ya bajeti mpaka likafika kututia aibu likaanguka sehemu ya nyuma huku upande wa mkono wa kushoto likaporomoka. Sasa Mhe. Spika, na humu nimeendelea kuona tena tunaendelea kusema kwamba tutavitunza, lakini sioni kwamba kuna umakini katika hili. Sitaki kupoteza muda mwingi lakini nimwambie Mhe. Waziri kwamba katika hili nataka aje anieleze kwa kina kwa nini tuendelee kumpitishia bajeti ya Idara hii na ya kusimamia shughuli hizi ikiwa ukiyapitia

majengo haya leo sitaki kuyapitia kwa vile nimeshazungumza hapa ukiyapitia yapo katika hali mbaya sana.

Mhe. Spika, kulikuwa na miradi hapa haipo katika Wizara yake lakini ilikuwa katika Wizara iliyopita alikuwa akiiongoza yeye nikawahi kusema hapa kwamba jumba lile la Beit el Jaib na Jumba la Kasri yalitajwa yatakuwemo katika mradi mpaka leo Mhe. Spika, tukaangalie hali ilivyo lile jumba la Kasri ambalo linatumika kama ni Ofisi ya Baraza la Mapinduzi na pengine kama sivyo vibali vinavyoombwa hapa vya kwenda kuvifanyia matengenezo kupitia bajeti ya Ofisi ya Rais basi lingekuwa hali yake taaban, lakini lilikuwa na fedha za kutengenezwa zinakwenda wapi fedha hizi zote na hali kiuhakika hairidhishi. Sasa mimi nasema kwa sababu ya muda naliacha hapo hapo.

Mhe. Spika, mimi nilizungumza ndani ya jimbo langu najiuliza hili, Mhe. Waziri yeye mwenyewe ni dhaifu au watendaji wake wanamuangusha au ndio utendaji wa Serikali yetu tu kama tulivyokwishazoea maeneo mengi hakuna utendaji. Mhe. Spika, nimelalamika mara nyingi kwake na katika Baraza hili kuhusu kutumika maeneo ya wazi kupigia *disco* au muziki wa nguvu. Mara moja Mhe. Waziri akafanya ziara na akanipigia simu kwamba nimpelekee Diwani wa eneo lango lile, akenda akatoa maagizo lakini maagizo yale hayafuatwi mpaka leo ukumbi wa Ngome Kongwe unatumika kupiga muziki wa wazi, ni eneo lililokuwa wazi, kuna maeneo ya wakazi ya watu pale. Wakati fulani ilikuwa dhahma kubwa Malindi kule kwa sababu ya *disco* la wazi katika hoteli ya Bwawani hakuna ukumbi wa *disco,* Bwawani sehemu ya *disco* ambayo iko chini imejengwa kitaalamu lakini mtu hariziki mpaka akapige kule juu kwenye ukumbi wa wazi abughudhi watu na akere watu wanaolala maeneo yale wote pale, lakini haya yako ukenda sijui kwa Raju, Gofu kila pahala sio kwamba nazungumzia jimbo langu tu kwa jumla nauliza ile kauli yake imefikia wapi.

La tatu Mhe. Spika, nisikitike kwamba kasema Mhe. Waziri nchi yetu bahati mbaya sana inajenga utamaduni mbovu ambayo si sehemu ya historia yake ya kutokuthamini watu na michango yao katika ujenzi wa nchi hii. Nilizungumza hapa kuhusu suala la aliyekuwa msanii maarufu aliyepata jina kubwa Zanzibar Marehemu Bi. Fatma binti Baraka kwa umarufu ni Bi. Kidude. Lakini ili kushughulika kwa kuonesha siku ya mazishi yake kulikuwa hakuendi sambamba na jinsi tulivyomhudumia wakati anaumwa na familia yake ilikuwa aibu, kwa sababu wakati ule walikuwa wanasema wazi wazi walivyokuwa wanahojiwa na vyombo vya habari, sasa katangulia mbele ya haki, lakini wako wengine yule angalau tulikwenda tukashiriki katika mazishi yake, kuna wengine hata ile kutambua mpaka leo kimya.

Mhe. Spika, nina mifano mingi lakini ndio hivyo muda unatukwaza lakini ninataka kutoa mfano mmoja ambao umetokea ndani ya mwaka huu wa fedha katika jimbo langu sote tunamfahamu na kama mtu hamfahamu akamfuatilie, maana yake atakuwa mtu wa ajabu kama hafuatilii historia kiasi hicho. Bwana mmoja anaitwa John De Silva, ni Mzanzibari mwenye asili ya Goa ambaye alikuwa mchoraji maarufu ameitangaza Zanzibar sana kupitia picha zake za uchoraji lakini pia kuandika hadithi na maelezo kuhusu Mji Mkongwe, picha zake Mhe. Spika, zimetumika mpaka kutengenezea *stamp* za kuitangaza Tanzania katika utalii, ametajwa katika vitabu mbali mbali vya makala nyingi zilizoandikwa duniani lakini hapa kwetu tu, kafariki huyu sikuona chochote kutoka kwenye upande wa serikali hata ile kumtambua.

Mhe. Spika, ilifanywa misa maalum ya kumkumbuka na familia yake nimepata bahati ya kushiriki. Lakini nilisikitika sikuona kiongozi yeyote wa serikali aliyekuja pale. Mhe. Spika, huu si utamaduni mzuri wa kuenzi nawataja hao wameshakwenda mbele ya haki, lakini wako wengi ambao mpaka sasa hivi wahai na tutaendelea hivi hivi hatukumbuki waliotangulia, hatuwaenzi walioko na baadae inaonekana ni jamii ya aina gani ambayo haiheshimu watu ambao wametoa mchango mkubwa katika hili. Mhe. Waziri akija aniembie wana mpango gani angalau wa kuwakumbuka watu kama hawa na mchango mkubwa ambao wametoa katika nchi.

Mhe. Spika, sasa nije suala ambalo nimeliweka mwisho lakini ni zito, ni suala ambalo ndio linabeba roho ya Wizara hii ni la utendaji mbovu wa Shirika la Utangazaji Zanzibar (*ZBC*). Mhe. Spika, wakati tulipokuwa tukijadili mswada wa *ZBC* tulisema sana tena sote humu ndani jinsi tusivyoridhika. Tulitegemea ile michango yetu ingekuwa ni changamoto ya kwenda kuona marekebisho katika chombo kile, lakini hali si tu haitengenei Mhe. Spika, inazidi kuwa mbaya kila kukicha. Mimi kwa kifupi Mhe. Spika, nasema uongozi na hasa Kiongozi Mkuu wa Shirika hili kashindwa kazi, Mkurugenzi Mkuu wa Shirika hili kashindwa kazi na sote tunajua kwamba mtu huyu amekuwepo katika nafasi ile kwa miaka mingi sana kama ni mtu wa kuleta mabadiliko tungeshayaona muda mrefu sana, tangu ilikuwa Idara ya *TVZ* peke yake, kashindwa *TVZ* leo tumemchanganyia na Sauti ya Tanzania Zanzibar tumemuwekea pamoja tukamwambia Shirika la Utangazaji ongoza wewe, kashindwa kule kumoja ataweza kuyaongoza yote Mhe. Spika.

Mhe. Spika, naomba nitaje maeneo machache tu. Moja ni katika *performance* yake Shirika hili. Nataka kutoa mfano wa *Television* lakini hata redio. Zanzibar ni katika nchi za mwanzo katika redio ni nchi ya mwanzo katika ukanda wote wa Afrika Mashariki ya Kati kuanzisha redio wakati huo ikiitwa Sauti ya Unguja, lakini sisi pia chini ya uongozi wa Marehemu Mzee Karume tumekuwa ndio nchi ya mwanzo kufikia Jangwa la Sahara Afrika kuanzisha

TV ya kwanza ya rangi na ilikuwa ikitajika kila pahala tukiuonewa gere tukionewa wivu na wenzetu waliokuwa hawana huduma kama hiyo, leo nani anatizama *ZBC*, *Television* imeanzishwa karibuni tu zimeifunika kabisa *ZBC* hata kama hazipaswi kutoa matangazo kama ilivyo *Zanzibar Cable Television*, lakini chombo kile ni cha kutoa matangazo ya *cable*, lakini leo watu wanaona bora wakaangalie vile kuliko kuangalia *ZBC* kwa sababu hakuna kilichokuwa ambacho hakionekani.

Mhe. Spika, mimi najiuliza hali hii itaendelea mpaka lini, tuangalie aina ya vipindi vya matangazo havina mvuto wowote, *television* gani ambayo haina hata mpangilio wa vipindi vyake vinavyoeleweka kwa kila siku, kwa kila wiki muda gani unapata kipindi gani, kila mtu anaweza akaingia saa yoyote akafanya kipindi chochote kikawekwa wakati wowote, tumeona wapi Mhe. Spika, mambo haya. Lakini hata wafanyakazi wetu katika vyombo hivi tunawaendeleza kiasi gani kitaalamu, lakini baya zaidi ni udhalilishaji wa wafanyakazi. Leo Mkurugenzi Mkuu huyu anafika kuwaambia wafanyakazi kwamba wanawake wavue hijabu wanapofanya kazi katika *ZBC* katika matangazo, ati ndio utamaduni na kimataifa, wapi Mhe. Spika.

Mhe. Spika, tunaangalia *television* ya Kenya ambao utamaduni wake pengine hata si kama wetu sisi lakini watangazaji walioamua kuvaa hijabu zao wanavaa muhimu wanaambiwa zivaliwe hijabu zinazokwenda na viwango na wawe *presentable* wawe wanapendeza wakionekana kwenye TV. Lakini leo katika nchi kama hii yenye asilimia 99 Waislamu unapotoka Mkurugenzi Mkuu ukawaambia wafanyakazi wanawake wavue hijabu unakusudia nini wewe, una dhamira gani katika nchi hii.

Lakini udhalilishaji wa wafanyakazi Mhe. Spika, hauishii hapo tu. Mhe. Spika, kuna mfanyakazi wa kike mmoja anaitwa Maryam, aliyekuwa sehemu ya *editing* ya vipindi akenda akajiendeleza mwenyewe kaondolewa kaambiwa anapelekwa sehemu ile aliyoisomea hasa mwanzo katika maeneo ya utawala, sina muda ningetoa maelezo marefu hapa lakini cha kusikitisha badala yake kachukuliwa msaidizi wake aliyekuwa ambaye hana uwezo wowote anawekwa ndio anaongoza pale, yaani shirika lile wewe ukija ukimkosoa Mkurugenzi Mkuu hata kwa jambo dogo ndio umejimaliza, hili si mali yake binafsi Mhe. Spika.

Mhe. Spika, leo kuna vitu mpaka Rais wetu Mhe. Dkt. Ali Mohammed Shein, kavipongeza hivyo vichache angalau vilivyobakia na jina, huyu anaviondoa ana dhamira gani huyu. Mhe. Spika, Mhe. Rais alikisifu kipindi kilichokuwa kinaitwa Fahari ya Zanzibar, kakisifu Mhe. Rais lakini Mkurugenzi Mkuu kakiondolea mbali ana dharau hata kwa Rais wa nchi. Mhe. Rais kamsifu mtangazaji Juma Mmanga na ni katika wafanyakazi wachache ambao

wamejenga uwezo mzuri, sasa kamuondoa katika sehemu ile kuna mvutano mkubwa baina ya Wizara na yeye juu ya wapi awekwe Juma Mmanga.

Mhe. Spika, mwaka jana mimi na Mhe. Bi. Panya tulimtaja hapa katika michango yetu tukasema aengwe-engwe asije akaondoka kama tulivyompoteza Marini Hassan. Leo Marini tumemkosa ni *star* kwa sababu ya mtu huyu huyu na Juma Mmanga tunaelekea kumpoteza na ana dhamira gani kutuulia vyombo vyetu vya habari huyu.

Mhe. Spika, jengine anafanya vipindi nakuendesha chombo cha Serikali cha walipa kodi ambacho kinapaswa kuakisi sera ya nchi ambayo imesimama katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar yenye msingi wa Umoja wa Kitaifa, leo yeye anaandaa kila aina ya uchochezi na fitna ili kuvuruga Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Lakini nimalizie dakika zangu 5 ulizonipa hizo tatu zilizobakia katika maeneo mawili.

Mhe. Spika, la kwanza naomba maelezo katika ukurasa wa 31 kumetajwa kwenye hotuba ya Waziri kumetajwa kuundwa kwa Kampuni ya *ZMF Company*. Sasa katika maeneo yake nimestaajabu kidogo naona kwamba inaambiwa hisa zake zinamilikiwa na Ofisi ya Rais, Fedha na Uchumi na Mipango na Maendeleo asilimia 60, *ZBC* asilimia 20 na Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo asilimia 20. Hebu nije nisaidiwe mimi kwa upungufu wangu wa maarifa hizi zote ni taasisi za serikali na anayeshikilia hisa za serikali, ninavyoelewa mimi anapaswa kuwa ni Hazina katika hii kugawanywa kwa wizara utaratibu mpya hii? na kama sivyo naomba nije nielekezwe Mhe. Spika.

Mhe. Spika, la mwisho tumetangaza kuingia katika *digital* katika hiyo hiyo *ZBC*, tumetangaza kuingia katika mfumo wa *digital* kutoka katika mfumo wa *analogue*. Baada ya kishindo kikubwa kapewa Kampuni inayoitwa *AGAPE*. Kuna maneno mengi mitaani tunamuuliza mara nyingi Mhe. Waziri, hebu atusaidie kwamba mbona kampuni iliyoambiwa ina uwezo mpaka leo ina mambo ya msingi haijakamilisha, walipaswa watuingize katika *digital* ikifika mwezi wa Disemba wameshindwa, tukaambiwa itafanyika mwezi wa Februari mpaka leo haijamalizika, *quality* au ubora wa viwango, wametakiwa hawa watu kwamba wanaleta ma-*generator* katika vituo hawajaleta mpaka leo, wametakiwa wajenge minara hakuna mpaka leo, kuna mahitaji yao mengi katika mikataba walitakiwa waelekezwe na mimi naelewa kwamba walipofanya uchunguzi wa kampuni zilizoomba zabuni aliyetoa mapendekezo ambayo walimtafuta wao mshauri aliwaambia wamchukue *AGAPE*, lakini akatoa sharti kwamba wafuate zile taratibu na yale makubaliano yaliyowekwa katika mapendekezo yao ya mradi kwamba atafuata yote, yote hayazingatiwi.

Mhe. Spika, mimi nasema hadi tuelezwe, tunavyosikia huko mitaani maana kuna mengi katika Zanzibar hii kwamba pale hapaendi kwa sababu kuna mvutano baina Katibu Mkuu wa Wizara na timu yake wana maamuzi yao na *ZBC* kwa uwezo wake wana maamuzi yao, na matokeo yake mivutano yao hawa wanatukwamishia huduma kwa wananchi wa Zanzibar. Maskini za Mungu ambao hawana njia ya kwenda kujiunga, sasa nilikuwa naomba maelezo katika hayo na kama nilivyosema Mhe. Spika, ikiwa sikupata maelezo ya kuridhisha kwamba kwa nini tuendelee kumbakisha Mkurugenzi, kwa nini Waziri anamng'ang'ania Mkurugenzi Mkuu huyu ambaye kafeli katika nchi hii siku zote ambaye anatukwamisha na hili la *AGAPE* kama sikupata maelezo ya kuridhisha mimi nazuia shilingi mia katika bajeti hii.

Mhe. Spika, siungi mkono hoja mpaka nipate maelezo.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, na mimi nashukuru kupata nafasi hii ya kuchangia hotuba hii ya bajeti ya Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kwa mwaka wa fedha 2013/14.

Mhe. Spika, awali ya yote kwanza nianze kwa kutoa shukurani nipongeze kwa Mhe. Waziri namna alivyokisoma kitabu chake kidogo kwa *speed* kali bila ya kufika popote na kwa kukimaliza mapema kwa sababu ya wakati. Jengine niwapongeze wote wale watatu waliotangulia na nashukuru wamefanya kazi kubwa sana ya kuchangia hotuba hii, kwa hivyo kazi yangu mimi itakuwa nachangia kidogo kidogo tu kwa kutaka kupata maelezo ili nitekeleze ule wajibu wangu na kutokana na hilo Mhe. Spika, naanza moja kwa moja na Chuo cha Maendeleo ya Utalii.

Mhe. Spika, Chuo hiki cha Maendeleo ya Utalii ni chuo ambacho kina umuhimu wa aina yake kwetu kutokana na kuwa kinatoa taaluma inayohusiana na mambo ya utalii na ikiwa ni njia moja kuu ya kuingiza uchumi katika nchi hii. Kwa mujibu wa maelezo yaliyoko katika kitabu Mhe. Spika, ni kuwa Chuo hiki cha Utalii kina jukumu la msingi la kutoa taaluma itayowezesha kujenga raslimali watu wenye ujuzi, utaalamu na stadi zinazohitajika na kukubalika katika viwango vya kimataifa ili kuimarisha sekta ya utalii Zanzibar.

Mhe. Spika, kwanza Chuo hiki kwanza kiko Maruhubi, katika kitabu sikuona namna gani Mhe. Waziri, akajitahidi katika kukihami chuo hiki na mmomonyoko mkubwa wa ardhi unaotokea katika sehemu ya baharini. Hiki chuo kimo katika hatari na Mhe. Waziri hakueleza chochote kuhusu kukihami. Kwa hivyo ningelimuomba Mhe. Waziri anieleze ni juhudi gani atachukua kuona chuo hiki kinachoimarishwa kinalindwa kutokana na *erosion* inayotokea.

Kwa mujibu wa maelezo yaliyomo katika kitabu hiki ni kuwa malengo ya mwaka 2013/14 kwa chuo hiki ni kufanya mazungumzo na vijana wa Kizanzibari kuwashajihisha kujiunga na chuo kwa kuwaonesha shughuli mbali mbali zinazofanywa na chuo katika skuli tisa za Wilaya tisa za Unguja na Pemba. Hapa naomba mimi nipate maelezo hichi chuo ni muhimu kwetu na ni chuo kama vyuo vyengine ilikuwaje moja katika malengo makubwa iwe ni kuwashawishi vijana kujiunga na hichi chuo, hivyo ni kwa sababu vijana hawapendi kujiunga au kulikuwa kuna sababu gani ya kufanya hivyo, halafu zimechukuliwa skuli tisa kwa wilaya tisa, naomba Mhe. Waziri anipe vigezo alivyotumia katika uteuzi wa skuli hizo na wilaya hizo kwa nini Wilaya moja haikuchukuliwa.

Mhe. Spika, halafu jengine ni kuwa zamani nilivyokuwa nikijua chuo hichi ilikuwa kinachukua vijana wale wanaofeli katika kuendelea na masomo kuanzia *Form II* na kadhalika. Je, hivi sasa bado inaendelea na uchukuaji wa vijana hao hao na kwa nini wakati wako vijana waliosoma na kuelimika wengine mpaka *Form Six* hawachukuliwi kujiunga na hichi chuo na wakapata hayo mafunzo kutokana na umuhimu wa chuo chenyewe kilivyo.

Mhe. Spika, malengo mengine yatakayofanywa katika mwaka huu wa fedha 2013/14 ni kuwajengea uwezo walimu kwa kuinua viwango vyao vya elimu yaani taaluma. Lakini nikitaka nijue je, kimaslahi kuwajengea uwezo kielimu ndivyo lakini maslahi, kweli hichi chuo kutokana na umuhimu wake ni lazima kipate walimu waliokuwa wana uwezo. Hivyo kweli hawa walimu wenye uwezo wanalipwa ukilinganisha pamoja sehemu nyengine ili watu wetu wasije wakatukimbia wakenda katika nchi nyengine. Kwa mfano tulinganishe watu wa chuo kama hichi wanaolipwa Bara na wanavyolipwa hapa vipi inalingana. Halafu nikitoka hapa naomba niende kwenye Shirika la Utalii.

Mhe. Spika, Shirika hili la Utalii ukiangalia ukurasa wa 39 imeelezwa kama ifuatavyo, ni kuwa Shirika la Utalii ni moja ya mashirika yaliyo chini ya Wizara hii ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo na kuwa shirika hili kwa kipindi kirefu hali ya biashara imekuwa sio nzuri kutokana na ushindani mkubwa uliopo katika sekta ya biashara ya utalii hapa nchini. Hapa ninapotaka kueleza ni kuwa hili shirika ni la serikali hivi sasa linafanya kazi shughuli za utalii, linaingiza mapato na kadhalika, ilikuwaje ikawa shirika hili likashindwa katika ushindani wa watalii ni kuwa wafanyakazi hawalipwi vizuri, mapato yanavuja na kadhalika mpaka ikawa hivi sasa shirika hili linakumbwa na kadhia kubwa sana.

Mhe. Spika, vile vile ninataka kujua Hoteli ya Bwawani. Hoteli ya Bwawani ni hoteli yetu tunayoringia, hoteli iliyojengwa na muasisi wetu wa mapinduzi Marehemu Mzee Abeid Amani Karume na mpaka sasa hivi ninasema ni ya

aina yake katika Zanzibar hii. Hoteli hii kwa bahati mbaya mpaka sasa kwa mujibu wa kitabu ni mbovu. Kwa mfano katika kipindi cha mwaka 2012/13 kumetengenezwa vyumba vinne na kufanya marekebisho madogo madogo ya vyumba pamoja na uwekaji wa waya wa mbu madirishaji ili kwenda sambamba na soko la ushindani wa sasa, mwaka mzima kazi ilikuwa hiyo na katika malengo ya mwaka 2013/14 ni kuwa kutafanywa ukarabati wa vyumba hamsini vya hoteli na kati ya hivyo kumi vinahitaji ukarabati mkubwa na arubaini ukarabati mdogo, kumbi nne za mikutano, viyoyozi kumi katika vyumba vya hoteli, ina maana hii hoteli iko katika hali mbaya sana.

Mhe. Spika, kwa sababu kipindi hiki kinachomaliza Wizara ilikuwa na uwezo wa kutengeneza vyumba kumi tu, hivi sasa imejipangaje wakati naona kuwa uliposoma kitabu cha bajeti fedha yake haijawa kubwa kiasi hicho ili katika mwaka huu wa fedha 2013/14 waweze kutengeneza vyumba hivi hamsini, watapata fedha kutoka wapi au wamejipanga vipi katika kufanya hivyo. Halafu vile vile tukitizama katika malengo haya ya mwaka 2013/14 ni kuwa kazi ya Wizara itakuwa ni kuitangaza hoteli ya Bwawani kwa njia ya vipindi vya matangazo kupitia redio, *television* pamoja na vipeperushi. Sasa hii hoteli inataka kutangazwa na ni mbovu namna hiyo basi sijui kwa nini kwanza haikutengenezwa mpaka ikamalizika halafu tena hayo matangazo ndio yatatangazwa ili watu waweze kuja na kuona kweli kutokana na jengo lilivyo ina haki ya kutangazwa hivyo na watu waweze kuitumia.

Mhe. Spika, halafu jengine hoteli hii ninavyojua mimi imekumbwa nayo na mmomonyoko wa ardhi na nashukuru Wizara hii kwa kushirikiana na Wizara ya Miundombinu kwa kupitia Shirika lake la Bandari, wamejenga kule uzio au ukuta wa kuzuia maji ya bahari yasiharibu na kuingia kwenye hoteli. Lakini wakati nilipokuwa katika Kamati ya Mifugo, Utalii na Habari tulitoa ushauri pamoja na wenzangu kuwa ile kazi iliyofanywa ni kubwa, fedha nyingi zimetumika lakini bado haiwezi ikazuia maji yasiweze kuchimbua na hasara ikaja kama kawaida, tulishauri kuwekwe mawe kama ilivyo gati ya Mkoani na halafu vile vile tupande miti, mikoko na kadhalika ili kupunguza nguvu za maji. Sasa sijui mpaka leo kwa nini wakati ushauri ule tumeutoa zamani haujafanywa kutokana na kuwa ukuta uliokuwepo hauwezi ukazuia mmomonyoko ule.

Mhe. Spika, mimi ninavyojua ni kuwa zamani palijengwa bwawa la kuogelea pale baada ya kuvunja Msikiti uliokuwa ukiitwa Msikiti Mabuluu, na bwawa lile bahati mbaya halikuweza kufanya kazi iliyokusudiwa na mpaka leo lipo kama historia, na Msikiti Mabuluu umejengwa tena na wakati pana Msikiti pale haielekei hasa pawe na bwawa la kuogelea. Je, baada ya kurejeshewa ule Msikiti ambao uling'olewa makusudi kwa sababu ya bwawa lile, lile bwawa lina mpango gani kuendelea vile vile au kuondolewa moja kwa moja.

Halafu na la mwisho kuhusu hoteli ya Bwawani, tulipokuwa tukenda kule kwenye ziara tulipata taarifa kuwa ile hoteli inataka kuuzwa moja kwa moja, ijengwe mpya ile ivunjwe kwa sababu haiingii katika hali halisi ya kileo ilivyo. Lakini huku naona kunataka kutumiwa pesa nyingi sana kuifanyia marekebisho, kuitangaza, kuvutia wageni, kuita ushauri elekezi katika kuweka kumbukumbu za wageni wapya wanaoingia na kadhalika na wakati tulisikia kuwa inataka kuuzwa. Je, hilo suala la kuuzwa limekufa naomba kupata jibu.

Nikitoka hapo Mhe. Spika, kama nilivyosema leo mambo yangu ni madogo madogo tu naomba kuzungumzia kuhusu Baraza la Michezo. Mhe. Spika, Baraza la Michezo ni chombo kikubwa sana na humu imeoneshwa nia hasa ya kukuza michezo katika nchi hii na michezo ni moja katika mambo ambayo yanamsaidia binadamu hata kupata ajira, michezo inaitangaza nchi na michezo ni muhimu kwa wote. Lakini kwa bahati mbaya Wizara imeweka maazimio haya makubwa ya kueneza michezo kwa wote na hata kushirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali lakini sikuona hasa mipango ambayo itaifanya hii michezo ukue.

Kwa mfano, Mhe. Spika, hapo zamani skuli zote kulikuwa na michezo na kulikuwa na walimu wa michezo na walimu walikuwa wakipatiwa mafunzo ya michezo, wakija Unguja hapa kutoka nchi mbali mbali kuwafundisha walimu na walimu wale wakawa wanawafundisha watoto na kila siku ya Jumamosi baada ya mapumziko, baada ya kipindi cha nne, cha tano na cha sita ilikuwa ni kipindi cha michezo na kulikuwa na mashindano ya michezo. Kwa hivyo, michezo ilikuwa inakua halafu tena ikawa na Zanzibar inajitangaza kimichezo lakini leo tunafanya michezo kwa sherehe tu kuonesha kuwa na sisi tumo. Hivyo kweli wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu imeweka mpango gani hasa wa kuwafanya hawa walimu waweze kuiendesha hii michezo kwa mujibu itakiwavyo ili hiyo azma ya kukuza michezo kwa wote iendelee.

Mhe. Spika, naona nirudie kidogo walikozungumza Waheshimiwa kuhusu *ZBC*. Kama inavyozungumzwa kwamba *ZBC* ni chombo kilichoundwa na taasisi mbili, Televisheni Zanzibar na Sauti ya Tanzania Zanzibar. Kwanza Mhe. Spika, mimi nataka nielezwe, hii Zanzibar ni nchi ilikuwaje hii Sauti ya Zanzibar ikaitwa Sauti ya Tanzania wakati ni ya Zanzibar? Kwa nini hii *ZBC* isiwe ni chombo kilichoundwa na Sauti ya Zanzibar na Televisheni ya Zanzibar iwe imeundwa na Televisheni ya Zanzibar halafu na Sauti ya Tanzania Zanzibar kwa nini isiwe Sauti ya Zanzibar. Naomba Mhe. Waziri anipe jibu ya hilo.

Halafu jengine Mhe. Spika, pamezungumzwa mengi hapa na *ZBC* ni chombo chetu sote na kinatakiwa kifanye kazi kwa maslahi ya wananchi wote na

wengine wanaokisikiliza waliomo ndani ya nchi na nje ya nchi. Lakini wenzangu wamezungumza walivyozungumza, sitaki nirejee, naomba tu kwa kuongeza kusema kuwa hiki chombo kwa sababu hakitakiwi kufanya kazi kisiasa na tushakibaini kinafanya kazi kisiasa na hakiko wazi.

Juzi Mhe. Spika, ukitizama magazeti, mitandao unaona viongozi wa Chama cha Wananchi *CUF* kule Bara waliopigwa na Jeshi la Wananchi wa Tanzania wanaonekana wazi na wanatoa maelezo yao, pamoja na jeshi kuwa walijitetea lakini inaonekana wazi, leo chombo hiki cha hapa hapa Unguja panafanywa mambo chungu nzima sisi tunasema tu, hii ni nchi yenye utulivu sijui ya amani, watu wanapigwa, watu wanaonewa, watu wanavunjwa hapa haijatoa hata siku moja kwa nini? Kwa sababu inayofanya ni serikali. Kwa hivyo, mimi naomba kama kuna chombo cha habari katika nchi hii kifanye kazi zile ambazo zitaonesha wananchi hali halisi ilivyo Zanzibar ili ambapo hata serikali inayoongozwa na binadamu inapokosea paweze kurekebishwa. Lakini ikiwa kuna mambo wenyewe wataona haya tuyape kipaumbele, haya tusiyape itakuwa kama wanakifanya ni chombo cha siasa, sivyo. Ikiwa mtu anaona ni lazima aende hivyo basi huyo hatufai waziri amuondoe moja kwa moja, amuondoe ashirikiane na hao wanaostahili lakini aondoke atatuharibia kwa sababu hiki ni chombo chetu sote.

Halafu jengine ni kweli sisi tulipiga kelele walikuwa watu wanakuja na fulana za msewe halafu wanatangaza tunawaona hivi, ni aibu, tukapiga kelele sasa hivi wanavaa vizuri, leo itakuwaje mtu awalazimishe Wazanzibari waliokuwa wana dini yao, silka na itikadi yao waje pale uchi watangaze kwa kuwa ni wanawake wameajiriwa sivyo. Sasa ikiwa mwenyewe anaona ile ndio hali ya watu kuishi lakini Wazanzibari sio walivyo pale ni bora apishe wengine. Kwa hivyo, mimi binafsi kwa hiki kifungu cha mwisho kama Mhe. Waziri hakutoa taarifa hasa kwa vile anasema atafanya marekebisho ni marekebisho gani atakayoyafanya kwa maslahi ya Wazanzibari wote. Mimi nitakuwa ni mmoja niliyekuwa bajeti hii sitaiunga mkono. Mhe. Spika, nashukuru sana ahsante.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Nakushukuru Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii nikaweza kuchangia hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo Mhe. Said Ali Mbarouk juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya wizara yake.

Mhe. Spika, wizara hii ni wizara muhimu na kwa sababu ni wizara inayosimamia vyombo vya habari na kama tunavyojua kwamba habari ni kitu muhimu, kuhabarisha watu ni jambo zuri ili wananchi waweze kuelewa mambo yanayofanyika ndani ya nchi na hata nje ya nchi. Watu bila ya kupata taarifa au kupata habari watakuwa wapo wapo tu hawajui kitu kinachoendelea.

Mhe. Spika, mimi ni Mnadhimu wa Chama cha Mapinduzi katika Baraza la Wawakilishi na nipo kwa mujibu wa kanuni na taratibu zetu ambazo tumejiwekea. Lakini pale ambapo nahisi chama changu hakitendewi haki, nina wajibu wa kusema kwa sababu mimi ndiye msemaji wa Chama cha Mapinduzi katika chombo hiki. Mimi nasikitishwa sana Mhe. Spika, kwa baadhi ya Wajumbe kunasibisha mambo yanayofanyika katika *ZBC* na Chama cha Mapinduzi.

Hili Mhe. Spika, Mhe. Saleh Nassor Juma amezowea sana, nilikuwa nikimsikia sana akisema na nimekuwa nikistahamili, lakini naona bila ya kulisema hili labda mambo haya yanaweza kuendelea jambo ambalo haliwezi kuleta taswira nzuri katika jamii. Mimi ninavyofahamu Mhe. Spika, kwamba *ZBC* ni chombo cha serikali na kina wafanyakazi wenye itikadi tofauti, si vyema hata kidogo kukitupia lawama chama fulani au Chama cha Mapinduzi kwa ajili ya mambo au matendo yanayofanywa na wafanyakazi ili ionekane kwamba labda wametumwa na Chama cha Mapinduzi sio haki. Kama kuna mambo ambayo yanafanyika kinyume na taratibu ni vyema yakazungumzwa yale mambo ambayo yanafanyika kuliko kukitupia lawama chama ambapo chama hiki kwa pamoja kimeunda Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Tumeanzisha Serikali hii ya Umoja wa Kitaifa kwa kuondosha mambo haya ambayo pengine yanaweza kuleta tofauti na leo tumeshuhudia kwamba Serikali hii ya Umoja wa Kitaifa inakwenda vizuri na imekusanya mawaziri kutokana na vyama vyetu viwili vikubwa.

Leo bahati nzuri Mhe. Said Ali Mbarouk ni Mwakilishi wa kutoka *CUF* ndiye waziri wa chombo hiki, ndiye anayeongoza chombo hiki. Sasa utakapofika pahala ukawa unakitupia lawama Chama cha Mapindiuzi unakitaja moja kwa moja kwamba ndio kinahusika na mambo haya, kwa kweli sio jambo zuri na niwaombe Waheshimiwa tabia hii tuachane nayo. Tuzungumze kile kitu ambacho kiko mbele yetu, tuzungumze hoja iliyo mbele yetu, vyenginevyo dhamira nzuri ambayo tulikuwa tumeianzisha tutaanza kukoroga humu, badala ya kusimamia serikali tukawa sasa tunavisimamia vyama vyetu jambo ambalo sio dhamira ya serikali yetu na Serikali ya Umoja wa Kitaifa. *(Makofi)*

Mhe. Spika, mimi namuamini sana Mhe. Waziri ni waziri aliyekuwa anasimamia vyema shughuli zake Mhe. Said Ali Mbarouk, anafanya kazi kwa uadilifu mkubwa na kama kuna kasoro naamini ataweza kuzichukulia hatua kasoro zile ambazo zimejitokeza.

Mhe. Waziri tumekuwa tukipata taarifa zake kutokana na watendaji wake na kwa kweli huwa tunapata taarifa kutoka kwa wafanyakazi wengi katika sekta mbali mbali, lakini katika watendaji wanaomsifu waziri wao ni waziri wa wizara hii. Kwa hivyo, ni mtu makini anayeweza kusimamia chombo hiki

kwa uadilifu mkubwa, kama kuna kasoro ambazo zinajitokeza ni kasoro za kawaida za kibinadamu zinaweza zikajitokeza katika eneo lolote katika suala la utendaji.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri katika kitabu chake ametuelezea vipaumbele katika sekta mbali mbali, kazitaja sekta ya habari, sekta ya utamaduni, sekta ya utalii na sekta nyengine. Pia ameeleza katika sekta ya habari kwamba kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora za habari na kwa wakati kwa njia ya magazeti pamoja na redio na televisheni kupitia teknolojia ya kisasa ya utangazaji wa *digital*.

Mhe. Spika, hiki ni kipaumbele kizuri na mara nyingi nimekuwa nikilalamikia juu ya vipaumbele na dhana ya vipaumbele. Wenzetu hawa wa *ZBC* wamekuwa na changamoto nyingi na hizo lazima tuzikubali, hatuwezi tu tukawatupia lawama tukaweza kuwatupia lawama viongozi wa *ZBC*, wafanyakazi wa *ZBC* lakini huku tunashindwa kuwawezesha kufanya shughuli zao za kazi na sote tunaelewa. *ZBC* ina changamoto nyingi ukiwemo ufinyu wa bajeti, hivi kweli unaweza kutekeleza shughuli hizi bila ya kuwa na fedha? Kwa hivyo, kushindwa kwa *ZBC* kufanya ushindani na vituo vyengine vipya ambavyo vimeanzishwa ni kutokana na ufinyu wa bajeti na wala sio utendaji. Mkurugenzi Mkuu wa shirika hili ni mtu mahiri sana, mwenye uzoefu katika shuguli zake za utendaji lakini atawezaje kufanya shughuli zake bila ya kumuwezesha.

Mhe. Spika, nilikuwa naangalia bajeti ambayo Mhe. Waziri huku nyuma ametuwekea bajeti katika mchanganuo mbali mbali kwenye kiambatanisho 'A' ambapo ameelezea juu ya fedha zilizoingizwa kuanzia Julai 2012, mpaka Juni, 2013 katika Shirika la Utangazaji, kwenye matumizi mengineyo ambapo haya ni matumizi ambayo fedha zake zinawezesha kufanya kazi, wamepata asilimia 51. Hivi hebu tujiulize asilimia 51 ya bajeti ndogo ya ufinyu wa bajeti ambayo wamepewa unawezaje kufanya mambo ambayo yanaweza yakaonekana, yanaweza kuleta ushindani katika vyombo hivi vya habari katika wakati huu wa utandawazi, haiwezekani hata kidogo. Kwa hivyo, kwanza ni lazima serikali iliwezeshe shirika hili na zaidi ukizingatia kwamba shirika hili lilianzishwa bila ya kujitayarisha sote tunajua hapa. Tulianzisha Shirika la Utangazaji bila hata ya kujitayarisha, lilianzishwa bila hata ya sheria mwaka mzima linakwenda bila ya sheria na kupewa majukumu mbali mbali, lakini leo *Alhamdulillah* tunashukuru tumeanzisha tumepitisha sheria chombo kile kipo na kwa mujibu wa taratibu sasa lililobakia ni kuliwezesha shirika hili kulipatia nyezo ili liweze kufanya kazi vizuri na kwenda katika ushindani wa kileo.

ZBC halina vifaa vya kufanyia kazi, *ZBC* linaripotiwa kwamba lina *camera* moja ya nje na *camera* tatu za ndani za kurikodia, hivi kweli unaweza kufanya kazi katika hali hiyo. Bado lina vifaa vya kizamani ambavyo haviendani na wakati wa leo. Kwa hivyo lazima tuwe wakweli, ni lazima Waheshimiwa Wajumbe tuwe wakweli. Mimi nadhani wale watakaohimiza kwamba shirika hili lipewe fedha za kutosha, lipewe mtaji wa kutosha, mimi hao nawaunga mkono na pale tutakapowawezesha tukawapa fedha za kutosha sasa hapo patahitaji kuwa na lawama na kumlaumu kila mmoja kuanzia Waziri, Mkurugenzi, Katibu Mkuu na kila mtu, lakini leo huwezi kumlumu mtu wakati humuwezeshi kufanya kazi.

Kwa hivyo, lazima tufahamu kwamba chombo hiki kinahitaji kuwezeshwa na Mhe. Waziri ni lazima *ZBC* ukae nao ujue mahitaji yao na ujue namna ya kuwasaidia kutatua matatizo yao waliyokuwanayo. Hili jambo la muhimu wana matatizo mengi Mhe. Spika, nadhani Mhe. Waziri anayajua matatizo yao wana matatizo mengi, hawana vifaa hata *scheme of service* ya wafanyakazi hakuna, hakuna motisha kwa wafanyakazi wa chombo kile. Kuna wafanyakazi wanafanya kazi mpaka usiku wanakesha, tunajisifu kwamba *ZBC* inafanya kazi masaa 24 lakini wale watendaji ndani ya chombo kile wanashindwa kuwezeshwa kutokana na ufinyu wa bajeti, mtu anakaa mpaka asubuhi hapati chochote, lakini haya yote yanatokana na ufinyu. Kwa hivyo, Mhe. Spika, mimi nadhani tuwatendee haki wenzetu, tuwape moyo wana kazi kubwa na tuitake serikali ikiwezeshe chombo hiki kiweze kufanya kazi zake vizuri kwa manufaa ya wananchi wote.

Jengine Mhe. Spika, katika eneo hili hili kuna wafanyakazi ambao wanakitumikia chombo hiki tunawaita mafundi mitambo. Hivi kweli fundi wa mitambo anafanya kazi miaka 35, 30 leo mshahara wake bado mkia wa mbuzi analipwa shilingi laki moja na nusu miaka 35 anafanya kazi tena ni *technician*, kweli tuko *serious* halafu leo kweli sisi tutake ufanisi katika chombo hiki. Mhe. Waziri hili naomba aje atueleze, kwa nini mafundi wako wa mitambo hawawezeshwi kupewa mishahara inayolingana na fani yao? Ndio maana Mhe. Spika, nilisema hapa juzi kwa bahati hukuwepo kwamba Wizara hii ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ikae mwisho sasa kama inavyokaa Wizara ya Fedha. Kwa sababu kuna mambo yanayohusu utumishi waje watusaidie hapa, haiwezekani wafanyakazi washafanya kazi miaka mingi ni mafundi, wamepewa dhamana, wamepewa vyeo halafu leo mishahara yao mkia wa mbuzi mtu anapata shilingi laki moja ishirini au laki moja thamanini ni kweli hiyo.

Kwa hivyo, lazima tuwawezeshe mafundi wetu waweze kufanya kazi zao vizuri, wako mafundi wengine wako humu humu wakiumwa kidogo hali ya mitambo inakuwa katika hali ya matatizo. Mhe. Waziri atakapokuja kufanya

majumuisho atueleze juu ya wafanyakazi hawa sita ambao wako katika sehemu za mitambo ambao kwa kweli hatuwapi zile stahili zinazohitajika pamoja na uwezo wao, juhudi zao na mambo mengine.

La mwisho Mhe. Spika, katika eneo la utalii. Utalii ni sekta kiongozi na nadhani dhana hii sasa hivi imeshaanza kupotea miongoni mwetu. Lakini huko nyuma tunakotoka sote tulikuwa tunajua kwamba utalii ni sekta kiongozi na utalii bila ya kutangazwa huwezi kuwa na utalii, lazima utalii utangazwe. Hebu tujiulize tunachukua *effort* gani ya kuona kwamba utalii wetu unatangazwa na watalii wanakuja. Bajeti tunayotenga kwa Kamisheni ya Utalii kwa ajili ya kuutangaza utalii je, inakidhi haja? pamoja na keki ndogo tuliyokuwanayo lakini lazima tuwe na vipaumbele katika maeneo kama haya lazima utalii utangazwe ili watalii wapate kuja, bila ya kuutangaza utalii tutakuwa tunaimba tu, tunakuwa tunaimba kila siku watalii ni lazima kuwe na bajeti ya kutosha bajeti iliyotengwa kwa ajili ya ku-*promote* utalii haitoshi kabisa ambayo imetengwa katika Kamisheni ya Utalii. Kwa hivyo, bajeti lazima iwe ya kutosha ili ile dhana ya kwamba utalii ni sekta kiongozi basi iweze kutimia.

Mhe. Spika, Chuo cha Utalii. Chuo hiki kwa mujibu wa ripoti ya Mhe Waziri kimejenga jengo la ghorofa moja ametueleza kwamba limekamilika, lakini kuna baadhi ya maeneo bado hayajakamilika. Lakini inaonekana hakuna fedha safari hii zilizotengwa kwa ajili ya maendeleo ya Chuo cha Utalii sikuiona. Sasa Mhe. Waziri aje atueleze kwamba je, pale walipokuwa wamefikia katika ujenzi ule wa chuo ndio umetosha, kwa nini hakukutengwa fedha kwa ajili ya kuliendeleza lile jengo na mambao mengine, sikuona. Kwa hivyo, aje atwambie Mhe. Waziri kwamba tumetenga fedha eneo fulani kwa ajili ya kuliendeleza lile jengo au lile jengo limekamilika mia juu ya mia tupate kujua. Lakini kuna haja ya kutenga fedha ili jengo lile liweze kukamilika na liweze kutumika. Sisi tunawapongeza sana, tunawapongeza sana Mhe. Waziri, Mkurugenzi wa Chuo cha Utalii amefanya kazi vizuri lakini lazima tuwawezeshe ili waweze kukamilisha ile mipango.

La mwisho Mhe. Spika, kwenye hotuba yake Mhe. Waziri ametueleza juu ya watalii kutangaza utalii, lakini hajatupa takwimu za watalii wanaoingia nchini na nchi zao, amekuwa anafanya kazi yaku-*promote* utalii, kuwaita watalii lakini kwenye kitabu chake hajatueleza kwamba katika kipindi hiki cha mwaka huu kuna watalii kadhaa wameingia nchini wakionesha na nchi zao ili Baraza lako tukufu lione kazi nzuri inayofanywa ikilinganishwa na miaka ya nyuma. Mwaka uliopita watalii walikuja hawa, mwaka huu wako hawa na tunategemea mwakani watalii watakuja kiasi hiki. Mimi sikuona humu kwenye kitabu na wakati unapofanya kazi lazima yale matokeo yaweze

kuonekana, matokeo mazuri yaonekane tuone kama kweli tuna-*improve* au bado tuko pale pale.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Spika, mimi naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja na niwaombe Waheshimiwa wenzangu wote waunge mkono hoja hii ili tumuwezeshe Mhe. Waziri akaweze kufanya haya mambo mazuri kwa ajili ya manufaa ya nchi yetu. Vile vile tuiombe serikali iongeze bajeti katika wizara hii hasa katika maeneo haya muhimu kwa ajili ya maendeleo ya nchi. Ahsante Mhe. Spika, tunakushukuru.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Spika, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutukutanisha hapa leo tukiwa wazima wa afya kujadili bajeti ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa mwaka 2013/2014.

Mhe. Spika, pili nikushukuru wewe kwa nafasi hii ili kuniwezesha na mimi kusema machache katika bajeti ya Wizara ya Habari na Utalii. Mhe. Spika, nampongeza Mhe. Waziri kwa uwasilishaji wake wa hotuba kwa ufanisi na kwa *speed* kubwa ambayo alitumia kusoma bajeti hii.

Mhe. Spika, kwa kuanzia mimi nitaanza katika ukurasa wa 18 kwenye Shirika la Utangazaji. Mhe. Spika, sitogusia ubovu wa shirika na mambo yote yale yanayohusiana na hayo, lakini kuna mambo mawili matatu ambayo nimehisi niyagusie ambayo wenzangu hawakuyagusia. Kwanza Mhe. Spika, naomba nigusie jambo ambalo nimeliona na ambalo halimo katika bajeti ni la ujumla linalohusiana na Shirika la Utangazaji.

Mhe. Spika, wakati Mhe. Saleh Nassor Juma anachangia hapa alikuwa mkali sana akazungumza kwa hamasa zote kwamba watu wa Shirika la Utangazaji wanavyokata jina la Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais badala ya kumpa heshima yote inayotakiwa. Alisema kwamba wanamkata jina na kusema tu, Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais, Seif Sharif Hamad.

Pia nakumbuka Mhe. Raya Suleiman wakati anachangia bajeti ya Wizara ya Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais na yeye alikuwa mkali na akachukizwa sana kwa kusema kwamba anachukia watu wenye ulemavu kuitwa viguru. Sasa na mimi Mhe. Spika, nachukia sana jengo letu la *Karume House* ambapo Shirika la Utangazaji liko pale, lile jengo limepewa jina tangu asili *Karume House*, lakini hivi sasa Mhe. Spika, ukipita pale usiku jengo lile linasomeka *Kru House* badala ya *Karume House*.

Nakumbuka nilipokuwa nawasilisha bajeti ya mwenyekiti wangu Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria Mhe. Ussi Jecha Simai alisema kwamba, kuna

mambo mengine hayawezi yakakaa mpaka kusubiri bajeti ndio yatengenezwe. Sasa Mhe. Spika, kwa kuwa ile *signal* ya jengo lile limekosa taa katika herufi a, m na e badala ya kusomeka *Karume House* sasa linasomeka *Kru House* kwa taa tatu tu ambazo zimekosekana katika neno lile. Sasa nimuombe Mhe. Waziri tukishapitisha hii bajeti akazungumze na watu wake wakatafute taa warudishie katika herufi zile ili lile jengo lisomeke kama kawaida *Karume House*. Kama haiwezekani basi wasiwashe taa usiku waliache vile vile ili mchana taa ya Mwenyezi Mungu ikiwaka jengo lile lisomeke *Karume House*.

Mhe. Spika, nikitoka hapo nilikuwa nataka nimuulize kitu Mhe. Waziri anipe ufafanuzi kidogo katika malengo ya mwaka waliyojipangia 2012/2013 ni kukamilisha ujenzi wa Kituo cha Matangazo ya Masafa ya Kati *MW* ambayo yalikuwa hayapatikani kwa muda mrefu. Lakini katika utekelezaji halisi ameeleza kwamba ujenzi wa mnara wa kurushia matangazo Bungi utekelezaji wake umekamilika. Sasa huku wameeleza kuhusu ujenzi wa kituo lakini wametwambia kuhusu ujenzi wa mnara, nataka nimuulize Mhe. Waziri ujenzi wa kituo umekamilika ama bado.

Jengine Mhe. Spika, ambalo nilikuwa nataka niligusie katika Shirika la Utangazaji ni deni ambalo Ofisi ya Hakimiliki inadai *ZBC*. Mhe. Spika, Shirika la Utangazaji linatumia kazi mbali mbali za wasanii, haipendezi kuona kwamba ofisi ya hakimiliki inapata shida sana kudai zile haki za wasanii kwa kutumiwa kazi zao kuwa moja ni Shirika la Utangazaji. Na tunaona hapa shirika linajinasibu kati ya majukumu ya msingi ni kuelimisha, kuburudisha wakati kumbe kazi zile wanazotumia kuburudisha wao wenyewe wagumu kuzilipia.

Halafu Mhe. Spika, la kusikitisha hao hao Shirika la Utangazaji wamewaandikia Ofisi ya Hakimiliki kwamba waanze kulipia *airtime* ile ambayo Ofisi ya Hakimiliki wanatumia kuelimisha wananchi, lakini wao wenyewe wanajisahau kwamba wao wanadaiwa shilingi 25 milioni na ofisi hiyo hawajalipa kutokana na kazi za wasanii ambazo wanazitumia. Sasa Mhe. Spika, mimi sijawahi kuzuwia fungu lakini hapa nitazuwia fungu Mhe. Waziri anambie ni lini deni linalodaiwa Shirika la Utangazaji na Ofisi ya Hakimiliki litalipwa ili tuone kwamba wasanii wetu hasa hawa wadogo wadogo wa *Zenji Flavor* na hata hawa wa kasida ambazo wanazitumia hivi sasa wanapata ile haki yao kutokana na mirahaba ambayo inagaiwa na Ofisi ya Hakimiliki.

Mhe. Spika, serikali inazungumzia kuhusu uwezeshaji wasanii na ndio maana Mhe. Rais alifungua lile jengo jipya la *studio* ya wasanii. Mimi nakumbuka kuna kikao kimoja Mhe. Mwenyekiti wa Chama wa CCM Taifa Mhe. Dr. Jakaya Mrisho Kikwete alitwambia kauli zetu viongozi zi-*reflect* matendo yetu, sasa huku tunazungumzia kuhusu kuinua maisha ya wasanii wakati

huku tunashindwa kulipa kwa kutumia zile kazi zao wanazozifanya. Sasa Mhe. Spika, hii inakuwa haipendezi na namuomba Mhe. Waziri akija hapa anipatie maelezo kwamba ni lini deni ambalo Afisa Hatimiliki linaidai *ZBC* italipwa.

Mhe. Spika, jengine ambalo nililokuwa nataka kulizungumza ni kuhusu mapato ya Shirika. Mhe. Waziri ametueleza kwamba kwa mwaka 2012/2013 Shirika lilipangiwa kukusanya jumla ya shilingi milioni mia mbili na thanini na laki saba. Nakufanikiwa kupata shilingi milioni mia mbili na laki tatu tisini na tisa elfu mia mbili na thamanini na tatu sawa na asilimia 77. Lakini katika malengo aliyojipangia kukusanya mara hii ni milioni mia mbili thamanini.

Sasa Mhe. Spika, nilikuwa najiuliza wakati Shirika lipo katika *transformation* wamefanikiwa kukusanya shilingi milioni mia mbili na kumi. Lakini sasa linaanza ku-*take off* wamerudisha nyuma makusanyo. Sasa nilikuwa nataka maelezo hapa Mhe. Waziri akija anieleze kwa nini shirika limejiwekea malengo madogo wakati linaweza kukusanya malengo makubwa zaidi ya hayo waliojiwekea.

Mhe. Spika, nikimaliza na Shirika la Utangazaji naomba niingie Chuo cha Maendeleo ya Watalii *page* ya 37. Nakipongeza chuo kwa kazi inayofanya kwa kutoa taaluma kwa vijana katika *field* mbali mbali. Mhe. Spika, chuo hiki ni roho ya utalii, pia nakipongeza chuo kwa kuimairisha miundo mbinu ya chuo hicho kwa kujenga jengo la ghorofa na madarasa ili kuwawezesha wanafunzi kujifunza wakiwa katika mazingira mazuri. Lakini Mhe. Spika, naweza kusema ni bado kazi ifanyike sana kukiendeleza chuo hiki. Kama chuo kitaendelea kutoa vijana lege lege Mhe, Spika, hawana *skill* za kutosha juu ya dhana nzima za utalii hatutofika sehemu na hasa vijana wetu wakienda katika *field* za ajira hizi hawatafanikiwa.

Mhe. Spika, hivi karibuni tumesikia *work permit* imeongezwa ili kulinda vijana wazalendo ambao wanaingia katika hizi *field*. Mhe. Spika, nataka kusema kama hatuto-*improve* vijana wakatoka vijana wazuri kutoka pale Chuo cha Utalii kwa kweli hata tukiongeza hizi *work permit* bado tatizo la ajira kwa vijana litakuweko pale pale. Kwa sababu hawatokuwa na *skill* za kushindana katika suala zima la utalii.

Mhe. Spika, hapa pia nilikuwa nataka kugusia mapato ya Chuo. Chuo kilipangiwa kukusanya jumla ya shilingi milioni mia mbili sitini na mbili na kufanikiwa kupata shilingi milioni mia mbili tisini na tano sawa na asilimia 113. Lakini katika mwaka wa fedha 2013/2014 chuo kimejipangia kukusanya shilingi milioni mia mbili na thamanini. Sasa nilikuwa najiuliza tena kwa nini tujiwekee malengo madogo wakati kinaweza kukusanya zaidi ya hizi ambazo

wamejiwekea mwaka huu. Mwaka jana wamekusanya zaidi ya hizi waliojiwekea mwaka huu. Sasa kwa nini tena wajiwekee malengo madogo wakati wanaweza kukusanya makusanyo makubwa kama walivyokusanya mwaka jana wakapita asilimia na kufikia asilimia 113.

Mhe. Spika, nikimaliza na chuo sasa nataka kuingia katika sekta ya utalii katika Kamisheni ya Utalii *page* ya 34. Mhe. Spika jukumu la msingi ya Kamisheni ya Utalii ni kupanga kuratibu na kusimamia kuendeleza shughuli za utalii ndani na nje ya nchi. Naipongeza sana Kamisheni kwa kufanikisha jukumu hili kwa upande wa utalii wa nje ya nchi, yaani *international tourism*. Lakini Mhe. Spika, katika upande wa *domestic tourism* hatujaona jitihada ambazo zinachukuliwa kushajihisha wananchi wa Zanzibar kujikita katika utalii wa ndani.

Mhe. Spika, katika malengo yake aliyojipangia 2012/2013 lengo namba 3 ni kutanganza usajili wa Zanzibar kitaifa na kimataifa. Ukiangalia utekelezaji halisi jitihada nyingi zimefanywa katika upande wa *International tourism*, yaani utalii wa kimataifa. Sasa nilitaka kujua Kamisheni inajipangaje juu ya hili ili kuona kwamba utalii wa ndani wananchi wa Zanzibar nao wanashajihishika kufanya utalii ndani ya Zanzibar. Kwa mfano wenzetu wa Tanzania Bara wa *TANAPA* wanashajihisha utalii wa ndani ambapo wanaweka *fee* za kutembelea vile vivutio vya mbuga za wanyama kwa bei ambayo wananchi wazalendo wanaweza kuingia.

Lakini pia wanatumia *TV* zao za ndani mbali mbali kutangaza sehemu za utalii zinazopatikana ndani ya nchi ili kuwaonesha wananchi ni aina gani ya utalii ambao unapatikana katika nchi yao na hii yote wanafanya haya kuwavutia wananchi. Sasa nilikuwa nataka uzuri wa wizara hii vile vyombo vya habari tunavyo wenyewe, lakini hatujaona kwamba ni jinsi gani vinatumika ili kuona kwamba wanashajihisha utaliii wa ndani. Hata yale mazingira yenyewe ya utalii bado hayajawa *friendly* kwa watalii wa ndani. Tuna hoteli tofauti za kitalii Mhe. Spika, lakini bado wananchi kwa kweli hawana kipato cha kufika huko na kuweza kutalii hizo hoteli ambazo zinapatikana Zanzibar. Seuze sisi tu Waheshimiwa Wawakilishi mpaka tusubiri semina zao Mhe. Spika, ndio tufike huko. Je, wananchi wa kawaida kweli inawawia vigumu kufika huko.

Mhe. Spika, kwa ku-*save* muda wako mimi nitaishia hapo lakini siungi mkono hoja mpaka Mhe. Waziri atakapokuja kunambia kwamba ni lini deni ambalo Ofisi ya Hakimiliki inadai katika Shirika la Utangazaji litalipwa. Mhe. Spika, nakushukuru.

Mhe. Viwe Khamis Abdalla: Ahsante Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia hotuba ya Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni Utalii na Michezo.

Mhe. Spika, nikianzia na mchango wangu naanza kwenye taarifa ya habari. Mhe. Spika, kwa kweli taarifa ya habari haitoshi kwa kipindi walioupanga ule muda wake hautoshi.

Mhe. Spika, angalau wangetenda muda wa saa moja kuliko ule wa nusu saa kutokana na bahari zilizokuweko nchini. Mhe. Spika, hawa waandishi wa babari watafute hizi habari wasikae tu pale ofisini wakasubiri kupokea habari.

Mhe. Spika, shughuli za Serikali kusema hivyo shughuli za Serikali huwa hazipati muda wa kuelezwa katika hii Taarifa ya Habari. Mheshimiwa Mzee wetu Abeid Aman Karume alianzisha chombo hiki ili zile shughuli za Serikali zinazotekelezwa katika nchi zionekane wananchi waweze kuona maendeleo ya nchi yao.

Mhe. Spika, nikitoka hapa niende kwenye *TVZ* Pemba. Mhe. Spika, *TVZ* Pemba haipatikani hasa Mkoa wa Kaskazini Pemba sijui huko kwenye Wilaya ya Chake Chake.

Mhe. Spika, nikitoka hapo niende kwenye hivi ving'amuzi. Mhe. Spika, wameweka ving'amuzi, lakini hivi vya *TVZ* hazipatikani zile *channels* ambazo wameziweka kwenye ving'amuzi, hazioneshi *channels* hizi haziendi na utamaduni wa Wanzanzibari. Mhe. Spika, tukiangalia utamaduni wetu wa Wazanzibari umepotea kabisa. Nimuombe Mhe. Waziri na tukiangalia wizara hii Naibu Waziri ni mwanamke, nimuombe Mhe. Naibu Waziri aandae muda maalumu wa kukutana na waandishi wa habari ili auelezee utamaduni wetu wa Wanzanzibari.

Mhe. Spika, kwenye ukurasa wa 19 wamesema wametekeleza kulipa pesa za likizo pamoja na *over time* kwa wafanyakazi. Lakini Mhe. Spika, kuna malalamiko ya wafanyakazi hawapatiwi *over time* wala posho la likizo. Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri atakapokuja aje anieleze ni sababu gani hawa wafanyakazi ikawa hawapatiwi pesa hizi za likizo na *over time*.

Mhe. Spika, kuna wafanyakazi wako hapa toka asubuhi saa 3 mpaka wanaondoka muda mwengine wakati wa kula mchana, sisi tunaweza humu tukachelewa tukaondoka saa tano za usiku au saa sita. Mhe. Spika, posho hili ambalo wanalipwa wafanyakazi hawa kwa kweli halitoshi. Mtu unamuweka hapa toka asubuhi anaondoka usiku siku nyengine unamlipa shilingi elfu tano ile chai ya asubuhi basi haitoshi.

Mhe. Spika, nikitoka hapo niende kwenye Ofisi Kuu Pemba. Mhe. Spika, Ofisi Kuu Pemba iko kule kwa kuwa malengo ya kuwasaidia wananchi. Ofisi Kuu Pemba viongozi wetu wa Serikali sasa hivi imekuwa na viongozi wengi. Viongozi wanakwenda kule Pemba, anaweza kwenda Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais, Mhe Makamu wa Pili wa Rais na Mhe. Rais mwenyewe muda mwengine anaweza akaweko kule. Lakini hizi *camera* kutokana na upungufu ulioko kule Pemba wanapokwenda viongozi hawa hulazimika zitoke huku Unguja ili zi-*serve* kule Pemba. Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri aje anieleza katika bajeti hii wamejipanga vipi kule Pemba kufikisha hizi *camera*.

Mhe. Spika, kwa kuwa Wizara hii ya Habari ni wizara yangu nilikuwepo katika kipindi cha miaka miwili na nusu naomba niunge mkono hoja hii asilimia kwa mia.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Mhe. Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii kuchangia hotuba hii ya Waziri wa Habari na Utamaduni, Utalii na Michezo Zanzibar.

Mhe. Spika, kwanza kabisa sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kunijalia kuwa katika hali ya uzima na afya njema. Na kuweza kuniruhusu kusimama mbele ya Baraza lako hili kutoa maoni yangu katika mchango huu.

Mhe. Spika, naomba uniruhusu kuchukua nafasi hii kumpongeza Mhe. Waziri pamoja na Naibu wake na watendaji wake wote katika kupanga safu nzuri ya habari.

Mhe. Spika, napongeza mfumo wa utangazaji tulionao wa redio na *television.* Mhe. Spika, kunakuwa na vipindi vizuri vya kuelimisha jamii, kwa mfano kunakuwa na kipindi kama vile mawaidha ya dini yanaelimisha jamii katika imani zetu tulizonazo lakini inashangaza kipindi kile cha imani ya kidini baada ya muda mfupi kinafuatana na ngoma za "Ndombolo yasolo".

Sasa kule tumefundishwa vizuri lakini muda mfupi tunapotoshwa. Namuomba sana Mhe. Waziri kunapokuwa na kipindi kile cha mawaidha basi vipindi vinavyofuata viwe na maadili mema. Lakini hakimalizi hiki kunakuwa na mtiririko huo ambao unaotupotosha. Hii inakuwa haipendezi kabisa.

Mhe. Spika, nikienda katika Idara ya Habari Maelezo, kuna habari kadhaa zinatolewa kwenye redio na *television* ambapo hapana shaka ni elimu. Ni elimu nzuri kwa jamii na kutoa mafunzo mazuri. Vipi Mhe. Waziri baada ya habari hizo nzuri baada ya taarifa ya habari nayo kunakuwa na maelezo baada ya habari, lakini vile vile baada ya maelezo baada ya bahari kuna na aya za

Qur-ani na hadithi ya Mtume (SAW), basi kuna mengine mazungumzo ya habari, mimi naomba baada zile aya za Qur-an na hadithi za Mtume (SAW) basi kuwe na neno jengine linajijenga pale sio maelezo baada ya habari haipendezi, hapa si pahala pake. Isipokuwa watafute kwengine waweke kama mazungumzo baada ya habari au maelezo baada ya habari.

Mhe. Spika, nikiendelea na mchango wangu katika Idara ya Habari na Maelezo ni moja ya kazi zake zinazojulikana na kusimamia mikutano ya wana habari. Lakini inasikitisha sana wanahabari hao hawana sehemu ya kufanyia mikutano yao, ni tatizo. Hapa namuomba Mhe. Waziri akija anifahamishe kwa kina, wenzetu kule Tanganyika wanao ukumbi wa Maelezo ya Habari wanafanya mikutano na hii pia inachangia pato la Idara husika, lakini hapa sifikirii kama upo. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri na hapa isaidie Idara ya Maelezo Habari kupata ukumbi wa kisasa ili ipate kufanya mikutano yao kufanyakazi zao kwa ufanisi kabisa.

Mhe. Spika, nikija katika mchango wangu Shirika la Magazeti. Hili linatoa taaluma nzuri watu wanasoma na wanapata habari muhimu lakini katika taaluma hizi zinazotolewa kwenye magazeti, likishasomwa watu hulitupa au kufungia samaki au maandanzi. Hebu Mhe. Waziri nataka ukija hapa utuelezee vipi lina hifadhi gani gazeti kama limeshasomwa linaweza kuhifadhiwa vipi au ni vyema kufungia maandazi tu. Ninapendekeza *TV* kuwa na kipindi maalum cha kusoma gazeti na sio gazeti moja tu. Tusome kama wenzetu wanavyosoma na kuwe na kipindi maalum cha kusoma magazeti kama wenzetu wanavyofanya.

Mhe. Spika, nikitoka hapo nakuja kwenye sekta ya utalii katika ukurasa wa 7. Ni ukweli usiopingika kama sekta ya utalii inaongeza pato la taifa katika nchi hii lakini ukiangalia huko mbele tunakokwenda utamkuta mzalendo hafaidiki na nchi yake kwa nini niseme hivyo, nasema hivyo kwa sababu za msingi kila eneo zuri basi limetengwa kwa mambo ya utalii, ukizikuta fukwe zile zote basi ni sehemu ya watalii, wazalendo iko siku hata kupita itakuwa dhiki. Ukikuta sehemu za bahari halikadhalika nazo maeneo yametengwa kwa sababu ya utalii na kuna siku mtu atakuta hana sehemu ya kupita. Naomba Mhe. Waziri na hili nalo alione wazalendo awaone nao wafurahie nchi yao katika shughuli zao za kikazi.

Mhe. Spika, niende katika sekta ya utamaduni katika ukurasa wa 7 vile vile. Mhe. Spika, sekta ya utamaduni hii kunakuwa na michezo ya asilia, kwa mfano kulikuwa na mchezo wa ng'ombe na huu ulikuwa maarufu sana na sehemu nyingi mchezo huu ulikuwa unafanyika. Mchezo huu ulikuwa unafanyika Chwale na ni sehemu pekee ulipobakia mchezo wa ngombe, peke yake. Lakini Pujini ulikuwa unachezwa mchenzo huu na ulikuwa na wapenzi

wengi sana lakini ile asili imeachwa sasa. Kuna michezo ambayo haijengi utamaduni wetu.

Mhe. Spika, katika michezo mashindano ya ngalawa na madau yalikuwepo, lakini siku hadi siku yanaendelea kufa. Ilikuwa ukifika wakati wa mashindano ya ngalawa, kulikuwa na ngalawa zinatoka sehemu mbali mbali Unguja na Pemba. Kulikuwa na mashindano kuanzia Forodhani mpaka huko lakini sasa hivi yamepotea baada ya kutoka Bumbwini na sehemu mbali mbali nyengine ulikuwa unatoka. Michezo ya kuogolea hili lilikuwa ni jambo zuri sana hasa wilayani lilikuwepo na katika vijiji yalikuwepo mashindano ya kuogelea. Sisi kule Kojani tulikuwa tunafanya mashindano ya kuogelea, tunatoka sehemu ya pale bandarini ngazini mpaka Mwamba Mkuu hatua kubwa sana unachukua zoezi la nguvu. Lakini sasa tunaiomba wizara kufufua michezo ile kwa sababu katika kujenga mwili na kupata uzoefu mkubwa kila inapofika muda mashindano yafanyike.

Mhe. Spika, kulikuwa na mambo ya ngonjera hayo yote yalikuwa yanajenga utamaduni mzuri lakini sasa mambo yote hayaonekani haya. Mashindano ya ngoma za asili tulikuwa tunashuhudia pale Jadida kulikuwa kufanyike starehe hizi, lakini sasa hivi hazifanyiki tena na mambo ya msewe ilishamiri sana, lakini sasa inaondoka, imebakia pale Mchangamdogo lakini nayo itatoweka, tuliwahi kutoa vijana wakenda Nigeria kwa msewe. Lakini sasa hivi unapuuzwa kabisa, ule ndio utamaduni wetu ngoma za kiheshima. Mhe. Waziri tunaomba ufufue michezo hiyo.

Mhe. Spika, kulikuwa na michezo hii ya kuvuta kamba na kufukuza kuku yote inatoweka haionekani kabisa. Mhe. Spika, kulikuwa na bao la kete, wakitoka watu Pemba kuja kushindana hapa Unguja kwa kule Pemba kulikuwa na mzee hatari anapiga bao sana na huku Unguja kulikuwa na mzee Nkiwa, sasa hivi michezo hii imepotea hakuna kabisa na ilikuwa ni michezo mizuri na yenye heshima.

Mhe. Spika, katika Baraza la Michezo la Taifa. Michezo ni mizuri na pia michezo ni ajira lakini tumeshuhudia katika timu zetu sasa hivi maandalizi ni madogo sana, ndio maana kila timu inafanywa kichwa cha mwandawazimu. Ni kukosa maandalizi kabisa, ili tuweze kufanya vizuri basi tunapoingia kwenye mashindano ya kitaifa tufanye maandalizi ya mapema kabisa ili tuweze kufanya vizuri tunakokwenda. Zanzibar ilikuwa na vipaji vingi sana na tunakumbuka hapa tulikuwa na wachezaji wetu mahiri na kule Pemba walikuwa wako kina Eddy Abdalla, Ali Chande, Abdi Malik wote hawa walikuwa na vipaji vizuri sana na hapa walikuwepo akina Juma Kidishi lakini wote hakuna sehemu ya kuwaenzi tena tumewatupa moja kwa moja kama hatukufanya hivyo hatuwezi kufanikiwa.

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo ni muhimu na nimesahau naomba ninukuu katika ukurasa wa 64. Mhe. Spika, majukumu ya msingi ya Shirika la Magazeti ya Serikali ni kusimamia uchapishaji wa magazeti ya Serikali Zanzibar, kuwaelimisha wananchi ili kukuza uelewa wao wa mambo kutoa habari zenye kuhamasisha jamii na kushiriki kwenye harakati za maendeleo ya nchi. Katika mwaka wa fedha 2012/2013 Shirika la Magazeti ya Serikali ilipanga kutekeleza malengo yafuatayo:

Kuna malengo kama matatu haya lakini hapa Mhe. Waziri nilikuwa naomba utekelezaji halisi. Mhe. Spika, Shirika linapenda kuliarifu Baraza lako Tukufu kuwa gazeti limeweza kuwafikia wasomaji wengi zaidi kwa kuongeza maeneo ya usambazaji kama vile Mkokotoni, Nungwi, Uroa, Makunduchi, Jambiani kwa Unguja na kwa upande wa Pemba maeneo yalioongezeka ni Madenjani, Wete, Konde na Mkoani. Sasa hoja yangu iko hapa.

Hapa kasema Mhe. Waziri katika kitabu chake hiki anasema analiambia Baraza lako hili tukufu kwa kuwa kuna ongezeko lakini mimi nasema ninapopajua mimi Madenjani bado hapajawa na ongezeko lolote la magazeti haya, hayapatikani mpaka nazungumza hapa hakuna magazeti yanayoletwa pale hakuna kabisa. Mhe. Waziri utakapokuja hapa unieleze kwa kina ili nipate kukupitishia bajeti yako.

Mhe. Spika, baada ya kuzungumza hayo naomba anipe majibu mazuri Mhe. Waziri ili nipate kuunga mkono. Lakini kama hajanipa maelezo mazuri basi itakuwa siungi mkono hotuba hoja hii.
Ahsante sana Mhe. Spika nashukuru.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, nachukua nafasi hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia uhai, uzima na furaha ya kuja hapa kwa ajili ya kutoa mchango kwa maslahi ya Wazanzibari.

Mhe. Spika, naomba univumilie kidogo hali yangu ya sauti si nzuri lakini nitachangia kadri ambavyo Mwenyezi Mungu atakavyonijaalia.
Nianze mchango kwanza kwa kumshukuru Mhe. Waziri, Katibu Mkuu na timu yake na wafanyakazi wote wa wizara hii kwa jinsi ambavyo wametuletea kitabu kifupi sana lakini kimeeleza maelezo ya kina ambayo yamepangwa vizuri.

Mhe. Spika, naomba kwanza niwakumbushe wenzangu pamoja na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwamba Serikali ndio inayo wajibu wa kuleta maendeleo, usawa, umoja na ustawi wa jamii. Serikali imechaguliwa kwa ajili ya kuleta huduma za jamii, serikali imechaguliwa kwa ajili ya kuleta maslahi ya Wazanzibari wote.

Mhe. Spika, lakini tumejenga tabia Zanzibar lazima tuwe wazi kwamba kila mtu anayebahatika kuchaguliwa wa Rais au kuteuliwa, huwa anafikiria kuwa yeye ana hadhi ile ile ya Rais na anayeteuliwa na Waziri basi ana hadhi ile ile ya waziri, wanasahau kwamba wameteuliwa kwa ajili ya kumsaidia Mhe. Rais, wawe wameteuliwa kwa ajili ya kumsaidia Mhe. Waziri. Mhe. Spika, mimi naomba utamaduni huu kama Wazanzibari tuuwache na tujue kwamba Rais anapokuteuwa na waziri anapokuteuwa ni kwa lengo la kukusaidia, kwa sababu Rais ni mmoja lakini anatakiwa atoe huduma katika nchi nzima.

Mhe. Spika, nasema hayo kwa sababu yanayofanyika Zanzibar na hasa wizara hii, inaonesha wazi kwamba watu wanajiona wao ndio ma-Rais, wao ndio mawaziri na wao ndio Wazanzibari hasa wanaostahiki kupata haki mbali mbali. Mhe. Spika, natoa wito tuache tabia hiyo na tuone kwamba sote tuna wajibu wa kuwahudumia Wazanzibari wale wanyonge walioanzia Micheweni hadi Makunduchi kwa Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, kwa msingi huo basi niseme kwamba mimi binafsi nampongeza sana Mhe. FeruzI. Namwita mheshimiwa kwa sababu aliwahi kuwa Naibu Katibu Mkuu wa CCM Zanzibar. Mhe. FeruzI aliwahi kuwa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi na kwenye historia yake sijaona pahala ambapo aliwagonganisha Wazanzibari, daima alikuwa akijenga hoja kwa msingi ule ambao yeye anauamini, bila shaka chini ya Chama cha Mapinduzi lakini alikuwa anajenga hoja, hoja ambazo kila mtu akisikia alikuwa anaona kuwa ni hoja za msingi.

Mhe. FeruzI daima alikuwa anawaunganisha Wazanzibari badala ya kuwagawa, kwa sababu Rais amemteuwa kushika nafasi ya kushika nafasi ya kuongoza sekta ya utalii, basi nina imani kwamba sekta hii itakwenda vizuri na pia yeye atakuwa ni chanzo cha kuwaelimisha wale watendaji wengine ambao wao sio wanasiasa ni wataalamu, lakini pengine hawafahamu lugha za wanasiasa au pengine hawajui malengo ya serikali hii.

Mhe. Spika, mimi nimuombe sana kaka yangu Mhe. FeruzI awaelimishe watendaji wenzake wajue malengo ya serikali, wajue malengo ya *GNU* na wajue kwamba sote wana siasa lengo letu ni kuwahudumia Wazanzibari badala ya kuwagawa. Baada ya kutoa pongezi hizo Mhe. Spika, niseme kwamba ni vyema tukaunga mkono hoja pasiwe na sababu na pale mjumbe anapoona hana sababu ya kuunga mkono basi asionekane kwamba ni mkorofi. Muhimu humu tukishazungumza hoja ambazo zinafanyiwa utafiti kwa ajili ya kujiridhisha. Kwa hivyo, mimi kwa msingi huu Mhe. Spika, naomba nitamke wazi kwamba siungi mkono hotuba hii, sio siungi mkono kwa sababu namchukia Mhe. Waziri, sio kwa sababu namchukia Katibu Mkuu na timu

yake, hapana. Lakini nachukia utendaji mbovu wa wizara hii ambao hauleti ufanisi kama Mhe. Rais alivyokusudia.

Mhe. Spika, kwa hivyo nitatoa shilingi 100 kwa mafungu ya Idara ya Utumishi na Uendeshaji, nitatoa shilingi 100 kwa mafungu ya Shirika la Magazeti, nitatoa shilingi 100 kwenye sekta ya utamaduni na sanaa na nitatoa vile vile shilingi 100 kwenye Idara ya Mipango na Sera.

Maeneo yote hayo Mhe. Spika, hayaleti ufanisi kama vile ambavyo Rais mwenyewe alivyokusudia kuwachagua wenzetu hawa kuleta ufanisi. Mhe. Spika, nasema hayo kwa uchungu. Kaka yangu Mhe. Salmin Awadh alizungumza na mimi ni Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, tena namuheshimu sana na nakubaliana na mchango wake kwamba sio vyema tu kuwalaumu CCM au kuwalaumu CUF. CCM na CUF haijamtuma mtu afanye ubadhirifu kwenye mali za umma. Tunasema hayo mara nyingi kwamba kama mtu anafanya ubadhirifu wa mali ya umma au kama mtu anafanya ubinafsi asijiegemeze kwenye Chama cha Mapinduzi na Chama cha CUF, ni udhaifu, ubaya na ukorofi wake. Kwa sababu tukiwahoji hawa wanaofanya ukorofi huu, hawana barua rasmi waliyopewa rasmi wala hawana barua rasmi waliopewa na Chama cha CUF kwamba fanyeni ukorofi huu. Kwa hivyo, sisi Wawakilishi ndio tunatakiwa tuwadhibiti madamu hawana agizo la Chama cha Mapinduzi na wala hawana agizo la Chama cha CUF, kwa nini wafanye ukorofi kwa kuwafanyia wananchi. Mhe. Spika, naunga mkono hiyo hoja ya Mhe. Salmin Awadh kwamba tusiwalaumu sana CCM, wakati mwengine wao wenyewe wanakwazwa na binafsi wao ambao hawana imani na serikali hii.

Baada ya mchango huu Mhe. Spika, nasema kwamba siungi mkono hotuba hii kwa sababu wizara hii chini ya Mhe. Waziri imeshindwa kufikia ufanisi uliokusudiwa. Sio kwamba hawana uwezo, lakini kwa mtazamo wangu na uchunguzi wangu kwamba wao wenyewe wanagongana, wanafikiria hii ni keki yao. Hii sio keki ya Mhe. Waziri na watu wake, ni keki ya Wazanzibari kutoka Micheweni mpaka Makunduchi, wasifanye jeuri au asifanye kibri kwa sababu tumewaamini kwa kuwapa dhamana.

Mhe. Spika, wanapogombana wanagombania ndizi na wala mgomba sio wao ni aibu. Kwa hivyo, wasifikirie kuwa Rais amewachagua kwamba wao wagombane tu. Rais alimchagua Mkurugenzi yeye ndio Rais, alimchagua Kamishna yeye ndiye Rais, aliyechaguliwa bodi yeye ndiye Rais, hakuna. Rais amewachagua kwa sababu ya kuwahudumia watu wanyonge wa nchi hii.

Mhe. Spika, nasema hayo kwa sababu mimi siamini sana kwamba tatizo la wizara hii ni tatizo la fedha kwamba fedha ndogo. Sawa ni sababu moja ya msingi kwamba fedha ndogo na mimi naungana na Mhe. Salmini Awadh

kwamba ni lazima tuwatetee wizara wapate fedha. Lakini hiyo inayopatikana wanagawanaje ndani ya wizara yao, wanazingatiaje matumizi ya fedha hizo za umma ndani ya wizara yao.

Nasema hayo kwa sababu Mhe. Spika, wizara hii haina uchungu wa fedha na ushahidi wa hayo nataka Mhe. Waziri anijibu. Mtendaji mmoja wa wizara hii aliwahi kupoteza milioni 6 katika wizara hii, akachukuliwa hatua za ndani na hatimaye akarejeshwa pale pale. Je Wawakilishi tuamini vipi kama nyinyi mnaweza kusimamia fedha za umma kwa ufanisi na uadilifu.

Kwa hivyo, sio kwamba fedha ndogo tu lakini hawana imani, hawana utendaji bora na hawana nidhamu ya fedha. Mhe. Waziri unijibu sasa, fedha ambazo zimepotea shilingi milioni 6 kwa mtendaji ambaye si mwaminifu, alichukuliwa hatua na wizara yako baadae mkamrejesha, ziko wapi na kwa nini mmefanya hivyo. Kwa nini tuwaamini kuwapatia fedha nyengine wakati hamna uaminifu wa kutumia fedha za umma kwa msingi huo.

Mhe. Spika, wenzetu hawa wanagombania tu *digital* kama nilivyosema. Tatizo la *digital* Mhe. Spika, ni vita vya maslahi, sio kwamba hawana wataalamu katika wizara hii, wana wataalamu wengi tu lakini tatizo letu ni kwamba watu wanagombania maslahi. Ushahidi wa hilo Mhe. Spika, ni kwamba tulipotaka kuingia kwenye *digital* wizara hii ilikuwa na lengo la kumpaka mkandarasi kampuni ambayo itasimamia, mwanzo baadhi ya watendaji walikuwa na lengo la kusimamia kwa Kampuni ya Huwa Way ya China, ambayo gharama yake ilikuwa ni dola milioni 28, lakini wizara ikasema kwamba hizi fedha ni nyingi. Wakajenga hoja kwamba tutafute nyengine, wakampata *AGAPE* dola milioni 5, dola milioni 28 hadi dola milioni 5 maana yake zimepungua dola milioni 23, hadi hii leo watu wanagombana tu kwa maslahi. Kwa hivyo, kama mnagombana kwa maslahi wacheni hizi nafasi tuachieni nchi yetu, tuachieni wizara yetu nyinyi mkagombane, mnagombana kwa sababu ya keki tu.

Mhe. Spika, leo *AGAPE* hana anachokifanya, tunajua kwamba habari ni haki ya raia. Leo Pemba hatupati matangazo ya TV wala redio kwa ufanisi, nyinyi mnagombana tu, mnagombana na shamba ya marehemu bibi. Kwa hivyo, nyinyi tokeni kaeni pembeni mkagombane muwaachie akina Feruzi na wengine wajenge hii nchi, hatuwezi kuwaachia watu wakagombana kwa sababu ya maslahi. Nani asiyejua kwamba dola milioni 28 ni nyingi kuliko dola milioni 5, kama dola milioni 5 ataleta ufanisi kwa nini mgombane.

Mhe. Spika, ninayo barua hapa ya mkataba mwengine, huku kazi hiyo kapewa *AGAPE* jamaa tayari wanamtafuta *Star Times* tayari na yeye asimamie. Maana yake kama mtu hajapata asilimia 10 basi hajaridhika katika

nchi hii. Mhe. Spika, kwa hivyo sio sababu kwamba fedha ni ndogo, tatizo ni kwamba watu wanafikiria kuwa hii wizara ni yao, ni mali yao na watafanya watakalo. Mhe. Waziri ni lazima uturidhishe na mimi nakuomba kwamba sitaki unijibu kwa jumla, nijibu hatua kwa hatua kila nilichohoji, vyenginevyo mimi nitaridhika tuje tupige kura ili watu wote wakubali, lakini mimi nitakataa peke yangu. Lakini hatuwezi kukupa fedha watu wakavuruga kwa sababu ya utashi wao.

Sio agizo la CCM nasema tena wala sio agizo la Chama cha CUF wala sio agizo la Rais, ni utashi wa watu ambao wamejisahau wajibu wao. Mhe. Spika, katika hilo naomba nipate maelezo kwamba ndani ya kituo cha matangazo ya *ZBCTV* kumejengwa mnara wa *Tigo*, naomba nipate maelezo nani kajenga mnara ule na ninaambiwa kwamba kuna kodi pale ya dola 1,000 kwa mwezi tuambieni fedha hizi zimeingia wapi. Mnatumia fursa ambazo sio sahihi mnajinufaisha. Mhe. Waziri hebu niambie mnara ule wa *Tigo* nani kaidhinisha na dola 1,000 kwa mwezi ambazo zinatolewa na Kampuni ya *Tigo* zinaingia katika *account* gani, halafu leo utuambie kuwa mapato ya *ZBC* yanaingia hapa. Naomba unipe jibu hilo, vyenginevyo sitounga mkono hotuba hii.

Mhe. Spika, nikuombe sana kwa busara zako katika hoja zangu mimi uniachie nihoji moja moja na kama sikuridhika tupige kura, watu wote wakikubali shauri yao lakini mimi sikubali. Kwa nini, kwa sababu wanapotosha dhamira nzima ya serikali. Rais amewaamini watu lakini wanafanya utashi. Mhe. Spika, nchi hii Rais ni mmoja tu ni Dk. Shein na hakuna Rais mwengine hapa Zanzibar. Kwa hivyo haiwezekani kuwa Rais amekuamini halafu wewe unafanya utashi tu kwa sababu ya jeuri zako. Watu wanafikiria labda Urais ni ukoo. Kama mimi tumehusiana na Dk. Shein basi na mimi ni Rais na mjukuu wangu ni Rais, babu yangu ni Rais, hakuna. Rais nchi hii ni mmoja tu na ni lazima aheshimiwe kwa yale aliyoyazungumza.

Mhe. Spika, vile vile Mhe. Waziri anipe maelezo ya mnara wa Bungi ambao umetumia mamilioni ya fedha hakuna ufanisi. Mnara ule wa *FM*, leo anatuambia kwamba tuidhinishe pesa, halafu watu wakavuruge hakuna majibu. Kwa hivyo, nipatie maelezo ya mnara wa *Tigo* pale *ZBCTV* na pia nipatie maelezo ya mnara wa *FM* kule Bungi kwa nini hakuna ufanisi.

Mhe. Spika, niende kwenye maslahi ya wafanyakazi na hii nazuia vile vile Idara ya Utumishi siungi mkono na nitazuia fungu hili, kwa sababu katika watu ambao ni wakaidi basi ni Idara hii ya Utumishi. Tumezungumza kwa lugha zote, aliyekuwa Sheikhe alitoa mawaidha yake, aliyekuwa muimbaji ametoa nyimbo zake, kila mtu ametoa nasaha kwamba tuwapeni maslahi

wafanyakazi wetu ili ufanisi upatikane. Mhe. Waziri tumesema mara kadhaa kwamba posho la shilingi 5,000 kwa watendaji wetu haliridhishi ni kidogo.

Mhe. Spika, ni nani anayeishi kwa shilingi 5,000 wakati ni kazi yenye fani kubwa. Mhe. Spika, uliahidi wewe hapa kwamba utawapatia nguo kwa ajili ya huduma za hapa ofisini, hebu tuambie ni wangapi umewapatia nguo hizi na umetumia shilingi ngapi.

Mhe. Spika, jengine ambalo haliridhishi Mhe. Salmin Awadh Salmin amezungumza kwamba kuna mafundi wetu watano. Mafundi wale kweli walisoma cheti cha *FTC* pale Mbweni, lakini nina hakika *FTC* ambayo wewe ulisoma na mimi nilisoma hiyo hiyo *FTC*, ni tofauti na digirii ya leo ya kawaida. Wamekaa kwenye Idara hii ya Televisheni mafundi zaidi ya miaka 30, mnasema hamuwatambui vyeti vyao. Mimi natoa *challenge*, watafute digirii wako walete wafanye mtihani na wale mafundi wa *FTC* wa miaka 70 kama watawashinda wale mtihani wao, ni utashi tu.

Mhe. Spika, mwaka jana waliongezewa posho la mshahara wa shilingi 274,000, mmewapunguzia hadi shilingi 150,000, nani kapunguza. Kama Baraza waliidhinisha shilingi 274,000 linalotukasirisha, nani mwenye uwezo wa kupunguza. Kwa hivyo ni utashi tu.

Mhe. Spika, ninayo barua ya mfanyakazi mmoja ambaye ni fundi anaitwa Mussa Kheir Haji. Ni fundi wa mitambo ya TV, ni fundi mzuri tu, amestaafu juzi yuko Dar es Salaam TV analipwa shilingi 600,000 kwa mwezi, ushahidi huu hapa. Amestaafu juzi hapa mmemuacha kwa ukorofi wenu, leo yuko Dar es Salaam kule anafanyakazi, anapewa shilingi 600,000 kwa mwezi. Leo hapa mnawapa wazee shilingi 120,000 tukiwaambia mnasema nchi haina pesa, sio kweli. Kama hii nchi haina pesa kwa nini Mkurugenzi apewe zaidi ya shilingi milioni moja. Kwa hivyo, ni matumizi ambayo hamzingatii maslahi ya wafanyakazi.

Kwa hivyo Mhe. Spika, mimi siungi mkono kwa kuwaidhinishia pesa watu wakafanye jeuri. Kwa hivyo, huyu amestaafu na yuko Dar es Salaam anafanyakazi. Wamebakia sita wale pale, mwakani wanastaafu, wataona mwenzetu kaelekea Dar es Salaam na wakiondoka wale wanakwenda Dar es Salaam hakuna fundi mitambo hapa msidanganyane. Vijana wenye digirii ya kwanza wawe hawana uwezo, lazima wafundishwe na wakomae ndani ya watendaji wale wa serikali. Nasema msitafute kisingizio cha fedha ni utashi, ubinafsi na maslahi ambayo hamuyazingatii. Kama tatizo ni fedha kwa nini wengine wapate mshahara mkubwa zaidi na wengine wadhalilishwe.

Mhe. Spika, nimalizie kwa kusema kwamba huduma na sekta ya sanaa. Vile vile kuna mfanyakazi wa wizara hii ambaye alichora nembo ya Zanzibar. Mfanyakazi ambaye alichora nembo ya Baraza la Wawakilishi. Mara hii ndio ilipitishwa sheria ya hati miliki, alipaswa yule alipwe mpaka afariki na akifariki familia yake ilipwe. Aliombwa alipwe shilingi milioni 100. Mhe. Waziri Abubakar Khamis Bakary yule pale alimuomba na kumnasihi kwamba punguza, akakubali na Mhe. Waziri Abubakar Khamis akaandika barua ya kumlipa shilingi milioni 50,000,000, lakini hakulipwa mpaka leo. Mnamsubiri afe mje mumsifu tu, kafariki alikuwa mzuri na hodari, lakini kutoa fedha mkawaenzi hamuwezi.

Mhe. Spika, sheria ile ya hati miliki tuliipitisha hapa ni lazima alipwe, kama halipwi haki yake hatuwezi kuwadhalilisha watu. Mhe. Waziri mimi nikuombe sana kwamba simamia maelezo haya kwa kina. Mtu yule ambaye alichora nembo ya taifa. Kule Uganda kuna mwimbaji tu wa nyimbo za kawaida amedai dola 250 kwa nyimbo yake. Huyu mtu hapa aliyechora nembo mbali mbali anapewa shilingi milioni 25 au 30, halafu anaambiwa basi yamekwisha, ikiwa huyu haenziwi atakuja kuenziwa Bi. Kidude.

Mhe. Spika, wizara hii ina utashi mkubwa ni lazima wabadilike, wasijiegemeze kwenye misimamo ya vyama, vyama havijawatuma ni ubinafsi wao, ni ukorofi wao na lazima tuwashughulikie kwa misingi ya sheria. Mhe. Spika, baada ya hayo nasema siungi mkono hoja na nakuomba sana kwa busara zako kila nilipohoji basi nipatiwe majibu na siungi mkono mpaka niridhike kwa sababu wizara hii kwa kweli inawakandamiza wafanyakazi.

Mwisho kabisa Mhe. Spika, wamenunua kamera hawa wenzetu wa *ZBC* na niseme wazi kwamba nasikia kamera aliyewauzia ni Mhe. Raza, kwa nini mkanunua kamera moja kwa moja msipitie kwenye Bodi ya Manunuzi. Kamera moja iko Dar es Salaam na kamera moja iko Barazani. Kwa nini mkanunua kamera bila ya kuzingatia Bodi ya Manunuzi ya wizara, sio matumizi mazuri ya fedha, wala sio utaratibu mzuri wa sheria ya fedha. Kama hivyo ndivyo Mhe. Spika, Mhe. Waziri naomba unijibu hoja zangu hizo ili niipitishe bajeti yako, si hivyo tutasameheana na nitakuomba radhi sana sitopitisha bajeti yako, ahsante.

Mhe. Asha Bakar Makame: Ahsante sana Mhe. Spika, kwanza na mimi nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametuwezesha siku hii ya leo katika shughuli zetu za kila siku za kitaifa.

Lakini pia Mhe. Spika, nichukue nafasi hii nimpongeze sana Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wote ambao walikaa na kumsaidia katika kutengeneza hotuba hii ya bajeti. Vile vile niseme kwamba nampongeza sana

Mhe. Waziri, nasema haya kwa udhati wa moyo wangu, ninavyomuona Mhe. Waziri wa Habari anavyofanya kazi zake kwa mujibu wa utaratibu na kwa mujibu wa kuamini kwamba Rais amemteuwa yeye kuwa waziri na yeye aoneshe imani yake kwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Mhe. Spika, kwa nini nikasema haya, kwa sababu Mhe. Waziri hii ni wizara yake ya ngapi. Alipoondoka kule Mhe. Spika, kwa kweli aliwacha pengo. Sisemi mwengine hafai lakini baada ya kufika tu wizara ya uvuvi alichukua jitihada na katika mtu ambaye tumekwenda naye China, basi yale masomo ambayo tumepelekwa China basi ni yeye mmoja ambaye aliyaanzia kuyafanyia kazi waziri huyu wa habari. Kwa hivyo, mimi ni lazima nimsifu mtu akifanya vizuri ni lazima umpe wajibu wake. Hakuna kizuri kisicho na kasoro Mhe. Spika, hakuna wizara hata moja hata ikifanya vipi ni lazima na hila ziwepo, kwa sababu hakuna kinachokamilishwa, ni kutokana na watu wengine ambao hawajui wajibu wao, hawajui taratibu zao, hawajui malengo ya serikali hii ni malengo ya aina gani. Kwa hivyo, niwaombe mimi kama ni mtu mzima, wale ambao wanahisi wanataka kuchukua shilingi, basi niwaombe sana tumpe tena muda waziri huyu ili aweze kuyakamilisha yale ambayo mmeyazungumza humu aende akayatekeleze ipasavyo. Hilo moja.

Sasa Mhe. Spika, niingie kwenye mjadala. Maana mimi nikiwa na jambo kama sikulizungumza humu basi sina raha, na desturi yangu siku zote lile la kweli nalisema kweli na lile la uongo silizushi likawa la kweli.

Mhe. Spika, tumeingia hapa sisi wajumbe wako wa Baraza la Wawakilishi kwa kuwatetea wananchi, tumeingia hapa hakuna jinsia, tumeingia hapa hakuna ukusini au ukaskazini, tumeingia hapa sisi ni Wawakilishi wa watu wa taifa hili la Zanzibar.

Sasa leo hapa ndio nataka kuzungumza, maana juzi hapa mimi sikufurahi maneno yaliyozungumzwa. Hapa hakuna kamati inayoitwa ya Kipemba, hakuna kamati inayoitwa ya Kiunguja, hakuna kamati inayoitwa kwamba hii ni ya mtu binafsi au hakuna kamati inayoitwa hii ni ya Chaani au hakuna kamati inayoitwa hii ni ya Mtambwe, maana lazima na mimi nitaje kwetu. Hapa kuna kamati iliyoundwa na Baraza la Wawakilishi na kila Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi ana haki ya kutetea popote na ndio maana kamati hizi Mhe. Spika, zikawa zinatembelea sehemu mbali mbali. Hazikupangwa hizi zitembelee Pemba kwa maslahi ya Wapemba au Unguja kwa maslahi ya Waunguja.

Mhe. Spika, sio vyema tukafananisha Kisiwa cha Pemba na jimbo. Kisiwa cha Pemba ni miongoni mwa visiwa viwili vinavyounganisha Pemba na

Unguja, ndio ikaitwa Zanzibar. Zanzibar isingeitwa kama hakikujumuishwa Kisiwa cha Pemba. Mhe. Spika, hili nilisema nilizungumze kwa sababu naona tunaanza kuleta mambo ambayo yatatugawa miongoni mwetu, yatatugawa kiu-Pemba na kisha yatatugawa kiu-Donge, kisha yatatugawa kiu-Mkwajuni na kisha yatatugawa ki-Makunduchi. Sio vyema.

Hilo Mhe. Spika, nilisema nilizungumze na nalizungumza kwa nia safi kabisa. Mimi leo ukiniambia sikuhusu Unguja utanitukana. Mimi nimeolewa hapa Unguja, nimezaa na nimeshajukuu, isitoshe babu yangu mzaa mama yangu kaowa Bubwini, ana watoto na wajukuu, huyo ni babu yangu mzaa mama yangu mimi. Sasa utanitowaje mimi kuwa nisiwe Muunguja. Baba yangu ni Mpemba kahusu Tumbatu, utanitowaje mimi. Tusifike huko Mhe. Spika, sisi ni lazima tuwaoneshe tunaowaongoza na kuwatetea kwamba sisi ni kitu kimoja, tusilete sasa hivi baina ya sehemu na sehemu. Naomba sana kama mtu mzima wenu tuendelee kutafuta na kutetea maslahi ya nchi na maslahi ya wananchi, ili watu wetu watuone kwamba sisi ndio matumaini kwao.

Baada ya kusema hayo Mhe. Spika, sasa hivi nakwenda kwenye hoja kidogo sana, maana nilikuwa nakereketwa na hili. Mhe. Spika, nimetoa maelezo ya Mhe. Waziri lakini niseme tu kwamba katika suala la bwawani mimi nitamuomba Mhe. Waziri, kwa sababu hili suala la bwawani lilizungumza sana. Kwanza tuwathamini wale wafanyakazi ambao wameiweka bwawani mpaka leo ikawepo. Nayazungumza haya kwa nia safi kwamba ile bwawani kama sio wafanyakazi wale wameisogeza sogeza, leo ile bwawani isingekuwa bwawani, ingeshaota madudu, ingeshaporomoka, lakini kutokana na wafanyakazi hawa ambao tokea enzi ya bwawani imefunguliwa mpaka leo wako pale, tuwathamini na wao Mhe. Spika.

Kwa hivyo, namuomba sana Mhe. Waziri tuliwaita wafanyakazi wa bwawani wote tukazungumza na tukakubaliana, ikawa wengine waajiriwe ambao walikuwa wamewekwa wafanyakazi wa kutwa hawakuajiriwa na sasa hivi wameajiriwa. Najua kwamba ukimuajiri mfanyakazi kuna kipindi lazima umchunguze tabia zake, lakini huyu utamchunguzaje yuko miaka 30 pale utamchunguzaje na tokea afanyekazi hajafanya makosa. Kwa hivyo, naomba sana wapewe haki zao zote, kama ni kukopa benki wakopeshwe na kama ni kufanyiwa marupurupu yao yote wafanyiwe, tusidhulumu kitu ambacho sisi wenyewe hatukubali kudhulumiwa. Namuomba sana Mhe. Waziri, hili nilisema nije nilizungumze hapa kwa sababu nimetumwa. Sasa sitaki nionekane sikuifanyia kazi, wananisikia wenyewe watu wa bwawani.

Lakini jengine Mhe. Spika, nizungumzie suala la Kamisheni ya Utalii. Mhe. Spika, kulikuwa na Shirika la Utalii, kama alivyosema yeye mwenyewe waziri hapa na kama tulivyoliona. Lakini lile Shirika la Utalii mimi niseme

kweli kwamba lilipigwa vita na sisi wenyewe, haidhuru sasa halikufanyakazi vizuri. Tumeweka Kamisheni ya Utalii, kama tumeweka Kamisheni ya Utalii Mhe. Spika, basi tuipe nguvu zote kwa sababu ndio itakayokuwa dira ya kuleta watalii hapa Zanzibar, lakini kama hatukuipa nguvu zote za kifedha basi tutakuwa tunajidanganya na tukisema kwamba utalii sasa hivi ni uti wa mgongo. Mimi nasema bado haujakuwa uti wa mgongo. Tuiimarishe Kamisheni hii ya Utalii ipasavyo kwa mujibu wa kimataifa, maana wenzetu huko tusiwaone hivi, ndio hapa nikasema kwamba Kamisheni ya Utalii sasa hivi inatuletea tija, kwa sababu hii Kamisheni ya Utalii sasa hivi ndio utalii wenyewe hasa na ndio unaotuletea tija Mhe. Spika, tukitaka tusitake, namuomba sana Mhe. Waziri na naiomba sana Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo na naiomba serikali hasa kwamba bado ikae itafakari kwamba Kamisheni ya Utalii, kwa sababu tumevunja Shirika la Utalii nguvu zote tuzipeleke katika Kamisheni ya Utalii.

Mhe. Spika, nitoke hapo kwa sababu wenzangu wengi wamezungumza, nitoke hapo nije kwenye kiwanja cha watoto Pemba. Mhe. Spika, kama tulivyofanya rai tukasema kiwanja cha watoto hapa Unguja tumtafute mfadhili. Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Waziri tutafute wafadhili basi na kule Pemba, kwa sababu kile kiwanja nacho kule kiko pahala pabaya ni tofauti na Unguja. Kile kiwanja pale kipo pahala pabaya kwa sababu kina Unguja, kwa sababu kile kiwanja kiko kwenye bahari na kila kitu kinamong'onyoko Mhe. Spika, kwa hivyo tutakuja kukosa kaa na gando. *(Makofi).*

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, pamoja na wataalamu wake na hata kule kule Pemba watafute matajiri waliokuwa wazaliwa wapewe, ili waweze kutengeneza Kiwanja cha Watoto Pemba na wao watoto kule wafaidike na raslimali yao ya mapinduzi ya Zanzibar. Kwa kweli zile ni raslimali ya mapinduzi ya mwaka 1964 na mwenyewe Mzee Marehemu Abeid Amani Karume na inshaallah akulaze mahala pema na tutakutaja tu kwa mema yako uliyoyafanya. *(Makofi).*

Jambo jengine Mhe. Spika, nije katika vijana wetu ambao tunao humu ndani. Mhe. Spika, *wallahi* taratibu na sheria lakini kama ingekuwa taratibu na sheria zinaturuhusu basi hawa vijana tungewatia sehemu yetu ya Baraza la Wawakilishi. Kwa kweli ni vijana ambao tuwaangalie sana, sisi hapa tukikaa dakika 10 basi dakika ya 15 tunatoka nje, yaani humjui kijana wala mzee humu ndani lakini wao kwa kweli wanafanyakazi haidhuru ni miongoni mwa kazi zao, lakini kila kazi inategemea uzito wake. Vijana wetu hawa wanafanyakazi na wale walioko kule juu wanafanyakazi nzito sana. Kutokana na hali hiyo, Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri wawe na posho maalum tena aje aniambie na tena nitakuwa mtu wa mwanzo katika kamati hii kuja

kupinga kama hawakuwa na posho maalum hawa kwa nia ya kufanya mema. *(Makofi).*

Nikiendelea na mchango wangu na ninachangia kidogo kidogo na sasa hivi nitamaliza.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, malizia kwa dakika 5.

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Spika, nije katika masuala ya michezo tunavyo vilabu mbali mbali.

Kwanza nije kwenye *ZFA* na hapa ninamuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, kwamba tunapochagua viongozi katika masuala yetu hapa ya mipira basi sisi viongozi tusiwe *bias*, isipokuwa sisi viongozi inatakiwa tusimamie na haidhuru mimi ninayo timu yangu. *(Makofi).*

Kwa mfano mimi Asha Bakari Makame ninayo timu yangu ya Mwenge kule Pemba, lakini haina maana kwamba mimi timu yangu ya Mwenge imefanya vibaya nikaja nikaitetea humu. Jambo la msingi natakiwa niwafundishe taratibu, sheria pamoja na kanuni tulizoziweka za vilabu na mambo mengine. *(Makofi).*

Mhe. Spika, nataka nimueleze Mhe. Waziri kwamba hiyo klabu ya Mwenge imefanyiwa madhambi, sasa namuachia yeye Mhe. Waziri kwa sababu huyo mkuu wa *ZFA* Pemba anayo timu yake. Kwa hivyo namuachia yeye na *ZFA* yake Pemba, tupate jawabu kwamba wasidhulumiwe maana na timu ile nayo ni ya zamani na haifi ikawa kwa sababu tena aah! Haifi moyo.

Mwisho Mhe. Spika, niwaombe Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwamba tumpe muda Mhe. Waziri wetu, ili yale tunayomueleza aende akayafanyie kazi, basi nakuombeni kasma zote tuunge mkono wizara hii. Pamoja na yote hasa mwanangu Mhe. Hija Hassan Hija, Mhe. Ismail Jussa Ladhu pamoja na Waheshimiwa Wajumbe wote wale ambao wana dhamira ya kuchukua shilingi 1 au 100, basi waziache shilingi 100 hizi, ili zizidishe kufanyisha yeye aweze kufanya kazi kwa ufanisi, isipokuwa tumsubiri mwakani sasa na kama hakuyatimiza yale basi na mimi nampiga vigongo vile vile. *(Makofi).*

Baada ya kusema hayo, Mhe. Spika naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Mhe. Spika, ahsante sana. *(Makofi).*

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe tunakushukuru. Sasa tumkaribishe Mhe. Hamza Hassan Juma na baadaye Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, na mimi nikushukuru kwa kunipa nafasi hii kwa ajili ya kuzungumza machache katika Wizara hii ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo.

Mhe. Spika, mimi moja kwa moja nataka nianze kwa kutoa pongeza kwa Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wote kwa kazi kubwa ambayo wanayoifanya katika kutupatia taarifa mbali mbali kupitia vyombo vyetu vya habari. Vile vile kusimamia na kulinda pamoja na kuimarisha utamaduni wetu wa Zanzibar. Sambamba na hilo kusimamia gurudumu na uti wa mgongo kwa utalii wa nchi yetu. Pia jukumu la kusimamia masuala mazima yanayohusu michezo.

Tukiangalia majukumu haya yote yanawagusa wananchi moja kwa moja. Kwa hivyo, naomba sana Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake kupitia kwako Mhe. Spika, kwamba wasikilize mawazo ya Waheshimiwa Wawakilishi na pale ambapo tunahitaji kuyafanyia kazi kwa haraka basi tuyafanyie kwa haraka, lakini yale ambayo yanahitaji muda basi ni vizuri wakawa wanatupa maelezo ya kutosha ili na sisi tuwe na matumaini yale ambayo tunayopendekeza kwamba tujue utekelezaji wake unakuwa katika hatua gani.

Mhe. Spika, mimi nataka nianze moja kwa moja katika Shirika la Utalii. Kwa kweli kwa kipindi kirefu tumekuwa tukisema sana kuliimarisha Shirika letu la Utalii, lakini pengine kwa sababu moja au nyengine imefika pahala serikali imeweka mkono chini. Sasa mimi nadhani Mhe. Spika, hili wazo sio baya kwa sababu huwezi kubeba mzigo usiobebeka na lazima itafika pahala itabidi uutue. Kwa hivyo, nafikiri liwe funzo kwa mashirika yetu mengine ya serikali.

Mhe. Spika, mimi nilitegemea sana kwa kuwa uti wa mgongo wa uchumi wetu kwa sasa ni utalii, basi ilikuwa ni vyema kabisa kufanya kila jitihada kuhakikisha kwamba serikali ina chombo chake ambacho kina-*operate* katika shughuli nzima za utalii, pamoja na kwamba kuwa na Kamisheni ya Utalii lakini hili shirika kwa kweli ni chombo ambacho kingeliweza kutusaidia sana. Vile vile nadhani bado hatujakubali kubadilika katika kutekeleza hasa zile sheria mbali mbali ambazo tunazozipitisha. Kwa mfano, inawezekana kwamba tunapitisha sheria lakini katika kutekeleza tunakuwa tunahofu, yaani tunatawaliwa zaidi na hofu kuliko kujiamini.

Mhe. Spika, nadhani kuna taratibu tulizipitisha hapa kwamba serikali ilijitoa katika kufanya biashara, lakini bado kuna sheria tulizipitisha hapa kwamba serikali kuingia kwenye mashirikiano aidha makampuni au taasisi nyengine zozote binafsi kuweza kushiriki kikamilifu katika mchango wa kiuchumi.

Mimi ningelitarajia sana kwamba Mhe. Waziri baada ya kubebeshwa jukumu hili, angelifanya jitihada za makusudi za kuhangaika na kutafuta *investors* mbali mbali kushirikiana katika kuliendeleza Shirika hili la Utalii. Kwa kweli kwa upande wetu wala tusingekuwa na gharama kubwa kwa sababu tayari kuna *assets* za shirika tunazo. Kwa maana hiyo, kumpata mbia ilikuwa yeye ni kuja kuendeleza pale ambapo sisi tumekwama.

Lakini leo kwa masikitiko kabisa ambayo ni makubwa sana leo tumekuja na shoka kulivunja kabisa Shirika hili la Utalii. Sasa Mhe. Spika, namuomba sana Mhe. Waziri kwa kuwa hii shoka bado haijakata mpaka moyo wa shirika basi nafikiri kuna muda anaweza kuendelea na jitihada zake binafsi, ili kuangalia labda kuna njia gani anaweza kupenya. Mhe. Spika, maamuzi haya ya serikali na Mhe. Waziri kama akiweza kujenga hoja vizuri akiweza kupata *investors* wakaingia ubia, nadhani serikali itaweza kumkubalia. Mhe. Spika, mimi ninao ushauri wa bure katika hotuba tofauti na leo mara ya tatu naendelea kusema kwamba kuna mkutano mkubwa sana utafanyika nchini Marekani na mkutano huo kutakuwa na *investors* zaidi ya 150, wafanyabiashara, wawekezaji wakubwa matajiri duniani ambapo hata Zanzibar imepata mualiko huo.

Kwa hivyo, nikisema hivyo nadhani nimeshasema kwenye *hansard* zangu zikirejewa kuhusu mualiko huo. Mhe. Spika, nadhani Mhe. Waziri wataalamu wake wangetafuta namna ya kushiriki kwenye mkutano huo, kwa ajili ya kuangalia na tunaweza kuja kupata muokozi akaliokoa Shirika letu la Utalii na serikali yetu ikaendelea kuwa na hisa, ambapo hisa zetu ni zile *assets* ambazo tunazo na wao wenzetu wakaja kujitahidi katika kusaidia ku-*operate* hizi huduma za utalii.

Mhe. Spika, nafikiri jahazi yetu bado inakaribia ufukweni ya Shirika la Utalii basi naamini wimbi kubwa likipiga inaweza ikaelea na ikarudi tena baharini, ili kuweza kutuvusha, kwa sababu mimi nasikitika sana kwamba nchi za visiwa na tunategemea zaidi uwekezaji wa utalii na halafu sisi tukawa moja kwa moja tuna-*monitor* tu lakini hatushiriki moja kwa moja katika kuendeleza huu utalii wenyewe.

Mhe. Spika, kama nilivyosema kwamba huo ni ushauri wangu na yeye mwenyewe nampa nafasi pamoja na watendaji wake waangalie wataweza kutusaidia vipi.

Nikiendelea na mchango wangu sasa naomba nizungumzie kuhusu Hoteli ya Bwawani. Kwa kweli narejea tena kusema kwamba katika mafunzo ambayo tuliopata nchini China moja ni kulinda na kuenzi yale mambo mazuri ambayo tuliyoanzishiwa na viongozi wetu waasisi pamoja na kuyaendeleza. Mhe.

Spika, hata na mimi sivutiwi kabisa kuona Hoteli ya Bwawani imegeuzwa madhumuni yake kutoka kuwa hoteli na inatumika hivi sasa kama ni sehemu za maofisi ya serikali.

Eneo hili pia Mhe. Spika, bado namuomba Mhe. Waziri ajaribu kuangalia uwezekano wa kutafuta utaratibu wa *PPP* kuweza kuiendeleza hoteli ile na hoteli ipo pazuri tena *view* yake nzuri naamini Mhe. Waziri akijitahidi basi anaweza akapata *investors* na ikarejea katika hali yake ambayo iliyokusudiwa pale mwanzo.

Tukiacha hoteli yenyewe ya Bwawani, sasa tuje katika wafanyakazi wa Hoteli ya Bwawani. Mhe. Spika, mimi ninasikitika sana ninapowaona wafanyakazi wetu wa serikali wanasikitika hasa katika suala zima la maslahi yao, wanajiuliza sisi ni wafanyakazi wa serikali au kampuni ama taasisi gani. Mhe. Spika, leo inafika pahala wafanyakazi wale wanashindwa hata kuwa na dhamana ya kukopeshwa katika mabenki.

Mhe. Spika, sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tukitaka kukopa wewe ndio mdhamini wetu na unamuagiza Katibu, wadhamini hawa wajumbe wangu ili wakajiweke sawa katika kujitengenezea aidha maisha yao au majimbo yao. Sasa leo inapofika pahala wafanyakazi wa Hoteli ya Bwawani hawana dhamana wa kuwawekea *guarantee* kwa kweli ni suala la kusikitisha sana.

Tukiacha hivyo Mhe. Spika, labda Mhe. Waziri aje anisaidie maelezo sijui katika Mfuko wa Hifadhi ya Jamii wanaekewa ile akiba yao. Sasa kama inafika pahala wanaekewa fedha zao katika Mfuko wa Hifadhi ya Jamii, kuna sababu gani inayowakwamisha katika kupata fursa nyengine hasa kama hizo za mikopo.

Vile vile Mhe. Spika, wafanyakazi hawa kama nilivyosema hawajui kama ni popo au ndege, yaani hata ile hatma yao hawaijui. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, wakati atakapokuja kufanya majumuisho atusaidie hasa wale wafanyakazi wa Hoteli ya Bwawani ni wafanyakazi wa serikali au wafanyakazi wanaokuja kufanyakazi kwenye hoteli ile na halafu wanakwenda zao kukaka ili mtu ajijue *future* yake. *(Makofi).*

Kwa mfano, sisi siku zote tunapiga kelele kwamba tunalalamikia kuhusu wawekezaji kwamba wanawaajiri wafanyakazi katika mahoteli mikataba haina uhakika. Sasa leo kama wawekezaji wameshaanza kusikiliza kilio chetu na kupitia Waziri makini kabisa Mhe. Haroun Ali Suleiman, kwamba tayari wawekezaji katika sekta binafsi wameanza kutoa mikataba ambayo inaonesha

haki zao, stahili zao, hatma zao pamoja na kinga zao kiafya na mambo mengine. Kwa hivyo, leo inakuwaje kwa taasisi yetu hii ya serikali Mhe. Spika, kwamba wafanyakazi wanaishi katika maisha ambayo hayana uhakika. Kwa hivyo nadhani Mhe. Spika, suala hili Mhe. Waziri angejitahidi akaja akatupa maelezo ya kutosha, maana moja katika buti zangu iko hapa kwenye Hoteli ya Bwawani ili tupate maelezo ya kutosha na tupate uhakika hasa na wao wenyewe wajisikie leo kwamba tukimaliza hii bajeti, wao ni wafanyakazi wa serikali au ni wa *part time*. *(Makofi).*

Mhe. Spika, nafikiri Mhe. Waziri kwa ninavyomjua kwamba si mtu mbabaishaji, ni mtu ambaye unapojenga hoja basi anafanya utafiti na anakuletea jawabu ambayo ni ya uhakika. Kwa hivyo, ninatagemea nitapata jawabu nzuri sana katika hili. *(Makofi).*

Mhe. Spika, ukurasa wa 18 kifungu cha 42 kinazungumzia Shirika la Utangazaji. Kwanza nataka niipongeze serikali kwa kusikia kilio chetu sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa kuona kwamba vyombo vyetu hivi *ZBC Radio* na *ZBC Television*, kwamba ni vyombo ambavyo ni vikongwe vyenye asili lakini miendano yake inasuasua. Vile vile tulisema sana kwamba vyombo hivi kuendelea kuwa chini ya idara havifiki pahala na wala haviwezi kufika pahala vikafanyakazi katika ushindani hasa huu sasa hivi wa sayansi na teknolojia.

Mhe. Spika, tunamshukuru sana Rais wetu wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kusikia kilio chetu na akaamua kwa makusudi kukubali hoja ya kuanzisha Shirika la Utangazaji ambapo *process* yake ilianzia tokea katika kipindi cha awamu ya sita. Lakini tujiulize tulipounda hili Shirika la *ZBC* je, tuliangalia mahitaji ya shirika au tulianzisha kwa utashi na wala sitaki niilaumu serikali, kwa sababu sisi wana siasa ndio tuliokuwa tuna utashi wa kuliondoa Shirika la *ZBC Radio* na *Television* kutoka katika Idara kuja kwenye Shirika. Mhe. Spika, tuangalie je, kuna mazingira fulani tuliyaandaa katika kuliandaa au kuliunda hili shirika, lazima tukiri kwamba haja ilikuwepo na ikatupelekea katika kuanzisha.

Matokeo yake hatukutafuta mtaji wa kuiondoa katika idara kuileta kwenye shirika, kwa sababu chombo chochote unapokitoa katika idara kuja kwenye shirika, kwani shirika ni chombo ambacho kinachotakiwa kijitegemee na mwanzo utakilea kidogo kidogo, lakini baadaye itafika pahala kiwe kinajitegemea kimapato na kiuendeshaji.

Mhe. Spika, wafanyakazi waliotoka katika Idara hizi za *Television* na *Radio*, ndio wafanyakazi wale wale tunaondelea nao katika shirika. Je, wote wanao uwezo wa ku-*compete* kuingia katika ushindani wa hivi sasa na taalamu ya

science na *technology*. Je, tuliandaa mtaji wa kuwastaafisha aidha kwa lazima au hiari ili kuweza kuajiri wengine ambao watakaoweza kuingia katika ushindani.

Mhe. Spika, nilijaribu kufuatilia wenzetu *TBC*. Kwa kweli *TBC* walipoanzisha Shirika la *TBC* basi serikali ilitafuta fedha na ikastaafisha pale wafanyakazi pamoja na kuwalipa mafao yao wale ambao wa lazima na wengine wa hiari, walazima ni wale ambao mazingira yao hawawezi wakaingia katika *technology* ya kisasa na sisi hatukufanya hivyo. Kwa hivyo, shirika hili ni lazima tukubali na kama mfano ingelikuwa Mhe. Spika, kama ingelikuwa utaratibu wetu wa bajeti tunaweza kusema kwamba kuna fungu liongezwe hapa, basi ningelisema hapa leo lazima tubane kule katika bajeti kuu ya serikali ili fedha zaidi ziongezwe huku.

Lakini utaratibu wetu wa bajeti, mimi nadhani Kamati ya Uongozi itabidi tukae tuangalie wenzetu Bunge la Jamhuri ya Muungano utaratibu walioanzisha hivi sasa kwamba unahisi umezaa mtoto lakini hukujitayarisha katika maandalizi ya kumtafutia vifaa, ili aweze kuendelea vizuri basi unaweza kumegua fedha kiasi fulani kutoka sehemu fulani na kuongezea, ili mtoto huyu awe na ufanisi mzuri.

Mhe. Spika, ukiangalia kutokana na muda siwezi kuvitaja vyote. Lakini ninayo orodha ya vifaa zaidi ya 25 *TBC Radio* na *Television* hawana tena ni vifaa vya kisasa. Sasa Mhe. Spika, sitegemei kama chombo hichi au vyombo hivi vinaweza vikenda kwa ufanisi.

Jambo ambalo nataka kuliomba na Mhe. Spika unataka kuniambia kwamba bado dakika tano nimeshakuona ulivyokaa.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, unazo dakika kama tatu basi.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Hiii! Mhe. Spika, naiomba serikali hii ya mwaka huu ndio imeshapita au kama inawezekana Mhe. Waziri akajenga hoja apeleke *paper* kwenye *cabinet*, ili aombe fedha katika Mfuko Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kuliongezea fedha Shirika letu la *ZBC Radio* na *Television*, ili waweze kununua vifaa vya kisasa vyenye ubora na vinavyoendana na wakati, vyenginevyo Mhe. Spika, tutakuja hapa tutalaumu kumbe sisi wenyewe tunataka kumkama ng'ombe ambaye hata hayo maziwa yenyewe hana.

Mhe. Spika, nikiangalia shirika hili limepita katika mikondo mingi limeanza tokea mwaka 1974 *Television* na likenda mpaka mwaka 1984 na vifaa ambavyo vilivyopatiwa mwanzo vilikuwa na maisha ya miaka 10. Kwa hivyo,

kuanzia mwaka 1994 matangazo yale ya *television* yalikuwa yanarushwa kwenye gari kwa muda wa miaka 10, yaani ndani ya gari *OB van* linakwenda ndio linarusha matangazo.

Sasa baada ya miaka 10 mwaka 1994 tukaanza kupata ufadhili wa Japan na Ujerumani kipindi kile Mhe. Spika ndio tukaweza kwenda na vifaa hivi mpaka leo. Kwa maana hiyo, kuingia kutoka katika mkondo mmoja kwenda kwenye mkondo mwengine Mhe. Spika, tumekwenda katika hali ya kusuasua sana. Mhe. Spika, nadhani tuliboreshe hili shirika letu kifedha na baadaye tuwasikilize katika utendaji wao.

Lakini kitu ambacho ninachokiomba inaonesha *ZBC Radio* na *Television* kidogo kuna matatizo katika mambo ya kiutawala. Mhe. Spika, kitu ambacho ninachokiomba kwamba uongozi uwe na utaratibu wa kuanzisha zile *morning call*, bila ya *morning call*, taasisi yetu hii kwa kweli tutakuwa tunaendelea kulaumiana na kushutumiana bila sababu za kimsingi na wakianzisha hizi basi nafikiri matatizo yote wafanyakazi katika suala zima la maslahi yao. Vile vile Mhe. Spika, *scheme* kwa sababu tumeanzisha shirika lakini hakuna na hata hizo posho zao ni za kubabaisha tu. Kwa hivyo, nadhani haya ni masuala ambayo tunaweza tukayaboresha na tukajenga. Hata hivyo, tunalo deni kubwa sana la umeme na hapa nina karibu milioni 416,000,000/= tunadaiwa, simu *TTCL* tunadaiwa karibu milioni 43,000,000/= na madeni mengine karibu milioni 124,000,000/=, yaani karibu milioni 583,000,000/= tunadaiwa hapa.

Sasa je, fedha hizo tunazo na kwanza hizi za Shirika la Umeme Mhe. Waziri atakapokuja hapa itabidi anieleze, kwa sababu tulifanya semina Shirika la Umeme na wao wako hali kidogo sio nzuri na taasisi hizi kwa kuwa kuna mafungu hapa ya fedha, nadhani Mhe. Waziri aje atusaidie atueleze ataweza kuyalipa vipi.

Mhe. Spika, pia katika shirika au taasisi ambayo imeanzishwa *Zanzibar Multi* …

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, muda wako umekwisha.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, baada ya hayo nitakuja kuunga mkono baada ya kumaliza buti zangu, ahsante sana Mhe. Spika. *(Makofi).*

Mhe. Spika: Sasa Waheshimiwa Wajumbe, hoja hii inakusudiwa ifanyiwe majumuisho kesho asubuhi na tukiingia tu hiyo ndio kazi yetu, ili angalau kidogo tupunguze ule muda mrefu ambao ratiba yetu imeshatetereka mno kwa zaidi ya siku 7. Sasa muda uliobaki tukitumia dakika 15 mpaka saa 8:00 ni

wajumbe 6 tu ambao tunamudu kuwaita na wachangie na ningeomba basi ikawa hivyo ili angalau tufike wajumbe wapatao 20 kwa kuchangia.

Kwa hivyo, wajumbe ambao watakaopata nafasi ni pamoja na Mhe. Salma Mohamed Ali, Mhe. Mohammed Haji Khalid, Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa, Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi, Mhe. Panya Ali Abdalla na Mhe. Haji Faki Shaali (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum).

Hao ndio wajumbe 6 ambao watapata nafasi na niombe radhi sana kwa wale wengine ambao watakosa nafasi basi wanaweza kujiandaa kufanya matayarisho ya maandishi na kumpelekea Mhe. Waziri ili aondoke nayo akakae na watendaji wake kesho apate nafasi ya kutoa majibu. Tumkaribishe basi Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi na baadaye Mhe. Mohammed Haji Khalid, usizidi dakika 15.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante sana Mhe. Spika, mimi nadhani sitozifika dakika zako 15 pengine dakika 10 tu na sijui kama zitafika.

Mhe. Spika, kwanza nimpongeze Mhe. Waziri kwa kazi yake nzuri aliyoifanya hapa kwa kuwasilisha hotuba yake hii kwa ufupi sana. Lakini pia nimpongeze Mhe. Waziri pamoja na Naibu wake, kwa kazi wanazozifanya usiku na mchana hawalali ili kuiweka sawa wizara yao hii.

Mhe. Spika, baada ya hapo nije katika vitabu nianze na Kamisheni ya Utamaduni na Michezo. Nije katika kifungu cha 94 (iii), nitanukuu kidogo kifungu hicho kinasema kwamba:-

Kifungu cha 94 "(iii) Kuweka mkakati maalum wa kuimarisha na kuendeleza vikundi vya sanaa na utamaduni."

Mhe. Spika, nimpongeze Mhe. Waziri sana kuweka mikakati maalum na kuimarisha na kuendeleza vikundi hivi vya sanaa na utamaduni. Vikundi ambavyo Mhe. Waziri ameviwezesha. Vikundi hivi ameviwezesha kuvijengea uwezo.

Nimuulize Mhe. Waziri katika vikundi hivi ni vingapi ambavyo umeshaviajiri au tunavifanya vikundi hivi kwa kupokea wageni tu wanapoingia nchini?

Mhe. Spika, nije katika kifungu cha 94 (i),

Kifungu cha 94 "(i) Kuandaa mkakati maalumu wa kuibua vipaji vya sanaa na michezo maskulini kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu."

Niseme kwamba hili ni jambo zuri sana. Mhe. Waziri michezo maskulini ni kitu muhimu sana kwani vipaji vingi huanza maskulini, hata Wawakilishi, Mawaziri, Wabunge na wataalamu wengi wote wanaanzia huko. Mhe. Waziri hapa nikupongeze kwa kuweka mikakati mizuri sana katika maskuli yetu. Lakini pia mtawaondoshea uvivu, maradhi, watoto wetu kutokana na kukosa hata mazoezi maskulini, hili nalo pia Mhe. Waziri nikupongeze. Naiomba wizara itenge fungu maalum kwa wachezaji bora na wenye vipaji ili kupata wachezaji wazuri.

Pia nimuombe Mhe. Waziri azijengee uwezo timu zetu za Wilaya za madaraja ya pili na madaraja ya tatu. Timu hizi nyengine zinashindwa hata kupanda daraja kutokana na ukosefu wa fedha. Namuomba Mhe. Waziri hili aliangalie sana, alitilie mkazo na aziangalie kwa jicho la huruma timu zetu hizi ili ziweze kupanda daraja.

Mhe. Spika, hapa kidogo nilikuwa ni mnyonge zaidi kutokana na Naibu Waziri wa Habari, nilimwambia kwamba ninazo timu zangu ambazo zipo Kangani, Kukuu na Mjimbini. Timu hizo ni timu ya *Danger FFC* na Maendeleo iliyopo Mjimbini. Hizi nilimtaka Mhe. Naibu Waziri aje kuziona na kuzipa angalau motisha ili ziweze kuendelea. Timu hizi ni nzuri sana tu. Akaniahidi Mhe. Naibu Waziri wa Habari kwamba atakuja kuziona na vifaa tayari keshanitayarishia. Kwa hivyo Mhe. Naibu Waziri na Waziri ukisikia namuomba Mhe. Waziri utakapokuja anijibu.

Mhe. Waziri nije katika Idara ya Makumbusho ukurasa wa 44 kifungu cha 99 Mhe. Waziri hapa alisema,

Kifungu cha 99 "(i) Kupima na kuyapatia hati miliki maeneo ya kihistoria Unguja na Pemba.

(ii) Kuimarisha majengo ya kihistoria kwa kufanya tafiti, kukusanya taarifa zake na kufanya matengenezo."

Hapa nikuulize Mhe. Waziri hivi tangu mwaka 1964 hii nchi yetu ilivyopata uhuru hadi hii leo bado makumbusho hayana hatimiliki. Ndio kwanza idara inajipanga kuyatafutia hati miliki. Hii kweli hatuifanyii haki nchi yetu ya Zanzibar. Hivi kweli watu wetu watatuelewaje, kwamba hati miliki mpaka hii leo makumbusho haya hayajapatiwa. Ndio kwanza watu wanajipanga ili kutafuta hati miliki hizo. Naomba Mhe. Waziri utakapokuja unipe jibu.

Pia Mhe. Waziri isitoshe idara imejipanga kuanzisha makumbusho mengine mapya. Mhe. Waziri kwa kuwa makumbusho ni mambo ya kale na kwa kuwa makumbusho yanatokana na ukale. Je, haya makumbusho mapya

unayoyaanza yatakuwa makumbusho au nyumba za kukaa. Mhe. Waziri naomba jibu.

Vile vile nije katika Bodi ya Sensa na Filamu, ukurasa wa 48, hapa Mhe. Waziri katika kitabu chake kinasema kwamba,

Kifungu cha 110 "(i) Bodi imeendelea na mikakati ya ukaguzi wa filamu utakaowezesha kuiokoa jamii na wimbi la mmong'onyoko wa maadili pamoja na kutoa matangazo ya kuelimisha jamii juu ya kuenzi na kulinda maadili na kuelezea athari za madawa ya kulevya na elimu ya maadili kwa wageni."

Mhe. Spika, hapa nimpongeze Mhe. Waziri kwa kupambana na kuzifuatilia filamu zisizofaa kuonyeshwa hadharani. Nampongeza Mhe. Waziri sana pamoja na hilo kwa kuwa wizara ndio mas-uli ya tamasha la filamu, huoni kwamba Mhe. Waziri kuna mambo mengine yanahitaji kufanyiwa utafiti zaidi kwa vile hayaendani na mila na desturi zetu katika nchi yetu ya Zanzibar. Hususan wakati huo wa tamasha la filamu, Mhe. Waziri nakuomba ulifanyie utafiti zaidi katika hili tamasha linapokuwa hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, nije katika ukurasa wa 53, kuhusu kituo cha Afrika Mashariki na Kati. Hapa Mhe. Waziri kidogo nitanukuu tena katika kifungu cha 121 kinasema kwamba,

Kifungu cha 121 "Mhe. Spika, juhudi mbali mbali zilizochukuliwa za kuwasiliana na nchi wanachama wa chombo hicho lakini kwa muda wote huo hakuna hata nchi moja iliyokuwa ikijibu mawasiliano hayo. Kwa kuwa Tanzania imeteuliwa kuwa Makao Makuu ya Kamisheni ya Kiswahili ya Jumuia ya Afrika Mashariki, Serikali imeamua kubadilisha matumizi ya majengo yaliyokuwa yakitumiwa na *EACROTANAL* kuwa yawe Makao Makuu ya Kamisheni ya Kiswahili ya Jumuia hiyo."

Lakini Mhe. Spika, katika kifungu chake cha 119 ukurasa wa 52 kinasema katika mwaka wa fedha 2012/2013, kituo cha Afrika Mashariki na Kati ya utafiti wa simulizi asili na lugha za Afrika, *EACROTANAL* tumeidhinishiwa jumla ya shilingi 21 milioni kwa ajili ya kazi za kawaida mpaka 2013 tumefanikiwa kupata shilingi 18 milioni sawa na asilimia 86.

Hapa niseme kwa kuwa Mhe. Waziri kituo hichi ni maarufu sana. Watu wengi huja kujifunza lugha zetu za kiswahili na mambo mengine. Lakini hivi sasa kituo hichi kimepoteza muelekeo wake, hakuna hata mwanafunzi mmoja anayekuja hapa, hata wale wa kigeni kuja kujifunza lugha za kiswahili na simulizi asili. Je, Mhe. Waziri hebu tueleze kuna tatizo gani la kutokuja

wanafunzi hawa na pia kukosa mawasiliano kwa wanachama wa chombo hichi isipokuwa Tanzania peke yake. Naomba Mhe. Waziri anipe jibu.

Kubwa zaidi Mhe. Waziri katika kitabu chake kinaeleza kuwa kimeidhinishiwa shilingi milioni 21 kwa kazi za kawaida. Hadi Juni, 2013 chuo hicho kimefanikiwa kupata milioni 18 sawa na asilimia 86. Je, Mhe. Waziri kwa kuwa chombo hicho kimekosa kuungwa mkono na wanachama wake wote. Mhe. Waziri nieleze fedha hizo kwa wakati huu zinatumika vipi pale wakati chama hichi hakipo na kimekosa kuungwa mkono. Naomba Mhe. Waziri hapa ukija unipe muda.

Mhe. Spika, namalizia mwisho nije katika Baraza la Michezo kifungu cha 125(i). Hapa Mhe. Spika, Mhe. Waziri alisema kwamba,

Kifungu ch 125 "(i) Kuimarisha programu za vyama vya mchezo vya taifa.

Nimuulize Mhe. Waziri tangu kukaa uwaziri ni chama kipi ambacho kimetuletea sifa nchini kiasi kwamba tunajivunia kuwa chama fulani kimetuletea sifa au kimetuletea kombe au medali au nishani yoyote ambayo itatufanya tuwe katika kumbukumbu katika taifa letu.

Mhe. Spika, nakushukuru ahsante.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kupata fursa ya kutoa mawazo yangu machache juu ya Wizara hii ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uwezo wa kusimama hapa na kukupongeza wewe kwa dhati kwa kunipa nafasi ya kuzungumza. Nimpongeze Mhe. Waziri na watendaji wake kwa kutuletea bajeti hii ambayo tunaijadili.

Mhe. Spika, mawaziri wote baada ya kumaliza bajeti zao siku ya pili kwa kawaida huwa hawahudhurii. Hii ni kwa sababu moja tu, walikuwa na kazi ngumu na nzito siku iliyotangulia, ile nenda rudi, kaa simama inawachosha. Je, hawa watu ambao wapo mbele yetu waandishi hawa watatu wanasimama kila siku saa zote, kwa mawaziri wanakaa muda wa masaa mawili tu na wanachoka siku ya pili hawaji. Je, hawa tunawafikiria vipi?

Kipemba tunasema kusimama sana unafanya matende. Kwa hivyo hawa wasifanye matende ikawa matende yao hayana maana. Kama ni kweli wanapata posho ya shilingi elfu tano, Wizara inawaonea kweli kweli. Ningeomba isiwaonee kwa sababu kazi wanayoifanya ni ngumu, wengi wetu kusimama pale muda wote huo hatuwezi.

Mhe. Spika, nianze na mchango wangu katika Shirika la Utangazaji ambalo lina majukumu ya kutoa habari, kuelimisha, kuburudisha, kuhamasisha jamii juu ya masuala ya kiuchumi, kijamii na kisiasa. Hili ndio jambo la msingi jamii ijue mambo yote yanayotokea katika nchi. Shirika lina wajibu wa kufanya hayo majukumu waliyoyataja pamoja na kuwa sheria ya kuanzisha shirika ni ya juzi. Vyombo hivi vipo muda mrefu mno. Ukiacha mwanadamu taasisi ambazo mwanadamu anaziunda na kuziongoza kila miaka ilivyopita ndipo ufanisi unapoongezeka.

Nasikitika kuwa katika vyombo vyetu vya serikali vinaanza vizuri kila muda unapokwenda juu baada ya kuwa na kasi zaidi, vinarudi chini. Sijui tatizo huwa lipo wapi. Baada ya kukua jinsi muda unavyokwenda taasisi zetu zinarudi chini kama alivyo mwanadamu mwenyewe kila anavyokuwa anapungua nguvu. Mimi hapa kumfukuza Mhe. Issa Haji Ussi simpati atanikimbia na kama nikimkamata atakuwa kijana huyo ana matatizo ni mgonjwa. Lakini ilivyo yeye anifukuze tena muda mfupi anikamate.

Lakini ukija kwenye haya mashirika yetu Mhe. Spika, inashindwa na *Radio FM* imeanza juzi tu. Kwa nini? vyombo hivi zaidi *radio* ipo kabla wengi waliokuwemo humu hawajazaliwa, itakuwaje leo iwe duni kiasi hivi ilivyo, mpaka mimi niite *UBC* kwa sababu Pemba hatupati matangazo yetu na ukipata uitegeshe masikioni, kwa nini baada ya kwenda mbele tunarudi nyuma. Tatizo ni nini Mhe. Waziri? huwa vifaa, watu hawana uwezo au kuna nini. Mimi sipigi buti, wala sikuulizi hoja yoyote lakini katika kuunga mkono siungi mkono tu kwa sababu niunge mkono jambo ambalo tunalolizungumza lina ufanisi.

Mhe. Waziri ungejua kuwa vyombo vyako hivi badala ya kupata ufanisi vinadidimia. Kwa kweli si jambo zuri wala halipendezi kwa redio hizi zilizoanza juzi kuwa zipo juu, ni bora kuliko Shirika la Utangazaji ambalo ndio mdomo wa serikali. Serikali imepikuliwa na vyombo hivi. Nyinyi watendaji mmetoa macho tu, nafasi yetu inachukuliwa na vyombo binafsi. Maana yake hamna ushindani au mna ubia na vyombo hivi?

Mhe. Spika, niseme kuwa lugha ya baadhi ya watangazaji si nzuri kwa baadhi ya viongozi. Katika Kiingereza unapomtaja mtu na cheo chake kuna kitu kinaitwa *noun in a position*, huwezi ukasema Mohammed Haji Khalid, *member of the House of Representatives* au *Member of Representatives* Mohammed Haji Khalid bila ya kutia *Honourable* katika Kiingereza hiyo ipo. Lakini katika kiswahili utamaduni huo haupo kwa sababu ni Waswahili na tunazungumza Kiswahili, tuendeni katika utamaduni hasa wa Kiswahili katika kuwataja viongozi wetu na nafasi zao.

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo nataka niliseme ni Shirika la Magazeti. Majukumu yake tutizame ukurasa wa 24. Wanasema hivi:-

Kifungu cha 53 "(ii) Kukuza uwezo wa waandishi wa habari wa magazeti na wafanyakazi wa Shirika kwa kuwaendeleza kielimu ili kuwaongezea uwezo katika utendaji wao wa kazi na kuongeza ubora wa makala, habari na matukio. "

Hili ningemuomba Mhe. Waziri lisimaliziwe katika kitabu tu lazima hili Shirika la Magazeti ambalo ni la serikali waandishi wake huduma hii wapewe kweli kweli. Wawe na uwezo, ujuzi wa kuandika, elimu ya kazi yao ili wafanyakazi kulingana na taaluma yao.

Kipindi kilichopita nilionesha gazeti la serikali la Zanzibar Leo pengine mwandishi kwa kutoelewa au kutojua, kwa kutojifahamu kwa kutokufanya utafiti, kanita jina langu kamili vizuri Mhe. Mohammed Haji Khalid wa CCM, Mwakilishi wa Matemwe. Kwa kuwa mimi ni CUF na akanita CCM na akanipa jimbo la Matemwe. Imani yangu uchaguzi ujao Jimbo la Matemwe CUF tunalichukua. Lakini kwa kuwa kanita CCM na sio CCM na nilisema huyu mwandishi hana hatua yoyote aliyochukua ina maana hata ule utaratibu wa kuwa mtu anapokosea anaomba radhi hawajui. Inaonesha hawana elimu hata kidogo na wewe ndiye unayehusika. Mtu akikosea anaomba radhi, kuomba radhi sio kujidhalilisha.

Mhe. Spika, alikosea alisema alinipa ushindi mimi ambaye nilishindwa lakini ulimi uliteleza, wala u-Spika wake haukuondoka yupo pale pale na aliweka sawa tu kauli yake kwa sababu ni mwanadamu. Leo watu wako wewe nikwambie wana kibri labda wanaona kuomba radhi ni kujidhalilisha. Kuomba radhi si kujidhalilisha bali ni uungwana, alipokosea kakubali kujirekebisha.

Mhe. Spika, nije kidogo katika Baraza la Kiswahili kuhusu matumizi ya maneno ya Kiswahili. Sina hakika kuwa hili Baraza la Kiswahili kipi ambacho tunatumia kwa sababu hakuna elimu au taaluma inayotolewa. Hivi sasa kuna maneno ya ajabu ajabu yanatumika sivyo. Kwa mfano kama mimi nitasalimiana na mtu, hatimaye ananambia tutaonana baadaye. Maana hasa ya baadaye ina maana baada ya muda mfupi tu huyu mtu mtaonana tena. Lakini mtu anakwambia baadaye wakati huo anakuaga anakwenda zake Marekani. Hapa maana ya baadaye imepotoshwa kabisa.

Ukimwambia mtu wa umri wangu, kama utamwambia mama tutaonana baadaye basi akipika atakuwekea chakula, kwa sababu baadaye ina maana utarudi tena. Sasa sina hakika hili Baraza lako linachukua hatua gani ya

kuwafanya watu wakitumie Kiswahili vile kilivyo sasa. Leo kuna mambo, poa, *fresh*, hichi sio Kiswahili.

Kuna mara moja alipita muuza vikombe, mama mmoja akamwita na kununua, akamuuliza shilingi ngapi. Akamwambia shilingi tano. Mama akachagua vikombe vinne akaingia ndani, akenda akachukua shilingi ishirini akampa muuzaji vikombe. Yule muuza vikombe akashangaa akamwambia aah! mama hazitoshi hizi nimekwambia shilingi tano ina maana ni mia tano. Yeye kamwambia shilingi tano aliamini kwa maana ya shilingi tano hasa, kwa sababu ni Mswahili.

Mimi ukinambia nipe shilingi hamsini elfu kwa sababu unajua Kiswahili, kwa hivyo nitakupa hizo hizo ulizozitamka. Haya matatizo ya Kiswahili sina hakika ni kiasi gani Wizara yako imejiandaa kuyatumia na kuna maneno ambayo tunayafanya ya Kiswahili lakini sio ya Kiswahili. Ningekuomba Mhe. Waziri ufanye utafiti wa kina juu ya matumizi halisi ya Kiswahili.

Zamani Zanzibar Kiswahili sanifu kilikuwa kinasemwa hapa mjini Zanzibar, wengine wote tuna lahaja tu za Kiswahili, kuna Kipemba, Kitumbatu, Kimakundushi. Mhe. Spika, akitaka kusema anaweza akasokota lugha mimi nisiifahamu pale, akafahamu Mhe. Ismail Jussa na Mhe. Haroun Suleiman anaweza akasema lahaja ya kwao, mimi nikawa siifahamu. Mimi naweza nikakisema Kipemba hapa nyinyi msifahamu hiyo ni lahaja. Lakini kama ni lugha basi twende katika utaratibu wa lugha inavyotakiwa, sio mambo poa, *fresh*, hichi sio Kiswahili.

Mhe. Spika: Mheshimiwa malizia hoja yako.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Mhe. Spika, nije kwenye Baraza la Sanaa. Nianze kwa kumuuliza Mhe. Waziri nini maana ya utamaduni kwanza na ni upi hasa utamaduni wa Mzanzibari. Mhe. Spika, kuna utamaduni wa mambo mbali mbali wa mavazi, malezi na kadhalika. Sisi hasa utamaduni wetu ni upi, ni kucheza ngoma, mavazi yetu tuambiwe kwamba ya Kizanzibari mtu avae vipi. Kuna watu wanapokuwa barabarani tunawajua kwa vazi kwamba huyu ni Mmasai, Mnaigeria, huyu ni mtu wa wapi. Sisi tuvae vipi mpaka tuonekane kwamba hili ndio vazi la Kizanzibari. Sisi tucheze ngoma gani mpaka ionekane kwamba hii ndio ngoma ya Kizanzibari. Sisi tutembee vipi mpaka ujue huu ndio utembezi wa Kizanzibari.

Mhe. Spika: Mheshimiwa nakushukuru.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Ahsante.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Bismillahi Rahmani Rahim. Mhe. Spika, napenda kuchukua fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa kuweza kunipa fursa hii na mimi kuchangia. Lakini pia nimshukuru sahibu yangu, rafiki yangu Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo pamoja na watendaji wake kwa kazi nzuri ambayo wameifanya.

Lakini pamoja na yote hayo leo swahibu yangu nitakuomba kidogo sitokupa asilimia zote katika mchango huu wa bajeti yako hadi pale utakapoweza kunitosheleza kwa yale mambo ambayo nilikuwa naomba ufafanuzi wake.

Mhe. Spika, mimi nianze na bakaa ya mwaka jana. Mwana jana nilipokuwa nachangia hapa katika sekta ya utalii niliomba kupata taaluma jinsi gani hawa watembezaji wa watalii wanapoweza kupata hizi taaluma na namna gani wanaweza kutoa maelekezo kwa wale wageni ambao wanakuja katika nchi zetu. Wageni hao kwa sasa inaonekana taarifa wanazozipata nyengine zinakuwa sio sahihi na wanapata maelekezo ambayo yanapotosha historia na asili ya Zanzibar. Sasa sijui wizara Mhe. Waziri utapokakuja hapa utatuelekeza namna gani mmeweza kufanikiwa katika hili na hadi sasa tuko katika hatua gani.

Lakini vile vile niombe katika wizara yako Mhe. Waziri haya malipo ya ziada ya magari yaliyokwisha kupewa leseni wakatakiwa kwamba walipe leseni zile kwa mujibu wa taratibu tulizowekeana, lakini wanapakia watalii wanatakiwa malipo ya ziada sijui tumefikia wapi mpaka sasa kwa sababu naona bado malalamiko yangali yanaendelea. Kwa hivyo Mhe. Waziri utapokakuja hapa naomba utueleze hasa nini kinachoendelea katika suala hili.

Jengine Mhe. Waziri ni hili hili tatizo la watendaji ambao tunao humu ndani. Mhe. Waziri miaka yote ya nyuma tulikuwa tunazungumzia kuhusu suala la watendaji ambao tunao kutoka asubuhi mpaka tunaondoka, hebu leo tufahamishe hasa na utuambie na utupe mikakati gani mlioipanga katika wizara yako juu ya suala zima la hawa watendaji ambao wanakuwemo humu kutoka asubuhi na malipo yao pamoja na posho zao, tunaomba utupe ufafanuzi wa kina leo.

Baada ya hapo naomba kuondoka sasa kuja katika masuala yetu ya mila na tamaduni pamoja na mambo mengine. Mhe. Spika, nchi yoyote duniani inakuwa na utaratibu wa mila zake na tamaduni zake ambazo zinaenziwa. Katika nchi yetu ya Zanzibar tunazo mila zetu na tamaduni lakini kwa namna moja au nyengine kumekuwa na mporogonyoko wa maadili pamoja na mila zetu na tamaduni zetu na kuweza kufikia pahala hata ile michango na ushiriki wetu katika mambo mbali mbali iwe ya kimichezo, ya sanaa na utamaduni yanakuwa yanaporomoka siku hadi siku. Sasa Mhe. Waziri utakapokuja hapa

naomba utusaidie hasa kitu gani kinachosababisha hata baada ya sisi twende mbele tunakuwa tunarudi nyuma.

Tukichukulia mfano katika mwaka wa fedha 2012/2013 tulikuwa na mashindano ambayo yalishirikisha Wazanzibari katika namna kumi na sita, lakini mara hii tumekuja katika namna tisa. Sasa baada ya kwamba tunaongeza juhudi zetu sasa sisi tunakuwa tunashusha zile juhudi zetu. Tunakuomba Mhe. Waziri utakapokuja hapa utusaidie.

Lakini jengine linahusu Idara ya Haki miliki Mhe. Spikia, suala hili limepata wachangiaji wawili watatu kutaka kujua lile deni la shilingi milioni hamsini ambalo linadaiwa na taasisi ile kwa Wizara yake tunachomuomba Mhe. Waziri utakapokuja hapa mimi nitazuia kifungu cha mipango na sera kama sikupata maelekezo yatakayoweza kunitosheleza juu ya suala la deni hili likiwa sasa linachukua miaka 3 bado halijalipwa na hatua mbali mbali zimepita katika ngazi za uwaziri na utendaji, lakini bado suala hili halijapatiwa ufumbuzi na ukitilia maanani wanaotakiwa kulipwa fedha hizi ni vijana ambao hawana ajira, ajira zao ni haya mambo ya kuimba na mambo mengine mengine ili waweze kujiendesha kimaisha. Kwa hivyo Mhe. Waziri utakapokuja hapa, nitaomba unisaidie maelekezo katika hilo.

Jengine Mhe. Waziri utakapokuja hapa nitaomba vile vile leo utupatie au hiyo kesho utakapokuja utupatie mwelekeo ya wizara juu ya suala zima la Hoteli ya Bwawani. Katika kumbukumbu zetu katika utawala uliopita wa awamu ya sita uliokuwa ukiongozwa na Dr. Amaan Abeid Aman, Mhe. Karume alitoa maelekezo na hapa kinachoangaliwa yule alikuwa ni Rais kwa wakati ule na kauli ya Rais inatakiwa kuzingatiwa na kutekelezwa haraka inavyowezekana. Lakini hadi leo hii Mhe. Karume alipendekeza ile Hoteli ya Bwawani kifanywe ni Chuo lakini kile Chuo hakijafanywa wala hatujui nini kinachoendelea, yaani wale wanafunzi wanaosoma kutoka pale Maruhubi waende wakafanye *practice* zao katika hoteli ile. Hilo halikutekekezwa lakini kama hiyo haitoshi hata kile Chuo cha Utalii chenyewe ambacho kiko Maruhubi Mhe. Karume alielekeza pia kujengwe ile barabara ya ndani katika kiwango cha lami. Vile vile hilo halijatekelezwa hadi leo hii. Sasa Mhe. Waziri utakapokuja hapa tutaomba utusaidie hilo.

Jengine Mhe. Spika, nilikuwa nataka kuzungumzia kuhusu mashirika haya ya televisheni tofauti ambazo zipo hapo tunao *Zanzibar Cable*, *Star TV, DSTV,* naomba Mhe. Waziri atusaidie kuweza kuona kwamba kunatengenezwa mikataba maalum ili mashirika haya ambayo yana televisheni zake binafsi waweze kufanya mkataba na *ZBC* ili vipindi ambavyo vinatolewa na *ZBC* viweze kuoneshwa katika televisheni vile vile kwa sababu televisheni hizi

nyingi hazina matangazo ya *ZBC*. Tunataka utengenezwe utaratibu maalum kuhakikisha kwamba kitu hiki kinapatikana na televisheni vile vile.

Jengine ilikuwa naomba kupata maelezo juu ya sababu zipi zinazosababisha televisheni Zanzibar Pemba haionekani.

Baada ya maelekezo hayo Mhe. Spika, kwa heshima na taadhima kwa niaba yangu, wananchi wa Jimbo la Kikwajuni nitaunga mkono hoja ya bajeti hii kama nitajibiwa kama vile ambavyo natarajia. Kwa sasa hivi ninampa asilimia hamsini. Ahsante.

Mhe. Salma Mohammed Ali: Mhe. Spika, kwanza ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama. Pili ninakushukuru wewe kwa kunipa nafasi na vile vile naomba nimpongeze Mhe. Waziri kwa hotuba yake. Mhe. Spika, kwa kweli leo mimi sitokuwa na mchango mkubwa kwa hali yangu lakini nimeona sitowatendea haki wanawake wa Wilaya ya Chake Chake kuwa sikusimama katika Wizara hii kwa sababu kuna mambo yao ambayo wamenieleza ili nimwambie Mhe. Waziri na natanguliza kusema mwanzo Mhe. Spika, ikiwa waziri hatonipa jawabu ya kuwaridhisha wanawake wa Wilaya ya Chake Chake basi nitazuia fungu.

Mhe. Spika, naomba nianze mchango wangu, hali ya makumbusho ya mambo ya kale ni muhimu katika nchi na ni vyema wizara ikasimamia vizuri ili kuona historia ya nchi yetu haipotei. Mhe. Spika, maeneo mengi ya makumbusho Pemba hayaridhishi na sioni kama kuna umakini wa kutosha. Mhe. Spika, utakapoyatembelea utaona mengi yamo katika mwitu na hata ya kufyekwa basi hakuna matengenezo yanayofanyika.

Mhe. Spika, hapa naomba maelezo ya Mhe. Waziri imejipanga vipi kwa hili lakini katika kiambatanisho namba moja kifungu cha kumi na tisa kiko ukurasa wa 60 kinaelezea fedha zilizoingizwa kwa makumbusho Pemba. Mhe. Spika, fedha zilizoingizwa ni asilimia 24 tu naomba nipate maelezo kwa nini fedha iliyoingizwa ikawa ni kidogo kiasi hichi na pia Mhe. Spika, kumbe ndio maana makumbusho yote yakawa taabani. Ukienda Msikiti wa Chooko Tumbe makumbusho Mhe. Spika, yako hoi, taaban. Na ukenda katika makumbusho ya Pujini kwa kweli hayasemeki ni aibu hata kusema kama ni makumbusho.

Mhe. Spika, vile vile ukienda katika makumbusho ya Mkumbuu yametupw kabisa lakini haya hayawezi yakaimarika kutokana na fedha ndogo inayoingiziwa Idara ya Makunbusho kule Pemba. Mhe. Spika, vile vile naomba tulinganishe tuangalie ukurasa wa 59 kifungu 12 fedha iliyoingiziwa Idara ya Makumbusho Unguja ni asilimia 94. Hapa Mhe. Spika, naomba

maelezo kwa sababu mkurugenzi wa Idara hii ni mmoja iweje leo Pemba waingiziwe asilimia 24 na Unguja waingiziwe asilimia 94. Mhe. Spika, huu si ubaguzi wa dhahiri. Mimi sikubali na hapa ndipo waliponituma wanawake wa Wilaya ya Chake-Chake kwa kweli nitazuia fungu ikiwa Mhe. Waziri hatonambia ni nini sababu ya ubaguzi huu. Vile vile pia anieleze Pemba katika bajeti hii imepangiwa asilimia gani ya bajeti yote ya Idara ya Makumbusho.

Mhe. Spika, naomba niendelee na mchango wangu kwa matangazo ya televisheni ya *digital* katika maeneo mengi ya Chake Chake huwa inapatikana ingawaje sio safi kama hapa Unguja. Sasa ninamuomba Mhe. Waziri ninasikia yeye ni *engineer* basi asaidiane na wale mafundi walioko Pemba kuona kama na sisi Pemba tunapata matangazo haya vizuri atumie huo ujuzi wake.

Jambo jengine ambalo naomba nilizungumze hapa ni kuhusu ving'amuzi kwa kweli Mhe. Spika, wananchi wetu ni wanyonge mno wengi wanahitaji ving'amuzi lakini hawawezi kununua ving'amuzi kwa shilingi sabini na tatu elfu, si sabini tatu ile aliyosema Mhe. Kingunge. Ombi langu kwa Wizara Mhe. Spika, ifanye mambo matatu. Kwanza ikopeshe ving'amuzi kwa wafanyakazi na wananchi halafu iwakate kidogo kidogo. Pili ipunguze bei ya ving'amuzi angalau ifike shilingi thalathini na tatu iweke wiki ya *promotion* na ving'amuzi viuzwe kwa bei ya nafuu ili wananchi wengi waweze kuvinunua hivi, ikimaliza hiyo wiki Mhe. Spika, wataendelea na utaratibu itakuwa angalau kuna wananchi washafaidika kwa hilo.

Mhe. Spika, sasa nizungumzie kuhusu suala la utalii. Hivi karibuni Mhe. Spika, kulizunduliwa Kamati za Utalii za Wilaya. Hili ni jambo zuri katika kushirikisha jamii kuendeleza ile dhana ya utalii kwa wote. Lakini Mhe. Spika, hapa mimi nina ushauri kidogo kamati hizi zishirikishwe katika uanzishwaji wa vitega uchumi vya utalii katika Wilaya zao hili Mhe. Spika, litakapofanyika la kuwashirikisha hawa tokea mwanzo basi litasaidia kuepuka matatizo na mizozo inayoweza kutokea baadae.

Mhe. Spika, hivi sasa tumeshuhudia mara nyingi kwenye maeneo haya ya vitega uchumi utasikia kuna mizozo ya ardhi. Sasa ikiwa kamati za Wilaya zitashirikishwa ninafikiria hii itasaidia.

Jengine Mhe. Spika, nitakalozungumzia ni katika sekta hiyo hiyo ya utalii. Kodi ambazo wanatoleshwa mahoteli ya nyota moja Pemba na Unguja. Mhe. Spika, hili nilipokuwa nikichangia hotuba kuu ya serikali nilisema, iweje hoteli ya nyota moja iliyopo Chake Chake yenye vyumba 40 ambayo hupokea wageni 200 kwa mwezi itoleshwe kodi sawa sawa na hoteli ya nyota moja

yenye vyumba 40 iliyoko Nungwi ambayo kwa mwezi ina uwezo wa kupokea wageni 2000. Mhe. Spika, hili kweli ni haki na namuomba Mhe. Waziri anambie hii kufanya hivi si kudamaza shughuli za utalii kule Pemba.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo naomba nilizungumzie naomba hapa nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mhe. Waziri kwa jitihada ya kuimarisha shughuli za michezo. Mhe. Spika, kwanza nampongeza kwa kutafuta msaada wa mipira 20,000 na kuigawa bure kwa wanamichezo. Hii Mhe. Spika, imesaidia sana vijana na wachezaji wa mpira wa miguu na mikono kupata mipira. Lakini vile vile namshauri aangalie uwezekano wa kupata vifaa vya michezo mengine, ipo michezo mengine pia Mhe. Spika, inahitaji vifaa. Kwa hivyo Mhe. Waziri awaangalie na hawa. Pongezi zangu zaidi ni kutokana na taarifa yake ya kuanzisha jengo la kisasa la mchezo wa Judo na michezo mengine katika eneo la Uwanja wa Gombani. Mhe. Spika, kwa kweli kumalizika mradi huu ambao Mhe. Waziri amesema utagharimu milioni mia tano ni mafanikio makubwa kwa wana michezo wa kisiwa cha Pemba.

Mhe. Spika, naomba nitumie nafasi hii kwa niaba ya wana michezo wa Pemba kumpongeza Mhe. Waziri na kumshukuru kwa hilo.

Mhe. Spika, nadhani baada ya mchango huo kwa kuwa muda hautoshi nimwambie tu Mhe. Waziri kuwa lile suala walilolizungumzia wanawake wa Chake Chake kuhusu makumbusho kule Pemba hatonijibu na wanawake wale wakaridhika kwa kutupwa makumbusho yaliyoko Pemba, basi nitazuia fungu la Idara ya Makumbusho.

Mhe. Spika ninakushukuru.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Spika, ninashukuru na mimi kunipatia fursa hii nizungumze machache katika kuchangia hotuba ya Mhe. Waziri wa habari. Mhe. Spika, nianze na mimi kumshukuru Mhe. Waziri na kumpongeza sana kwa kazi nzuri anayoifanya yeye na watendaji wake wote na nawatakia kila la kheri ili waendelee vizuri na kazi yao hiyo.

Mhe. Spika, mimi nianze katika Idara ya Utumishi na nianze kwa kuzungumzia maslahi ya wafanyakazi. Mhe. Spika, wenzangu wengi hapa wamezungumzia lakini naomba na mimi nikazie juu ya hilo. Mhe. Spika, wafanyakazi hawa wa habari wanafanya kazi katika mazingira magumu hakuna asiyeelewa kama wafanyakazi hawa kuwa saa nyengine huwa wanahatarisha maisha yao, wanafukuzwa saa nyengine katika kufuatilia habari zao. Lakini tukija katika maslahi au maposho yanakuwa madogo. Mheshimiwa na mimi niungane na wale wenzangu ambao wamesema wafanyakazi hawa wa habari ambao tunao katika Baraza hili basi

waongezewe wawe na posho maalum, kwa sababu kwanza tuangalie kufika kwao hapa tu wanafika mapema zaidi kuliko ya watu wote. Lakini pili wanasimama muda mrefu, tatu wanaangalia kioo kwa muda mwingi lakini nne mashine zile wanazoweka katika masikio hivyo vitu vyote vina athari katika mwili ya mwanaadamu. Hivyo ni lazima kuwe na posho maalum ambalo litaweza kutoa huduma pia ya afya zao.

Mhe. Spika, niseme kwa wafanyakazi hawa lazima tuweze kuwajali wafanyakazi wote hakika katika Wizara hii wako katika mazingira magumu kwa sababu pia wanashindwa kufanya kazi zao vizuri vitendea kazi hawana. Mimi niombe sana serikali wajue kama Wizara hii ndio ambayo ni kioo cha jamii ambacho habari zote tunazipata pale tunapata kujua mambo yetu mbali mbali kupitia Wizara hii. Kwa hivyo ni Wizara muhimu ni vizuri na hasa tumetoka katika mfumo wa *analogue* kuingia *digital,* hivyo ni lazima na vile vifaa navyo pia vitoke katika *analogue* viingie *digital*. Hatuwezi kuwa na mfumo ule wa *digital* lakini vifaa bado tunavyo vile vile vya *analogue,* hivyo hatuwezi tukaenda.

Mhe. pia nichukue fursa hii kuwapongeza sana wafanyakazi wa habari na niwaombe wenzangu kwa kweli wawapongeze sana hawa wanafanya kazi ngumu, wanastahili sifa ya kupongezwa na kila mtu. Mhe. Spika, lakini nije na masikitiko kidogo katika wafanyakazi. Mheshimiwa mimi najua hata katika Wizara nyengine tunaona mfanyakazi anapofanya kazi kwa bidii akawa anakidhi yale mahitaji ambayo yanafanyika, mimi huona hupewa tunzo au hupata *promotion* pengine ya kupandishwa hata cheo. Lakini hapa ninasikitika kuna kijana huyu ambaye tunamjua Juma Mmanga au Mheshimiwa Waziri utwambie kama kuna tatizo la kijana huyu tuweze kulijua. Mimi nilikuwa najua kazi yake anaiwakilisha vizuri na tulikuwa tunafaidika sana kwa kipindi chake cha magazeti. Lakini hatuelewi kwa nini hatumsikii Juma Mmanga hewani yuko wapi au anafanya nini au kama amepelekwa masomoni pia tunataka tuelewe au kama labda ameondoka pale kwa kupandishwa cheo zaidi tujue. Lakini vyenginevyo huwa tunawapoteza watu wenye sifa na kipaji ambao wanaweza kufanya kazi vizuri baadae ndio tunapokosa hapa wataalamu. Naomba sana Mhe. Waziri nipate jawabu juu ya mfanyakazi huyu.

Mhe. Spika, niende katika ukurasa 46 ambapo kuna Baraza la Kiswahili. Mimi niseme tujipongeze kwamba sisi Wazanzibari ambao hii ndio lugha yetu kuu na ni lugha ya taifa, kwa kweli Kiswahili fasaha, laini, chenye kufahamika, chenye kupendeza kinapatikana Zanzibar. Lakini bado ninahisi hatujakipa hadhi sisi wenyewe hiki kiswahili ili kikaweza kweli kikawa ni lugha ambayo itaweza kuleta manufaa kwetu na kwa taifa letu. Mimi niseme Kiswahili kwanza tungekitumia vizuri tungeweza kupata ajira za nchi za nje

kutoa walimu hawa wa Kiswahili tukenda tukafundisha kule. Kwa hivyo tungeweza hapa kuongeza ajira.

Lakini pia Kiswahili hichi tungeweza kukitumia kama wanavyotumia wenzetu wageni wanapokuja katika nchi zetu wanatumia lugha zao na tukawa tunatafsiriwa na wakalimani. Sisi Kiswahili hiki tungelitafisiri tukenda nchi za nje basi tusikitie mikobani maana yake tukiseme Kiswahili na sisi tuwe na wakalimani waweze kutafsiriwa wale wenzetu ili Kiswahili hiki kisibaki kudumaa tu hapa ikawa tunasema hakikui lakini kumbe tungelikikuza sisi wenyewe na sisi tungekipa hadhi tukakitumia na kingetafsiriwa kule kingepata hadhi fulani na sisi tungejivunia kweli lugha yetu.

Mhe. Spika, niende katika mila na utamaduni. Kwa kweli mimi naendelea kusema mila na utamaduni wa Mzanzibari unaendelea kutoweka siku hadi siku na hatimae tutakuja kuambukia hapa tumetawaliwa na mila za kigeni. Mhe. Spika, mimi nimuombe sana Mhe. Waziri kuziendeleza hizi mila na utamaduni na silka zetu ambazo tumezizoea Wazanzibari, basi tungeweza kuangalia katika serikali zile sheria hasa ambazo zitalinda hii mila na utamaduni wetu ili tuweza kuzitumia utamaduni huu uweze kubakia, vyenginevyo tutakuwa maskini kwa sababu nini tutawarithisha watoto wetu na wajukuu wetu, watakuja kukuta mila ambazo zipo. Naomba Mheshimiwa hili tuangalie sheria zetu zinasemaje na kama zina mapungufu basi tuweze kuzirekebisha ili utamaduni na mila zetu ziendelee kuwepo.

Mhe. Spika, niende katika sekta ya habari. Kwa kweli katika sekta hii ya habari mmetueleza katika kitabu kazi yenu moja kubwa ni kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora za habari na kwa wakati kwa njia ya magazeti, redio na televisheni. Hili ni hakika lakini Mheshimiwa, mimi niseme sisi wengine hata tuangalie TV gani lakini tunaridhika kuangalia yetu ya *ZBC* tunapenda kusikiliza redio yetu ya *ZBC*, hata tuangalie huko kwengine hata tusikilize lakini hivi vitu vina mvuto kwetu kwa sababu ndio vya kwetu. Lazima mtu athamini chake ndipo akisha akithamini cha mwenzake. Kwa hivyo Mheshimiwa tunachosikitika katika *ZBC* bado hakuna vipindi vya mvuto ambavyo vinambakisha Mzanzibari aiangalie TV yake au asikilize redio yake. Tunaomba sana Mheshimiwa, watu wajitume kutafuta vipindi ili tuone tuna vipindi vya uhakika kwa sababu kuna TV au redio zimeanzishwa hivi karibuni lakini wanahangaika kutafuta. Sisi kwa nini tudumae na tunapodumaa ndio tunaidumaza hii taasisi. Mimi naomba sana lazima tuhangaike wenzetu wa *TBC* wale kuna vipindi tele ninaviangalia wanakuja kufuata huku kwetu, kwa nini sisi tukae tusitoke nje kutafuta vipindi ili tukaja tukaleta vipindi, tunaleta vipindi hata havina maana yoyote.

Mimi naomba sana Mheshimiwa lazima na sisi tutafute vipindi ambavyo vitaweza kuleta mvuto. Utakuta kipindi kile cha ufunguzi asubuhi tuna Kur-an tukufu pale kila siku tuna *suratil bakra*, hatujamfika huyo *bakra* wenyewe tukajua *malau nuha*, tuko hapa kwenye *mabaudhata* tu yaani tunamjadili mbu hatufiki kwenye ng'ombe wenyewe tukajua yuko rangi gani. Mheshimiwa naomba sana sisi kwa hapa Zanzibar hatuna upungufu wa watu hawa, Mashekhe tunao wengi kwa nini tusiwe tunapata mbadala. Hivi sisi tunapoangalia hizi TV tunaangalia kwa kujifunza mengi, tunapata darsa pale pale. Kwa hivyo unategemea leo umeshapata kipande kile labda siku nyengine pataendelea pengine. Lakini pana mabaudhata, hapaongezeki pahala. Mheshimiwa tunaomba sana vipindi hivi viendelee ili vitupe elimu sisi wananchi ambao tunaviangalia.

Mheshimiwa niende katika Baraza hili la Sanaa. Baraza la Sanaa kwa kweli katika maelezo yake hapa linasema kufanya utafiti wa sanaa zilizopotea na kutayarisha takwimu za sanaa Unguja na Pemba na kuzihifadhi. Mimi nakwenda sambamba na hili lakini bado naona sanaa mnazitupa, tuna wasanii ambao wame-*act* sanaa nzuri nzuri na zinavutia mpaka leo zikioneshwa katika televisheni lakini hatuzioni, sijui ndio hivyo zishapotea tunaomba kama hizo zipo tuoneshwe. Wasanii akina Mashaka wamefanya kazi kubwa sana tena michezo yao inakwenda na wakati mpaka leo ikiangaliwa kwa sababu walikuwa wana-*act* kufuata mila na utamaduni wa nchi yao. Mheshimiwa mimi naomba sana lakini pia niombe kuziangalia sanaa hizo kabla ya kwenda kuoneshwa katika jamii basi zionekane sanaa hizo zinakwenda kweli na silka, mila na utamaduni wa Mzanzibari ili tusiweze kupoteza maadili yetu. Mheshimiwa katika nyimbo zetu katika utamaduni wetu wa nyimbo na mambo mengine pia niombe basi hili Baraza liwe kweli linaangalia mila na utamaduni wetu haupotei katika vitu hivi.

Mheshimiwa mimi nilitaka kusema hayo machache lakini namuomba sana Mhe. Waziri suala la ndugu yetu yule Juma Mmanga ambaye sasa tunakosa habari zake katika magazeti, naomba sana utakapokuja hapa utueleze ni kwa sababu gani na yuko wapi.

Baada ya kusema hayo naunga mkono bajeti hii kwa asilimia 100. Ahsante sana.

Mhe. Nassor Salim Ali: Ahsante Mhe. Spika, na mimi kuniangalia kwa jicho la huruma wana michezo nasema mwanamichezo nambari mbili angalau kunipa dakika 5 Mheshimiwa ninashukuru sana, sababu mimi mwana michezo nilianzia kucheza mchezo wa mpira wa miguu nikiwa katika Skuli ya Kengeja na timu yangu ilikuwa na timu ya Nyundo Sports Club ya Kengeja ni mchezaji mahiri sana.

Mheshimiwa kwa vile dakika ni kidogo, nianze katika sekta hii habari. Kuna msemo unasema mnyonge mnyongeni lakini haki yake mpeni. Mheshimiwa tumezungumza sana kuhusu Shirika hili la Utangazaji (*ZBC),* lakini mimi nadhani sio haja au haina maana kuweza kumlaumu kumtupia lawama Mkurugenzi yule lakini tukiangalia au tukijua kwamba hali halisi ya shirika lile ni mbaya. Mheshimiwa *ZBC* wamekuwa wakitengewa takriban milioni 33 kwa mwaka kwa ajili ya kuendesha vipindi na vipindi ambavyo Wazanzibari au Watanzania kwa ujumla walikuwa wakivipenda sana hususan masuala ya mpira wa miguu au zile mechi ambazo zinachezwa za *World Cup* na mashindano mengine ambapo zinahitajika kama *Euro* milioni sitini ili kuweza kuendesha mashindano yale. Sasa nadhani ipo haja kuiambia Serikali kuhakikisha kwamba tunatoa fungu kubwa kuweza kuboresha shirika lile ili tuweze kwenda na wakati tulionao huu wa habari. Lakini si vyema tu kuanza kutoa lawama au kumlenga Mkurugenzi huyu wa Shirika hili la *ZBC*. Mhe. Spika, *TBC* lilianzishwa shirika hili na ilipewa nyenzo, kwa hivyo ipo haja shirika letu hili la *ZBC* kupewa nyenzo sio kutoa lawama, baada ya kupewa nyenzo na kama utendaji utakuwa haupo basi tutaangalia nani wa kuweza kumlaumu.

Mhe. Spika, sasa nije katika sekta hii ya michezo. Kwa vile muda ni mdogo na nimeomba hili kwa sababu nilizungumze ilikuwa shuhuda mimi ikiongozwa na wewe Mhe. Spika, na Mawaziri na Waheshimiwa wengine Mhe. Mtando, Mhe. Gavu na wengine ambao tulikwenda kule nchini Ghana nakushukuru sana Mhe. Spika kwa kunipeleka Ghana kwa kuweza kuona mambo ambayo leo tunaweza kuyasemea haya.

Mhe. Spika, viwanja vyetu vya mpira wa miguu, tulikuwa tukitoa lawama tukipiga makelele, kiwanja cha Amani kibovu, viwanja vyengine vibovu lakini tatizo ni utumiaji wa viwanja vile, tulikuwa tukitumia viwanja vile kwa shughuli nyengine ambazo zinaharibu viwanja vile.

Mhe. Spika, kule Ghana tulipokwenda katika ziara yetu tuliona sherehe za uhuru wa Ghana na kile kiwanja ambacho kinatumika kwa ajili ya sherehe wewe ulikuwa shuhuda, kimejengwa nje ya kiwanja kile cha mpira wa miguu cha kitaifa pale Ghana, kiwanja kizuri na kimejengwa kwa ajili ya sherehe tu za kitaifa na nakumbuka katika ahadi ya Mhe. Rais ya kujenga kiwanja cha kisasa ambacho kitakuwa kinatumika kwa shughuli zetu za sherehe za kitaifa. Sasa sijui kwamba ahadi ile na utekelezaji wake umefikia wapi. Kwa hivyo ni vyema Mhe. Waziri atakapokuja atupe maelezo ya kina kuhusiana na suala hili la kujenga kiwanja cha kisasa ambacho kitatumika kwa ajili ya sherehe zetu za kitaifa ili kuondoa viwanja vyetu hivi tulivyonavyo vya Amani,

Gombani na vyengine kuviondolea mzigo katika masuala mengine ambayo yanatumika kwa kuharibu viwanja vyetu hivi vya michezo.

Mhe. Spika, kuhusu ushirikiano kati ya *TFF* na *ZFA*. Kumekuwa na tatizo kubwa, kuna mradi ambao unaitwa *FIFA Goal Project.* Mradi huu ni mradi ambao takriban miaka minne sasa, mara ile umeshatolewa mradi huo wa *FIFA* ambao ni kujenga katika viwanja mbali mbali katika kuinua hali ya michezo ulimwengu mzima na sisi Tanzania tumebahatika kupata mradi huu mara nne. Lakini cha kusikitisha ni kwamba sisi tumebahatika kupata mradi mmoja tu ambao ni kujenga kiwanja cha Gombani kule Pemba, wenzetu *TFF* wameweza kujenga ofisi pale Karume, wamejenga uwanja wa kisasa wa nyasi bandia pale Karume, wamejenga uwanja wa kisasa ambao ndio huu wa tatu ambao unajengwa kule Mwanza.

Mhe. Spika, mradi huu unalenga kwa Tanzania, Zanzibar tukiwa kama sehemu moja ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni haki yetu kupata miradi hii, kwa sababu sisi Zanzibar si wanachama wa *FIFA*, Tanzania ndio wanachama wa *FIFA* ikiwa kama Watanzania ni haki yetu kupata miradi ile ili kuendeleza soka letu la Zanzibar na Tanzania kwa ujumla. Kwa hivyo ipo haja ningemuomba Mhe. Waziri, hili anipe maelezo ya kina imefikia wapi katika kufuatilia yeye pamoja na Waziri ambaye anashughulikia masuala ya michezo wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Mabaraza haya ya michezo Zanzibar pamoja Tanzania *TFF* na *ZFA* ili kuwaelimisha na kuwafahamisha masuala haya ya mradi huu wa *FIFA Goal Project*. *FIFA* ilikuwa ikitoa miradi hii ya maendeleo ya soka ulimwenguni na sisi ni wajibu wetu kuyasemea kuhakikisha kwamba tunafaidika na miradi hii

Mhe. Spika, pia nichukue pia fursa ya kumpongeza sana kabisa Mwenyekiti wa Baraza la Michezo la Zanzibar Bi. Sherry, kwa juhudi zake ambazo amezichukua za kuweza kupata mipira takriban elfu ishirini ambayo imesambazwa Zanzibar nzima, skulini, timu zote za Zanzibar, mipira hii imefika mpaka Gando, Wawi, Kengeja, Mtambile, Muyuni pia imefika, haya yote yametokana na juhudi kubwa za bibi huyu pamoja na wasaidizi wake. Lakini ni vyema kwa kushirikiana sote pamoja ili kuunga juhudi hizi na Waziri kuhakikisha kwamba unatoa ushirikiano mkubwa katika kuendeleza soka letu la Zanzibar kwa kumpa ushirikiano mama huyu.

Mhe. Spika, kwa vile maelezo mengi nimeyaandika katika taarifa yangu au maelezo yangu kwa maandishi na wewe umenipa dakika tano na tayari nimeshawacha *microphone* nichukue fursa hii kukushukuru sana kabisa ingawa nilikuwa na mengi, lakini nimeshayaandika tayari ninayo. Kwa hivyo atakapokuja Mhe. Waziri anijibu haya ambayo nimeyaandika kwa maandishi

ili niweze kumpitishia bajeti hii ingawa napitisha kwa asilimia 90 kwa sababu haya yapo katika maandishi hizi kumi naziacha baada ya kupata majibu yako.

Baada ya kusema hayo Mhe. Spika, nakushukuru sana.

Mhe. Haji Faki Shaali (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum): Mhe. Spika, kwanza nakushukuru sana kwa kunipatia fursa na mimi kuchangia machache sana katika hotuba hii. Kwanza naunga mkono hoja kwa asilimia zote mia na zaidi ya hapo ninampongeza Mhe. Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Wakurugenzi na wafanyakazi wote wa Wizara hii kuanzia wakubwa mpaka wale wafagiaji maofisini wote nawapa pongezi. Najua kwamba wana kazi kubwa na ngumu kutokana na ufinyu wa bajeti na changamoto nyingi lakini lazima tuwape pongezi za dhati kabisa.

Mhe. Spika, baada ya kuunga mkono hoja na kupongeza, mimi ninataka nichangie kidogo katika Hoteli ya Bwawani. Waheshimiwa wenzangu waliotangulia kutoa maoni yao kila mmoja katoa kama vile anavyohisi yeye inafaa kuhusu kuimarisha Hoteli ya Bwawani na mimi ninataka nizungumze vile ninavyohisi inafaa katika kuimarisha Hoteli ya Bwawani.

Mhe. Spika, mimi tatizo ninaloliona binafsi kwamba taasisi nyingi za serikali tunaitelekeza hii Hoteli ya Bwawani pamoja na Baraza letu la Wawakilishi. Kwa mfano Mhe. Spika, juzi tu tulikuwa na futari katika hoteli moja sitaki niitaje jina kuharibu biashara, lakini mara nyingi tukifanya masemina yetu, makongamano, warsha au tunapoandaa *lunch* kwa shughuli fulani tunasahau kama kuna hoteli ya serikali inayoitwa Hoteli ya Bwawani na hii hoteli ndio inayotufaa katika shughuli zetu nyingi.

Mhe. Spika, mimi ninataka nitoe wito nimuombe Mhe. Waziri, kwanza naliomba Baraza la Tukufu kuanzia sasa tukiwa na semina, makongamano jambo lolote lile hebu tupelekeni kule Bwawani tuisaidie hoteli, lakini ikiwa serikali yenyewe inakwenda katika mahoteli ya watu binafsi. Tena jambo la kushangaza kama mwaka jana tulikwenda hoteli moja ya kitalii tukalishwa uporo, mimi nilipoondoka pale tumbo likaniuma, uporo wa mwezi mzima lakini Bwanani pale chakula kizuri, kitamu, kina ladha lakini haturidhiki mpaka tukapige maporo katika mahoteli mengine. Mimi nashauri sana Mhe. Spika, kwamba serikali ioneshe moyo wa kufanya shughuli zetu na tuthamini chetu katika ile Hoteli ya Bwawani ili wale waongeze mapato na kujinyanyua zaidi. Najua kuna siku tutahitaji kupumzika shamba kulala, hilo mimi sina tatizo lakini katika shughuli zile hata hatulali tuko hapa hapa mjini, basi kama hizo ambazo hatulali mashamba tupo hapa hapa mjini mimi naomba tubadilishe *minds* zetu twendeni katika Hoteli ya Bwawani Mhe. Spika, ili

tuisaidie hii hoteli iweze kujiendesha kibiashara na kuongeza mapato yao. Hilo ni suala la kwanza.

Mhe. Spika, la pili nije katika suala la *ZBC* ambalo nalo limechangiwa sana na Wajumbe wengi. Mimi nina ombi vile vile kwa Baraza lako tukufu la Wawakilishi. Mhe. Spika, naomba kiti chako na ofisi yako kwamba katika bajeti ijayo ya mwaka 2014/15 kwa kushauriana na Wizara husika inayosimamia Baraza la Wawakilishi, hebu tufanyeni utaratibu tuombe fungu la kusaidia alau kugharamia haya matangazo ya Baraza la Wawakilishi. Wenzetu Bunge la Jamhuri ya Muungano huwa linalipia matangazo haya yanayooneshwa moja kwa moja wananchi wakafaidika.

Nafikiri ikiwa *ZBC* tutaendelea kuitumia bure bila ya kuisaidia haitakuja juu na ile azma ya Wajumbe wako wanaopiga kelele kuhusu *ZBC* iimarike, kwa hilo haiwezi kuimarika kwa sababu angalia Mhe. Spika, kuanzia saa 3.00 za asubuhi mpaka saa 7.00 mchana na kwa huu mwezi wa Ramadhani mpaka saa 8.00 mchana wanarusha matangazo hewani, kurusha matangazo hewani kuna gharama kubwa. Sasa mimi nashauri kabisa kupitia Baraza la Wawakilishi hebu kuanzia mwakani bajeti ya 2014/15 na sisi tuweke fungu maalumu la kulipia matangazo haya ili tuwasaidie hawa *ZBC* waweze kurusha matangazo vizuri zaidi na wananchi wakatuona vizuri zaidi na tukasikika vizuri zaidi, na vile vile hata ile lawama itapungua kama ikiwa Baraza itajitolea muhanga ikasema aah! kuanzia mara hii hebu tuwekeni kama fungu la milioni mia tano au mia sita kwa ajili ya kurushia hewani matangazo yetu kama inavyofanya Bunge la Muungano, nadhani tutaweza kuisaidia *ZBC* kufanya kazi vizuri.

Mhe. Spika, nategemea vile vile tukifanya hilo hata zile hoja za Wajumbe kama Baraza litafanya hivi nafikiri tutaweza kumsaidia Mhe. Waziri, nafikiri ataweza kulipa shilingi 50,000/= badala ya shs.5,000/=, lakini kwa sasa hivi ukimwambia Waziri alipe shs.50,000/= wakati sisi hapa tunarusha bure hatulipi hata senti tano atazipata wapi pesa. Sasa mimi nafikiri Mhe. Spika, Baraza tuna mchango mkubwa wa kumsaidia Mhe. Waziri ili kuiendesha hii *ZBC*. Vile vile kuna kilio hichi cha kutafuta watangazaji wazuri nafikiri vile vile Mhe. Waziri ataweza kusaidia hili na kuwaendeleza zaidi kimasomo na kiufundi ili *ZBC* iende kileo.

Mhe. Spika, kweli mimi nakubali kwamba *ZBC* haiendi kileo. Jana nilikuwa naangalia mjadala wa demokrasia kuelekea 2015 katika *television* ya *Star TV*. Mhe. Spika, utaona kwa kweli hizi tofauti ziliopo ni kubwa mno. Mtangazaji yuko Mwanza kwenye hiyo *station* kubwa na mmoja yupo Dar es Salaam, kuna wachangiaji wengine wanaeleza kwa *satellite* pale unaona mijadala inavyokwenda vizuri kabisa. Sasa na hapa *ZBC* basi tunaweza tukenda huko lakini vile vile mimi nina ombi kwamba Baraza tuisaidie. Halafu vile vile na

coverage yao nafikiri vile vile na wao wenyewe wazidi kuifanya iwe kubwa wafike mbali zaidi ili ipate watazamaji wengi. Nafikiri vile vile Mhe. Waziri ataliangalia hilo.

Mhe. Spika, jengine ambalo ninataka nilizungumze ni kuhusu suala la kiswahili. Mhe. Waziri hapa kazungumza uzuri na akaeleza azma ya kushajihisha waandishi wa kiswahili. Mhe. Spika, hili suala naona linahitaji umakini wa hali ya juu, hili suala Mhe. Waziri wa Habari kwa kushirikiana na Waziri wa Elimu, mimi nafikiri angelikaa kitako hasa wakaliangalia mkakati mzuri. Kwa nini Mhe. Spika, nikasema hivyo ni kwamba kuna dalili huko tunakokwenda Zanzibar itakuwa na Baraza lake la Mitihani la Zanzibar ambalo litakuwa linatunga mitihani yake yenyewe kwa kutumia mitaala yake yenyewe. Lakini sasa Mhe. Spika, ikiwa tunaanzisha kwa mfano Baraza la Mitihani la Zanzibar, mitihani ya Kiswahili tunafanya sisi hapa hapa Zanzibar, lakini tunakwenda kutumia vitabu vya Kiswahili vilivyotungwa Tanzania Bara, itakuwa tumekataa nini tunafanya nini.

Sasa nafikiri Mhe. Spika, wakati tunajiandaa kuelekea kuwa na Baraza la Zanzibar basi mimi nafikiri ni vyema wizara mbili hizi zikashirikiane; Wizara ya Elimu na Wizara ya Habari ikawa na mkakati hasa wa kushajihisha waandishi wa vitabu vya kiswahili, vitabu vya riwaya, vitabu vya tamthiliya, vitabu vya mashairi na vinginevyo ili kwamba hapo tutapokuja kuwa na Baraza la Mitihani la Zanzibar basi alau tuwe na vitabu vile vya Kiswahili vyetu sisi wenyewe, kuanzia *O Level* mpaka *A Level* tuwe na vitabu vyetu sisi wenyewe. Lakini Mhe. Spika, kama unamtahini mtu kwa kiswahili lakini vitabu vya tamthilia vyote Bara, vya riwaya vyote Bara, vya ushairi vyote Bara, sasa nafikiri itakuwa hatujajiandaa vizuri. Namuomba sana Mhe. Waziri kwa hili walisimamie kwa nguvu zao zote ili vitabu vya kiswahili virudi kama zamani.

Mhe. Spika, hapa nilikuwa nakumbuka kulikuwa na vitabu vingi hapa kama vya Bwana Msa, vitabu vingi katika mitihani ya Tanzania basi kulikuwa na vitabu vya Bwana Msa na waandishi wa Zanzibar kama Said Mohammed na kadhalika na kadhalika. Bara zamani kulikuwa hakuna waandishi wengi wa vitabu vya Kiswahili lakini leo Mhe. Spika, utakuta vitabu vingi hasa vya tamthilia na vya riwaya na vya ushairi ukiacha vya Seif Khatib hakuna Mzanzibari mwengine, vyote utakuta vitabu vinatoka upande wa Tanzania Bara wakati Zanzibar ndio kwenye kitovu cha lugha ya kiswahili. Sasa hili mimi nalizungumza sana kwa sababu naliona kwangu muhimu kwa mustakbali wa maendeleo ya lugha ya Kiswahili na tusipofanya hivyo basi maandalizi yetu ya kuunda Baraza la Mitihani itakuwa mtihani mkubwa.

Mhe. Spika, vile vile hichi kiswahili ambapo hapa panahitaji mashirikiano yako Mhe. Waziri na ya Mhe. Waziri wa Elimu, kwa sababu Taasisi ya Kiswahili ambapo sasa hivi ni sehemu ya Chuo Kikuu iko Wizara ya Elimu, lakini lugha ya kiswahili iko kwa Mhe. Waziri wa Habari. Sasa Mhe. Spika, kichekesho kiliopo sasa hivi kwamba watu wengi wanavyofikiria nje kwamba Kenya ndio kwenye kitovu cha kiswahili, kwa sababu gani? kwa sababu Kenya wanatoa shahada ya kwanza, shahada ya pili ya kiswahili, sio kwamba mtu unafanya *education* kwenda kuchukua labda Kiingereza na Kiswahili aah! watu wanafanya *MA* ya Kiswahili katika vyuo vikuu vyao vya Nairobi. Sasa watu wengi nje wanafikiria kwamba shina la Kiswahili labda liko Kenya, lakini mtu wa Kenya akizungumza, *husema nakwenda kwa hospitali, nakwenda kwa sokoni* na huko ndiko watu wanakokimbilia wanafikiria kwamba Kiswahli ndio nyumbani kwao.

Sasa hili vile vile nashauri kwamba kwa sababu Mhe. Waziri kwa bahati nzuri yeye Kiswahili kiko katika Wizara ya Habari ndiye mwenye nafasi nzuri zaidi ya kutangaza nje, hii ndio faida ya lugha ya kiswahili kwamba Kiswahili kimewekwa katika Wizara ya Habari. Kwa hivyo kwa kutumia hii fursa kwamba Kiswahili kiko katika Wizara ya Habari basi hiki kiendeshwe sambamba na utalii, pale watu wanapokwenda kufanya *promotion* ya utalii basi vile vile panafanywa na *promotion* ya Kiswahili kwamba ieleweke ala! kumbe kiswahili nyumbani kwao kiko Zanzibar nafikiri haya yangelikwenda sambamba Mhe. Spika, watu wanafanya *promotion* ya utalii lakini wakati ule ule wanafanya na *promotion* ya Kiswahili kwa sababu wote ni wizara moja, nafikiri hakuna ubaya wowote kulifanya hilo na nafikiri pakiwa na mipango madhubuti Mhe. Spika, itawezekana.

Sasa Mhe. Spika, mimi sikuwa na michango mingi nilitaka nisisitize hilo la Hoteli ya Bwawani na narejea kutoa wito wangu kwamba Serikali pamoja na Baraza la Wawakilishi tujenge utamaduni wa kuitumia ile hoteli na mara nyengine tupumzike kwenda katika mahoteli yaliyokuwa sio ya serikali, labda pale itakapokuwa lazima Waheshimiwa wanataka kwenda shamba kupumzika aah! hilo na mimi naunga mkono kwenda kupumzika. Jengine nirejee tena wito wangu kukuomba Mhe. Spika, katika bajeti ijayo 2014/15 hebu tufanye huruma na sisi Baraza la Wawakilishi tuchangie chochote *ZBC* ili matangazo yetu yaende vizuri.

Baada ya hayo nakushukuru sana.

Mhe. Mussa Ali Hassan:Ahsante Mhe. Spika, nakushukuru kwa kuweza kunipatia nafasi hii kwa kuweza kuchangia bajeti hii ya Wizara yangu ya Habari, Utalii nikiwa Mjumbe wa Kamati hii.

Mhe. Spika, kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kuwa hapa kuweza kuichangia bajeti hii na kuipitisha kwa kura zote hasa kwa vile Mhe. Waziri, anajali sana Wizara yake pamoja na Watendaji wake.

Kwanza Mhe. Spika, nashukuru kwa kuweza kuchangia ukurasa nambari saba kuhusu sekta hii ya utalii. Kwa kweli nchi yetu imejikita sana na masuala ya utalii na hivi sasa ndio uti wa mgongo wa maisha ya nchi yetu kwa kuweza kuhakikisha utalii unaimarika siku hadi siku. Kwa kweli Mhe. Spika, nachukua nafasi hii kuweza kuipongeza sana sekta hii ya utalii kwa maendeleo ambayo tumeshafikia na kwa kweli ni kitu cha kutia mfano hatua ambazo tumeshazipata. Kwanza kwa kuchangia zaidi kuhakikisha kwamba aweze kuyashughulikia baadhi ya mambo muhimu ambayo Wizara hii ndio kichwa ambayo kitaweza kusaidia.

Mhe. Spika, kwanza Mhe. Waziri ahakikishe wawekezaji ambao wanawekeza katika sekta hii ya watalii kwanza wawe na uwezo wa kuweza kuwekeza hata kuweza kuwajali wananchi wetu wanapoweza kuuza vitu vyao katika mahoteli kwanza wahakikishe kwamba sekta hii ya utalii hawa wawezekaji wana uwezo wa kununua bidhaa kutoka kwa wananchi wetu sio kuwakopa kama wanavyoendelea hivi sasa. Kwa kweli wananchi wetu badala ya kuuza hvi sasa wanakopwa na wengi wao utakuta wananyang'anywa hawalipwi haki zao. Kwa hivyo Mhe. Waziri nataka hili atakapokuja anihakikishie hawa wawekezaji wanapokuja kuwekeza hapa Zanzibar angalau wanachekiwa *bank statement* zao za kuweza kuwekeza au wanakuja kukopa kwa wananchi wetu ndio wanaweza kuendesha hoteli zao. Sitoweka shilingi yangu ingawa ni wizara ambayo ninaiongoza katika Kamati kama hakunihakikishia kwamba utalii hivi sasa unawalipa wananchi wetu wote ambao unawakopa katika nchi yetu.

Vile vile Mhe. Spika, nitahakikisha kwamba Mhe. Waziri anihakikishie *foreigners* wanapokuja Zanzibar haiwezekani kwenda masokoni kwenda kununua bidhaa wenyewe, wananchi wetu wanafanya kazi gani na watapata ajira wapi ikiwa *foreigners* wenyewe tunawapa nafasi ya kwenda kununua papai kwa fedha za Tanzania, kama wananunua papai kwa fedha za kigeni hapo kweli. Kwa hivyo ni vigumu kumuweka muwekezaji kwenda mwenyewe katika masoko ambapo kwenda kununua bidhaa kwa fedha ambazo ni za Tanzania, ikiwezekana aweze kununua kwa fedha za kigeni ndio bidhaa hizo azipeleke hotelini. Kama si hivyo haiwezekani kuruhusiwa *foreigners* kuweza kufanya biashara yeye mwenyewe isipokuwa wananchi wetu ndio wahusika wakuu wa kuweza kununua vifaa na kuvikopesha katika mahoteli na katika kuwakopesha wahakikishe wanawekewa muda maalum wa kuweza kulipwa fedha zao ambazo walizokubaliana katika mahoteli.

Mhe. Spika, kwa kweli hivi sasa utalii unaimarika lakini kuna matatizo ya wawekezaji wengi ambao wanawekeza katika mahoteli hayo kwa kweli hawachukui mipango ambayo tulipanga Serikali ili kuwaajiri wananchi wa Zanzibar katika mahoteli yao. Wananchi wengi wa Zanzibar utakuta kwamba hivi sasa hawana ajira na utakuta tumejenga mahoteli ni mengi zaidi wananchi wa Zanzibar. Sasa sijui serikali inapata faida ambayo tuliyoikusudia, naomba Mhe. Waziri anihakikishie kwamba wananchi wangapi wamo katika mahoteli wa Zanzibar ambao wameshaajiriwa hivi sasa. Namuomba Mhe. Waziri akija anihakikishie kila hoteli anipangie idadi ya wananchi wa Zanzibar ambao wana nafasi muhimu katika mahoteli yetu. Utaona katika mahoteli yote makubwa wale ambao watu wanaohusika na mambo ya ajira katika mahoteli utakuta ni wageni hasa ni Wakenya, basi ingelikuwa angalau Watanzania tukalisema Watanzania wenzetu lakini naomba tu Mhe. Waziri kwamba vichwa vyote vya mahoteli waongoze Wazanzibari katika sehemu muhimu, ndio wachukuwe wageni badala ya zile nafasi za Wazanzibari ambazo labda hawaziwezi kuziongoza.

Mhe. Spika, nikiendelea zaidi naendelea na *ZBC*, kwa kweli Sauti ya Zanzibar hivi sasa inaendelea vizuri lakini ninashangaa sana utapokuta mwananchi au kiongozi yeyote hivi sasa kuweza kumlaumu muendeshaji vipindi katika *ZBC*. Mimi naona hakuna sababu ya kumlaumu Mkurugenzi kwamba anaendesha vipindi vibaya. Je, tukijiuliza Mkurugenzi tumemuwezesha katika vitu ambavyo vina umuhimu wa kuiongoza hii sekta. Kwa kweli mimi huwa nakwenda pale TV hata zile kamera za kuweza kupigia sehemu mpaka arudi muwekezaji mwengine ndio ichukuliwe kamera iende sehemu nyengine ya kazi, hapo ni vigumu kuweza kusema kwamba Mkurugenzi haiwezi hii sekta, Mkrugenzi huwezi kumlaumu kama humuwezeshi. Ni sawa sawa na majumbani kwetu mama humpelekei nyama wala humpelekei vitunguu ukalaumu kwamba hajui kupika, sasa utamlaumu vipi hawezi kupika wakati hukumtimizia. Kwa kweli leo sina zaidi ya kuchangia isipokuwa tu nitaunga mkono kama nitajibiwa masuala yangu ahsante sana.

Mhe. Spika: Mhe. Mussa nakushukuru na nawashukuru Waheshimiwa Wajumbe na hapa itakuwa ndio mwisho wa michango yetu nashukuru tumepata wachangiaji kama 20 wa kutumia *microphone* na kesho tukiingia kwenye majaaliwa tunamsikiliza Mhe. Naibu Waziri na baadae kumuomba Waziri atufanyie majumuisho.

(Saa 8.00 mchana Baraza liliahirishwa hadi tarehe 24/07/2013 saa 3.00 asubuhi)